ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
31.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe

32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini na Saba – Tarehe 07 Agosti, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka 2012/2013/

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati mezani Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2012/2013

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe jana tulipoondoka kwa kadri ya wachangiaji tuliokuwa nao tulimbakisha Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais ili aweze kuchangia. Sasa basi kwa sababu wageni bado hawajamaliza taratibu fulani hapa tukaweza kuwatangaza, tunaomba basi tuanze na Mhe. Waziri ili aweze kuendelea na baadae watakapofika wageni tutawatambulisha rasmi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninakushukuru sana kupata wasaa huu wa kuchangia machache kabisa katika hotuba hii ya Mhe. Nassor Ahmed Mazrui- Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kusema mengi Waheshimiwa wengi wamesema kuhusu maendeleo hii pamoja na mwenyewe Mhe. Waziri na mimi ninayaunga mkono yote, na ninaomba Waheshimiwa Wajumbe kama tulivyochangia basi tuipitishe hotuba hii, kwa sababu sote ni lazima niseme kwamba biashara sasa ni sehemu moja kubwa ya uchumi wetu nchini mwetu.

Kwa hivyo vikwazo vidogo vidogo, serikali imeweka utaratibu mzuri ingawa tunakwama ndio utendaji, unapofanya ndio unapoyaona matatizo. Kwa hivyo ninachotaka kusema kwamba serikali mengi haya mambo mwenyewe Mhe. Waziri atakuja kusema tutayafanyia kazi. Lakini na sisi kama Wizara inayosimamia vikosi kwa kweli hatutopendelea au hatutoacha mianya wazi kuona kwamba vyakula ambavyo vinaletwa nchini mwetu na vinasamehewa ushuru, halafu vinapelekwa nje kinyemela, vipelekwe nje kwa taratibu, iwe *real exported* na hiyo ndio dhana ya kisiwa chetu. Sera yetu ya biashara tokea siku za nyuma, *transit trade* hapa kisiwani petu bidhaa zinatoka nje zinakuja, zinakaa, zinasafirishwa lakini kihalali.

Sasa haitokuwa vyema kwamba vyombo vyetu, dola yetu ikae kuona chakula kinatiwa kwenye majahazi ambavyo vimekusudiwa kikitumike kwa wananchi wetu. Kwa hivyo ninavipongeza sana vikosi vyetu vya SMZ hasa KMKM kwa juhudi kubwa wanayoifanya kujaribu kukamata majahazi na vyombo vyengine ambavyo vinatorosha mchele, sukari, unga.

Mheshimiwa mmoja alizungumza kwamba waachiwe wakalipe kodi huko, kwa nini wasilipe hapa hiyo kodi na kama tuliwasamehe wakati huu mfano wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani, haitokuwa vyema watoroshe wao wakapate faida huko kwengine. Kwa hivyo mimi naomba sana wafanyabiashara tunawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini tutumie njia hizi zetu za kutupatia mapato tusikwepe mapato.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nichangie suala zima la uendelezaji wa zao la karafuu. Kuna Waheshimiwa Waasisi na wengine walizungumza suala la uendelezaji wa zao la karafuu, na ninakumbuka walifika kusema serikali ipo wapi, inafanya nini.

Niseme kwamba serikali ina mipango kabambe na mwenyewe Mhe. Waziri ataeleza hapa, lakini ninataka kusema tu kwamba utafiti wa karafuu nchini mwetu ulianza siku nyingi sana tokea wakati wa ukoloni, tokea miaka ya *thirties* huko na awamu ile ilikuwa zaidi kulenga kutafuta zao jengine mbadala ambalo lingeweza kusaidia uchumi wetu wa Zanzibar tusitegemee kama wataalamu wanavyosema *mono crop economy* au uchumi unaotegemea zao moja.

Kwa hivyo utakuta katika kituo cha Kizimbani mpaka leo pana mikakao, mibuni ipo, tulijaribu mpaka chai lakini tukafeli. Kwa hivyo utafiti wa wakati ule ukafa. Halafu utafiti mwengine wa awamu nyengine kujua chanzo cha maradhi ya mikarafuu, ilikuwa mikarafuu inakufa, hatujui tatizo lake, utafiti uliendelea.

Wakati huo tunatafuta chanzo cha matatizo ya mikarafuu basi ukaja sasa na sera hiyo hiyo ya kutafuta zao mbadala na vipi mkarafuu tuuendeleze. Kwa hivyo kazi kubwa sana ilifanywa katika vituo vyetu vya Matangatuwani, Daya ya Mtambwe kule, Kizimbani na kwengineko. Kazi kubwa sana ilifanywa na matokeo yalitoka.

Lakini *conclusion* moja kubwa ambayo naomba niikariri kwamba wataalamu ambao walikuwa ni Waingereza, walisema *for the next fifty years* kwa miaka mengine hamsini hawaoni zao jengine mbadala la fedha ambalo likachukua nafasi yake kwa Zanzibar, kwa zao ninasema.

Ukitizama kweli kwa sababu kwenye soko la dunia bei ya karafuu tokea wakati huo inapanda ikishuka, ile ndio *world trend* ndio ilivyo na si karafuu tu hata kahawa, chai na mengineyo. Kwa hivyo mazao yote haya mazao ya biashara wana hilo tatizo.

Sasa ninataka kusema kwamba ninashukuru kuwa tume-*diversify*, tumetanua wigo wa kuingiza mapato nchini mwetu. Labda kwa mazao niseme sasa mwani nao unajaribu ku-*compete* lakini bado tunaona zao la karafuu na hasa mwaka huu bei ilivyopanda ulimwenguni na wananchi wetu walivyoshughulikia na serikali imeweka mkakati maalum wa kulikuza zao hilo.

Sasa ninataka nisemee *point* moja kubwa sana ambayo Mhe. Nassor muasisi alizungumzia, suala la uendelezaji. Alitaja labda hatuwezi kuliendeleza kwa hizi *breeding practices* au hizi njia za ukuzaji za kisasa.

Ninataka kusema kwamba kwa *nature* ya zao la karafuu au mti wa karafuu na ugumu wake, *research* iliyofanywa siku za nyuma ime-im*prove* kwamba ni vigumu sana zaidi ya kutumia ile tunayoita mbegu, kwa kutumia njia nyengine labda kama mfano kwa kutumia *cuttings* au kwa kutumia *marcottings, layerings, craftings*. Njia hizi labda tunaweza kutumia kwenye michungwa, miembe na mengineyo tunaweza lakini kwa mkarafuu imekuwa ni vigumu sana.

Sasa kwa nini imekuwa ni vigumu, imekuwa vigumu sababu kubwa iliyoelezwa ni tatizo wanasema ni *arithmatic activity* ya mkarafuu. Pale unapofanya labda mfano *marcotting au cutting*, unataka mizizi itoke. Sasa mule kwenye *tip* zake ile mizizi itoke kwa rahisi, sasa kwa mkarafuu kidogo ni mgumu sana, ndio *research* zimetuonesha hivyo na *literature* ndio inavyosema.

Sasa hiyo ninataka kuwajuulisha Waheshimiwa kwamba hii kazi imefanywa na sio kama haikufanywa, na sio kama serikali maana yake imelidharau hili suala. Lakini ni wazo zuri kwamba labda sasa *findings* hizo zilitumika wakati huo, jee ndio *research*, sasa wakati huu jee, tunaweza kujaribu.

Sasa imeonekana labda mfano kwa kutumia *layerings na approaching crafting* kwenye mpera. Unajua mpera uko kwenye *family* moja na mkarafuu na mzambarau. Labda kwa kutumia njia hiyo, labda wanasema maana yake hao waliotafiti mafanikio yao labda ni asilimia mbili katika mia walipata.

Basi ndio wanaweza labda kufikiriwa tunaweza tukapata lakini ule ugumu wa mkarafuu wake, maana yake mkarafuu ni mti laini sana na siku zote tunazungumza, ukipanda mikarafuu mia basi ukipata hamsini tu, usiseme sabini, ukipata hamsini katika mia msimu umekwisha wewe ni mwanamme, wewe kwa kweli umejitahidi ni mkulima mzuri sana.

Lakini tunashukuru hivi sasa baada ya kupata haya mapendekezo ya kilimo hasa wakati mkarafuu upo mchanga upate kivuli, upate mbolea wakati upo mchanga basi kidogo unapata alau sabini, lakini kupata tisini mpaka mia, huyo kafanya maajabu makubwa sana. Lakini inawezekana tukifuata hizi *agronoming practices* zilizopendekezwa tunaweza.

Sasa ninataka kusisitiza tu kwamba si kama serikali haya haiyajui, wataalamu tupo na wengine tumekuwa wanasiasa lakini bado utaalamu upo ndani ya mikono yetu na ule haufutiki na wengine tulishiriki kikamilifu katika hizo *research* zilizofanywa. Bahati mbaya Mhe. Ali Juma Shamuhuna hayupo hapa lakini ninataka kusisitiza tu kwamba tunaposema kwamba serikali haifanyi kitu aah! Si kweli. Haya yamefanywa na yataendelea kufanywa na tutazidi kupata na kuweka fedha nyingi kuona kwamba tunalirahisisha zao zetu la karafuu.

Mfano mmoja nitatoa tulijaribu hata kutumia *hormones* ili tuone mikarafuu baada ya kwenda kuwa mikubwa basi ifanywe iwe mifupi ili uweze kuchuma kwa ngazi tu, mpaka utafiti huo tuliufanya na ikaonekana kwamba hizo *hormones* utatumia ngapi, halafu na *pollution* iliopo siku hizi tena, uharibifu wa mazingira, uharibifu wa ardhi ikaonekana kwa kweli haiwezekani kabisa.

Kwa hivyo tukaacha kazi hiyo ya *hormones* tukaona mkarafuu uachiwe uendelee ipasavyo. Lakini kubwa jengine ambalo utafiti unasema kwamba kwa njia ya kuuendeleza mmea wowote au zao lolote, njia ni *selection* na *breedings* ndizo zinazotumika sana.

Sasa mfano sote hapa tuliopo kwenye ukumbi huu Mhe. Mwenyekiti, tungekuwa tuna tofauti kati yetu, tuna *variability*, sasa sisi tunalenga mtu ambaye ninatoa mfano labda mwenye uzazi mzuri au mrefu kidogo ndio sifa nzuri, ninatoa mfano tu. Sasa zile tofauti zile tungezichukua na ndio tunachagua kile kilicho bora tunakiendeleza.

Sasa kwa mkarafuu imeonekana ile kabila ya mkarafuu yote ni moja, hakuna tofauti katika kabila mbali mbali. Labda mfano mgomba kuna kabila chungu nzima, kama mtwike, mkono na nyengine, kwa hivyo *with in genes* unaweza uka-*cross*, lakini kwa mkarafuu hakuna tofauti yoyote. Yaani mkarafuu wote umetokana na *genes type* moja. Hiyo ndio sababu nyengine kubwa sana kwamba mkarafuu unashindwa kuendelezwa kwa njia hizi za kisasa ambazo Mhe. Nassor muasisi alitaka labda zingetumika kwa kazi hii.

Kwa hivyo haya mambo yanajulikana na yameshafanyiwa kazi labda sasa hivi tuwashajihishe watendaji wetu wazidi kuendelea kuzidi kutafiti zaidi hayakuachwa kabisa. Kwa kutumia miti hii ya asili ambayo ni *family* moja, sasa inashauriwa labda turudi huko Malakasi ambako mkarafuu ulikotokea tukatafute mikarafuu mengine ya asili au iko mwitu, kwa mfano yapo mananasi mwitu.

Sasa kama ipo kule tukatafute basi mikarafu hiyo ya asili mengine labda tunaweza tukapata *genes type* au kabila jengine, sasa tuje tu-*cross* na mikarafuu yetu. Lakini jengine pia huu mkarafuu una tatizo mengine. Mkarafuu mara nyingi nyuki ndio wanafanya *breeding* lakini utafiti umeonesha ukishafanyika na kama mwenyewe unataka nyuki asifanye, ukafanye mwenyewe kama mahindi wanavyofanya au mitama au zao jengine, ukifunika vile unaona vifuko vyeupe basi havikai vyote vinapuputika. Ndio huo ugumu mwengine.

Ndio maana wazungu wanasema mkarafuu kuwa *“is a unique crop”,* yaani yale mambo yake kidogo mengi magumu sana. Lakini tunashukuru sana kwa hali ya hewa ya kwetu Zanzibar ukilinganisha na Indonesia, Brazil, sisi tunashukuru Mwenyezi Mungu katujaalia zao letu hili, jua liliopo na *temperature* iliopo inakua vizuri, halafu pia tunaweza kuianika vizuri na tukauza vizuri.

Hayo ndiyo wanayoshindwa Indonesia sasa. Ndio maana mpaka leo wanazitegemea karafuu zetu. Kwa hivyo ninataka kusema kwamba Mhe. Mwenyekiti, haya mambo yalifanyiwa utafiti muda mwingi, yapo na sasa labda pengine kipindi kikubwa na sasa zimekuja *methodology* nyengine mpya mpya za kutumia *marcotting*, *cutting* na *breeding*.

Labda sasa tuanze kwa huko lakini huko nako kunataka vifaa na utaalamu mkubwa sana. Utaalamu ninaamini tunao, labda vifaa tu vya *by take* tuone kama tunaweza tukaanzia huko. Mhe. Mwenyekiti, nimeona nilisisitize hilo tu.

Sasa nimalizie mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzungumza kidogo tatizo la Darajani ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa mmoja au wawili na wengineo. Mhe. Mwenyekiti, tunachosema kwa Darajani sisi serikali hatuna matatizo na wananchi na ningeomba sana tusilete kidogo hali ya kubaguana.

Nimemsikia Mheshimiwa mmoja alizungumza Wapemba wananyimwa pale, wanabaguliwa, wana nini, kwa kweli lugha ile ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, tusirudi huko, hatupendi kabisa kuzungumza Upemba, Utumbatu, Ubweleo, Udimani au uwapi.

Wafanyabiashara wa Darajani ninaamini si wa Pemba tu wote, kuna Wamachinga pale hatujui wanatoka wapi na ni wengi tu. Kwa hivyo kwa kweli lugha ile Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Waheshimiwa tusiende huko. Pale kinachotumika tunajaribu kuuweka mji wetu katika mpango. Hakuna mji usiokuwa na mpango.

Mhe. Mwenyekiti, leo ninaomba ukimaliza tu hapa wewe mwenyewe weka gari yako ukapite tu kwa miguu mule utaona, mule tulimuweka wafanyabiashara sasa watu wanakuja barabarani, wewe unaposimama unanunua kitu vespa inakubeba hapo hapo, ukifanya mchezo gari itakupita hapo hapo. Zile njia zote tumezifunga.

Sasa mji huo ni mji gani jamani. Mhe. Mwenyekiti, kila mji lazima una mipango, una taratibu. Sasa Manispaa haina lengo hata kidogo la kuwabughudhi hao wanaosemwa Wapemba aah! Lugha hiyo kwa kweli si nzuri na ningeomba sana wenzangu tusielekee huko, Manispaa haina ubaguzi huo.

Ndani ya Manispaa hayo yanayosemwa Wapemba wamo tele wafanyakazi. Sasa kwa nini tuwashutumu hivyo. Mimi ninafikiri cha kufanya sote tuzingatie maelekezo ya Manispaa. Mwahala kumewekwa wale wafanyabiashara waende Saateni. Mhe. Hamza kazungumza vizuri utaratibu umeandaliwa. Lakini sasa Saateni wamekwenda wengine wanarudi na wale wale wafanyabiashara waliopo pale Darajani wana umoja wao na wao wakatuandikia wizarani, jamani mutasaidie serikali.

Sisi kwa kauli moja tumeamua kwenda Saateni lakini wenzetu naona wanarudi. Sasa na sisi turudi huku Saateni tuhameni. Sasa tumewanasihi wale wanaouza mule tumewaomba, tumekwenda kidogo tumeweka matofali mule, wengine wanatandika bidhaa mpaka mule kwenye madirisha yao kusoma hawawezi. Baada ya kuwaambiwa hivyo kidogo wakasogea mbele.

Sasa kidogo haipendezi hakuna nchi yoyote isiyokuwa na taratibu au isiyokuwa na mpango, sote tunasisitiza umuhimu wa mji wetu wa kuwa safi, kuwa na mipango ili watalii waje lakini tukienda shaghala baghala kama hivi, ninafikiri hatutopenya. Hilo suala munalotuhimiza kutwambia kwamba tudumishe usafi haufanyiki.

Mimi ningeomba sana Waheshimiwa tusaidiane. Sasa sisi ndio wenye wananchi tuwashauri wafuate taratibu na sheria ziliopo. Cha kufurahisha zaidi Mhe. Spika, wale wenyewe wafanyabiashara wa Darajani baada ya kuona ule mzozo wa siku nyingi wa makontena na nini, wakaja na wazo kwamba wajenge *supermall*.

Lijengwe *mall* kubwa pale kama Dar es Salaam lile Machinga Complex. Sasa hilo ombi wamelileta serikalini na serikali tunalizingatia. Lakini tayari unajua kuna *master plan* ya mji wetu na Darajani pale kuna *master plan* yake iweze Darajani. Sasa serikali hilo ombi haijalitupa inalizingatia tutaona hilo *mall* linaweza likafanywa pale au kama likajengeka pale lakini kama halijengeki tukalijenge wapi, unaona wafanyabiashara wenyewe wa Darajani ndio walioleta ombi hilo serikalini.

Sasa cha kuelezea tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba tumeona kuwa kweli soko lile limezidiwa na kama nilivyosema sasa hivi kwamba ukienda katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani ndio hali utaiona zaidi. Lakini pia niseme Baraza la Manispaa limekuwa *very flexible*, tumeona aah! Hivi sasa kila mmoja anatafuta siku kuu ya Iddi tuachie

hivyo hivyo, tujaribu tu watu wa *traffic* tuwaombe gari wasimamie gari ziende taratibu wavuke lakini hali ukipita pale utaiona Mhe. Mwenyekiti, mwenye samaki wake anapara hapo hapo anatoa matumbo hapo hapo. Yale kila siku ambayo munayotuhimiza hapa ndio yanayofanyika, almuradi kwa kweli ule utaratibu na mpango haupo.

Sasa mimi nimefurahi sana hii *idea* waliyotuletea wenzetu wafanyabiashara wa umoja wao kwamba tukae pamoja tufikirie kujenga *mall* pale. Sisi hii *idea* tumeipokea serikalini na tutaifanyia kazi tuone vipi tutaifanikisha, kama si kubwa la ghorofa mbili tatu tunaweza tukasogeza mbele na tunashirikiana na Wizara zetu mbili; Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tumeunda *technical committee* na inafanywa hivyo kitaalamu kujua wafanyabiashara wale ku-*survey* wapo wangapi na wanauza nini na tuwagawe vipi. Kwa hivyo hilo suala linashughulikiwa kitaalamu ninataka kusema.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja na naomba sana Waheshimiwa wenzangu tumsaidie sana Mhe. Waziri tuipitishe bajeti ili aweze kutusaidia kuendeleza sera nzuri ya biashara hapa nchini kwetu. Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri kuna maelekezo hapa ya serikali ambayo yameletwa. Na haya yanahusu juu ya mchango ambao ulitolewa katika Wizara ya Kilimo kwenye suala linalohusu shamba la Wingwimapofu.

Hati inayohusu shamba lile imeletwa hapa kwa utambulisho kwamba shamba lile limemilikiwa kihalali pamoja na ramani yake. Kwa hivyo naona yule muhusika mkuu bado hajafika lakini nilitaka kutoa taarifa hii ili Ndugu Wajumbe muweze kufahamu.

Sasa atakapofika kwa sababu aliomba kuona hati hii ipo tayari kwa sababu ya kuja na kuweza kuiona hati husika.

Baada ya maelekezo hayo sasa tumuombe Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ili afanye majumuisho. Mhe. Waziri karibu. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: *Bismillahi Rahmani Rahiym*. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe binafsi kwa namna ambavyo umeendesha kikao hiki kwa umahiri mkubwa kuanzia jana mpaka hadi hii leo.

Vile vile ninapenda kuchukua fursa hii adhimu kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa wote waliochangia bajeti hii. Tunaithamini sana michango yao imetupa miongozo ya utekelezaji wa malengo yetu tuliyojipangia na utekelezaji wa kazi za kawaida kwa mwaka 2012/2013.

Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza lako Tukufu wametoa hoja zao nzito kwa hekma na busara kubwa. Waheshimiwa ambao wamechangia ni 17 na waliochangia kwa maandishi ni 5.

Mhe. Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kukushukuru kwa namna ya kipekee, pia kwa kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Mhe. Salmin Awadh Salmin pamoja na Makamo wake na Wajumbe wake wa Kamati yake kwa hotuba yao nzuri, yenye kutoa dira, mwelekeo, miongozo na maelekezo ambayo yatasaidia sana katika utekelezaji wa bajeti hii. Tuna hakika katika Baraza hili kuwa miongozo yote inayotolewa tutatekeleza kwa vitendo.

Vile vile ninaomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili kwa kuunga mkono hoja ya makadirio ya mapato ya matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda Masoko kwa mwaka wa fedha 2012.2013.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwataje Wajumbe wote waliochangia katika bajeti yangu kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Abdalla Mohamed Abdalla - Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo.
2. Mhe.Salmin Awadh Salmin
3. Mhe. Mohamedraza Hassanali
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
5. Mhe. Hija Hassan Hija
6. Mhe. Saleh Nassor Juma

7. Mhe. Asha Bakari Makame
8. Mhe. Mussa Ali Hassan
9. Mhe. Hamza Hassan Juma
10. Mhe. Nassor Salum Ali
11. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
12. Mhe. Salum Abdalla Hamad
13. Mhe. Fatma Mbarouk Said
14. Mhe. Subeit Khamis Faki
15. Mhe. Ashura Sharif Ali
16. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
17. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini (Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
2. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
3. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
4. Mhe. Panya Ali Abdalla
5. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

Awali ninamshukuru sana Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame kwa namna alivyoweza kufafanua mambo mbali mbali ambayo kwamba yatanisaidia sana katika uchambuzi wa majumuisho yangu.
Mhe. Mwenyekiti kwa jumla tumepokea mawazo ya Wajumbe mbali mbali kuhusu bajeti hii na naomba kufanya majumuisho kama ifuatavyo:

Mheshimiwa nimewataja wote waliochangia sasa hivi nitakwenda moja kwa moja kwenye hoja juu ya hoja na hoja ndani ya hoja. Hoja ni nyingi nimejaribu kuziorodhesha zile za muhimu sana ili zipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa kuna hoja ya mwanzo ya uidhinishaji wa fedha za ziada za shilingi milioni mia mbili na hamsini na tano. Fedha hizi ni fedha zilizoongezwa na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kugharamia marekebisho ya mishahara kwa wafanyakazi wa serikali. Pesa hizo zimetolewa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Fedha hizi kila wizara imepata mpaka kwenye Baraza letu la Wawakilishi. Na fedha hizi zimeidhinishwa na Baraza letu tukufu kupitia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha, alikuwa anajua kuwa mishahara itaongezwa na akaliweka fungu na makisio hayo yakaidhinishwa.
Wizara yangu mimi ambayo ina *transparency* ndio maana ikaoneshwa dhahiri kwamba kiasi gani cha fedha kimeongezwa kwa ajili ya ongezeko la mishahara. Lakini serikali nzima mawizara yote wameongezwa fedha kwa ajili ya ongezeko la mishahara sio Wizara ya Biashara tu. Kwa hivyo napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba kwa sababu ya *transparency* ya wizara yangu ndio inaonesha kima halisi cha ongezeko la mishahara kutokana na mishahara mipya iliyotangazwa na serikali.

Hiyo ndio ilikuwa utumiaji wa fedha za maendeleo Tanzania shilingi milioni mia mbili, fedha hizi zilitumika kuwasaidia vikundi vya wajasiriamali wadogo wadogo kuwapatia mafunzo, na kuwasaidia. Kwa mfano wamepata mafunzo wajasiriamali mbali mbali, tumepeleka umeme katika kiwanda cha dagaa Ndagoni wakati walikuwa hawana umeme na wakipata matatizo. Vile vile tumewasaidia vifaa vya uwekaji wa samaki katika vijiji vya Ndagoni. Vile vile tumesaidia kiwanda cha dagaa Nungwi, vile vile tumetumia fedha nyingi kwa kujenga banda la maonesho ya kitaifa ya Sabasaba hapo Dar es Salaam.

Pia tumesaidia kuwapeleka wafanyabiashara wadogo wadogo kwenda kuonesha bidhaa zao katika mabanda ya Sabasaba Dar es Salaam. Pesa nyingi sana zimetumika katika maonesho. Milioni hamsini zimetumika kwa kutengeneza banda la maonesho na milioni arubaini zimetumika kwa kuwapeleka wajasiriamali kwenda kuonesha bidhaa zao Dar es Salaam. Kwa hivyo milioni 90 peke yake zimetumika katika mabanda ya maonesho ya Sabasaba na nyengine zimetumika katika Kiwanda cha Dagaa cha Nungwi, Kiwanda cha Ndagoni cha dagaa na mafunzo mbali mbali ya wajasiriamali. Kabla ya mjasiriamali kumpeleka kwenye maonesho lazima umpe mafunzo ya bidhaa zake namna ya kuzi-*pack* na namna ya kwenda ku-*present.* Kwa hivyo fedha zote hizi zimetumika na hazikutosha kwa sababu wajasiriamali ni wengi lakini waliopelekwa ni kidogo kutokana na Mfuko uliokuwa ni mdogo.

Kifungu cha 220509 Ada ya Ushauri ya shilingi 38 milioni kwa Idara ya Mipango na Sera, fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kumtafuta mshauri mwelekezi kwenye mapitio ya sera ya biashara. Sera ya biashara ni kusema kwamba imeshapitwa na wakati na sasa hivi ndio inafanyiwa marekebisho. Kwa vile ni suala gumu kabisa lazima tutafute mshauri ambaye atakuwa na sifa ya kufanya kazi hii, na kima cha fedha hizi zilizotengwa kwa ajili ya kumpata mshauri huyo aweze kushauri serikali namna gani ya kuja na sera ya biashara ambayo itakidhi haja katika huu wakati tulionao. Kama ndugu yangu Mhe. Mohamedraza alivyosema kwamba biashara ni kiuno cha uchumi wa nchi hii.

Halafu nikija katika kile kifungu cha 220517 Utafiti wa Bajeti kuna ziada gani kwa Idara ya Mipango na Sera. Mhe. Mwakilishi fedha hizi ni kwa ajili ya utafiti wa bajeti pamoja na utoaji wa mafunzo ya maafisa wa wizara katika mfumo mpya kuhusu utayarishaji wa bajeti, *program base budget* pamoja na masuala yanayohusiana na utayarishaji wa mipango (*planning*).

Kwa hivyo kwanza hapa kuna suala la mipango na nyengine ni *program base budget.* Huu ni mfumo mpya ambao unataka utolewe taaluma ya kutosha, kwa hivyo fedha hizi zimewekwa kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi ili kutengeneza mipango pamoja na kutengeneza hiyo *program base budget*.

Kifungu 220601 shilingi 20 milioni Idara ya Viwanda. Mhe. Mwakilishi kama tunavyojua kwamba wizara yetu kwa pale mjini ina majengo manne, kwa sasa hivi tumetimiza majengo mawili, jengo lile ninalokaa mimi na jengo la pili ilikuwa zamani anakaa Mkuu wa Wilaya ya Mjini. Jengo hili sasa hivi limekarabatiwa kwa fedha nyingi sana.Jengo ambalo sasa hivi kama ni jipya na linahitaji *furniture* mpya na kila kitu kipya. Kwa hivyo fedha zilizotengwa hapa shilingi 20 milioni ni kidogo kutokana na jengo lilivyo na tunataka kuwaajiri *graduate* 15 ambao watakuwa wanafanya kazi katika jengo hili, tunataka *furniture* mpya, tunataka makapeti mapya, mapazia mapya. Kwa hivyo kwa kweli fedha hizi ni kidogo sana, lakini ndio *ceiling* yetu ilivyoturuhusu kufikia hapo. Mwaka jana ilikuwa kuna chumba kimoja lakini sasa hivi ni jengo zima ghorofa mbili *plus ground*.

Kifungu nambari 220300 shilingi 71 milioni Gharama za Safari Idara ya Mishahara. Fedha hizi ni kwa ajili ya kushiriki mikutano ya kikanda ya Afrika Mashariki *SADC* pamoja na kimataifa ikiwemo *World Trade Organization (WTO)* pamoja na kushiriki katika maonesho ya kimataifa ya biashara. Fedha hizi ni haba tangu mwanzo lakini vile vile kuna mkato unakuja kutoka Wizara ya Fedha, kwa hivyo kifungu hiki cha shilingi 71 milioni huenda likarejea lile lile fungu kama la mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tumsaidie Mhe. Waziri jana alisoma sana usiku, kwa hivyo sauti yake kidogo imepungua, sasa na sisi tukizungumza zile jawabu zitakuwa hazipatikani vizuri. Naomba tuwe wastahamilivu. Ahsante Mhe. Waziri endelea.

Kifungu Nam. 21110 fedha hizi ni kwa ajili ya posho la mafuta, posho la utumishi Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, simu kwa viongozi wa wizara, posho la matibabu, Katibu Mukhtasi, Madereva wa viongozi, wahudumu, makarani, masjala ya siri, posho hilo lipo kwa mujibu wa muongozo wa utumishi. Kwa hivyo, hii imetoka juu sisi tumeliingiza kwa mujibu wa toleo la serikali.

Halafu kuna ongezeko la fedha za safari kwa mwaka 2012 kutoka shilingi 59 milioni hadi kufikia 101 milioni kwa mwaka 2012. Fedha hizi ni kwa ajili ya safari za viongozi wa wizara katika ushiriki wa vikao vya kikanda, kimataifa pamoja na maonesho ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka uliopita kuna vikao vitano mimi sikuhudhuria kutokana na ukosefu wa fedha za kwenda katika safari za nje. Hata hivyo, fedha hizi zitakatwa kutokana na agizo lililotoka Wizara ya Fedha.

Fedha za Ruzuku kwa Mamlaka ya Vipimo na Kamisheni ya Ushindani wa Kibiashara, sheria hizi bado hazijafutwa na zinaendelea kufanya kazi kama ni sheria Nam. 4 ya mwaka 2003 ya mizani na vipimo na sheria Nam. 2 ya kumlinda mtumiaji. Kutokana na sheria hizo basi, kazi zitakazofanyika kufanya ukaguzi wa mizani kuhakikisha usahihi wake, kufanya ukaguzi wa vipimo vya mafuta na matenki ya mafuta, kufanya ununuzi wa vifaa vya ukaguzi wa mizani, kutoa mafunzo kwa wafanyakazi, kusimamia maendeleo ya biashara na ushindani, kumlinda mtumiaji, bidhaa na huduma na kuangamiza bidhaa zilizokwisha muda na zisizofaa kwa matumizi ya mwanadamu. Kwa hivyo

Mhe. Mwenyekiti, bado sheria hizi zinataka kutekelezwa na ruzuku hii katika ushindani inahitajika fedha hizo lazima tupate kufanyia kazi hiyo.

Kifungu nambari 220107 Ununuzi wa Kanda za Kurikodi Santuri kutoka shilingi milioni mbili hadi shilingi milioni kumi. Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu cha santuri ni *code* tu, lakini hapa kuna mambo mengi sana, kuna mambo ya kamera na mambo mengine ya kurikodi mambo mengi tu na *CD* na mambo kadhaa wa kadhaa.

Kulingana na muundo mpya ambao umeanzisha kitengo cha habari na mawasiliano *ICT*, fedha hizi zimewekwa kwa ajili ya kuimarisha kitengo hicho ikiwemo kununulia vifaa vya habari na mawasiliano. Kwa hivyo hapa *code* ni santuri lakini ni kukiimarisha kitengo cha mawasiliano katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa ndio utakuta shilingi milioni kumi ni fedha kidogo sana kwa shughuli za kibiashara ambazo zinataka zitoe habari kwa wingi kwa wananchi na kufanya biashara ili waelewe vipi biashara inavyoendelea na uchumi vile vile unaendelea katika nchi yetu.

Kifungu nambari 21118 Mazingira Hatarishi, hili posho la malipo kwa ajili ya walinzi wa wizara ambao wanafanya kazi usiku. Halafu kupata maelezo ya hatua iliyofikiwa kuhusu mkataba wa kuimarisha sekta ya mwani, mazao ya baharini na chumvi. Fedha hizo ziliwekwa kwenye makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na maelezo yake yashatolewa wakati wa bajeti yake. Kwa hivyo, hii wizara yangu ni wizara mtambuka ambayo yanahusisha wizara nyengine. Kwa hivyo, fedha hizi zinahusisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi na maelezo yake yametolewa katika ile bajeti iliyosomwa katika Wizara ya Uvuvi.

Sasa tunakwenda katika hoja nyengine ni hoja ya Shirika la Taifa la *ZSTC*. Waheshimiwa Wawakilishi wengi walichangia katika suala la *ZSTC* na wametoa lawama nyingi sana kuhusu shirika hili.

Waheshimiwa mnakumbuka mwaka jana hapa tulikuja tukaeleza habari ya Shirika la *ZSTC*, kwamba shirika hili linahitaji lifanyiwe mageuzi makubwa. Sasa unapokuwa wewe umeshanunua kitambaa chako cha nguo kizuri tu, ukimpelekea mshoni ukimuangalia namna anavyo kikata utakasirika hapo hapo. Vipi wee kitambaa hiki nimenunua fedha nyingi sana wewe unakipigapiga mikasi, ndivyo mlivyofanya ndugu zangu Wawakilishi. Shirika tunaligeuza kutoka hali iliyokuwa mbaya kuja katika hali nzuri nyinyi mnanung'unika, mnasikitika kwamba mbona hili shirika linakwenda hivi, mbona mnaingilia kati, mbona halipumui, mbona halituti. Hili shirika linataka mageuzi na serikali kwa makusudi na kwa dhati kabisa imechukua hatamu ya shirika hili kuligeuza ili liweze kuwa shirika madhubuti litaloweza kufanya biashara bila ya kuyumbayumba, na kwamba serikali imeweka wazi kuwa zao la karafuu ni zao la taifa, zao la karafuu halitobinafsishwa, ndio maana ikabidi lazima shirika hili lipewe meno na nguvu liweze kufanya kazi zake.

Kwa hivyo, sheria ya *ZSTC* ikaletwa katika Baraza hili na ikapitishwa na mageuzi ya shirika yanaendelea na alhamdulillahi nataka niwambie ndugu zangu Wawakilishi nyote na wananchi kwamba; shirika hili sasa hivi linajengwa katika misingi madhubuti ya nguzo za zege ili liweze kufanya biashara nyingi tu hususan biashara ya karafuu. Kwa hivyo, ningeomba ndugu zangu Wawakilishi muwe na subira msigeuke yule aliyenunua kitambaa akampelekea mshoni alipoona mshoni kitambaa anakitia mkasi akaanza kupiga kelele. Ukiona kitambaa chako kinapigwa mkasi ustahamili ndio mshoni anakikatakata akisha atakiunga utapata suti rasmi au utapata nguo rasmi. Ukianza kumshika mkono huyo mshoni usikate kitambaa changu hatoshona suti yako vizuri. Kwa hivyo nawaomba ndugu zangu Wawakilishi msitushike mikono tuachieni turekebishe, tuliunde Shirika la *ZSTC* madhubuti litakaloweza kuhimili mikiki ya kibiashara na kufanya biashara vizuri.

Ni kweli Waheshimiwa kabisa sheria ya *ZSTC* hapa imepitishwa lakini bado haijaanza kutumika, sheria ile Mhe. Rais ameshaweka saini lakini mimi Waziri sijaitangaza katika Gazeti Rasmi mpaka pale nitakapotangaza katika gazeti hilo ndio sheria ile itaanza kutumika, na sheria ile itatangazwa karibuni baada ya kumaliza misingi ya marekebisho na mageuzi. Mimi Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko nitatoa tamko la kuitangaza sheria ile katika Gazeti Rasmi la Serikali na kuanzia siku hiyo ndio sheria hiyo itaanza kazi zake. Matarajio yangu na nakuahidini hapa mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba sheria hii nitaitangaza rasmi katika Gazeti la Serikali si zaidi ya mwezi mmoja kuanzia tarehe ya leo. Kwa hivyo basi, mara tu baada ya kuitangaza sheria hii moja kwa moja tutatangaza bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la *ZSTC*.

Kwa vile natoa ahadi mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba haitozidi mwezi mmoja kuanzia leo *ZSTC* itakuwa ina bodi yake na itafanya kazi zake bila ya kuingiliwa na mtu yeyote itaachwa ipumuwe. Lakini kabla

ya hapo sisi tunakubali lawama kwa sababu ndio fundi lazima upige mikasi, ukatekate, upige bandi, ushone, tunataka shirika madhubuti, shirika ambalo litaweza kufanya kazi zake kitaalamu na kwa mujibu wa taratibu za kibiashara.

Vile vile imetoka hoja hapa kwa nini wametoka watu kwenda nje kutafuta masoko ya kuuza karafuu mkawaingilia. Mhe. Mwenyekiti, hilo nataka niliweke wazi kabisa, *ZSTC* tunaifanyia mageuzi na moja katika mageuzi ni kubadilisha *mind set* za wafanyakazi wa *ZSTC.*

Serikali iliwatuma waende nchi za nje wakatafute masoko au bei ya kuuzia karafuu, serikali inataka kujua karafuu mwaka huu wa 2012/2013 tutauza kwa kiasi gani katika masoko ya dunia na tutanunua kiasi gani kutoka kwa wakulima. Kwa hivyo, walioagizwa kwenda nchi za nje walipewa kazi moja tu hawakupewa kazi mbili, walipewa kazi ya kwenda kutafuta bei ya kuuzia na kushauri bei ya kununulia karafuu. Kwa hivyo, ikiwa wamekwenda kule wakaanza kuuza karafuu hilo halikuwa agizo la serikali, na mimi kama Waziri muhusika wa wizara hii sitokubali katu kuwaacha watendaji wakafanya kazi wanavyotaka wao, lazima wafuate misingi ya sheria na wafuate agizo la serikali. Niko *very strict* wala sitokubali kuendeshwa na watendaji, lazima watendaji wafuate sheria na wafuate maagizo ya serikali sio wafanye wanavyotaka wao.

Kwa hivyo mimi nimechukua hatua ya kuzuia mauzo yoyote mpaka pale itakapokuja ripoti serikalini inayoeleza bei ya karafuu duniani tupange bei ya kuuza na bei ya kununua karafuu kutoka kwa wakulima, hapo ndio tutaruhusu kuuza karafuu, vyenginevyo si Waziri mimi nitakaechezewa chezewa.

Ununuzi wa Karafuu. Karafuu zimezuiwa kuuzwa kwa mujibu wa kanuni inayozungumzia uanzaji wa msimu wa hivyo vituo vya ununuzi vitafunguliwa. Tunaahidi kwamba baada ya siku tatu kuanzia leo vituo vya karafuu vitafunguliwa rasmi na karafuu zitanunuliwa rasmi. Tuliowatuma wamesharudi kutoka nchi za nje na wamekuja na bei ya kuuza karafuu, tutakaa kitako tutajadiliana serikali kuona kwamba mkulima apewe bei gani, pale pale asilimia 80 ya bei tutakayouzia karafuu ndio atakayolipwa mkulima. Kwa hivyo, kuanzia leo katika kipindi cha siku tatu tutatangaza rasmi bei ya mkulima ya kuuza karafuu zake *ZSTC* na vituo vya kununulia karafuu vitaanza kufunguliwa. Sio vyote kwa mule ambamo karafuu ziko tayari tutavifungua. Sasa ndugu zangu Wawakilishi nipeni muda huo wa siku tatu tu kazi hii itamalizika.

Vile vile Shirika la *ZSTC* limo katika kipindi cha mageuzi, hivyo katika kipindi hicho tusitarajie kama kutakuwa na kupumua pumua. Hili itabidi liangaliwe kwa macho mawili ili lifanye kazi inavyotakiwa kwa mujibu wa masharti tuliyowawekea.

Jengine tumepata hoja hapa ukaushwaji wa karafuu kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Ukaushwaji wa karafuu duniani kote unafanywa kwa kutumia jua, kwa njia nyengine yoyote ile karafuu ukiikausha inapoteza uhalisia wake. Naomba Waheshimiwa Wawakilishi mwaka jana tumeletewa suala hili hili na mwaka huu suala hili hili. Mimi nashangaa sana kwamba tunasema bwana karafuu ukizikausha kwa njia yoyote ile inapoteza uhalisia wake, kila kitu kina *aroma* zake, unapoanza karafuu kuichakachua itapoteza ladha yake na harufu yake. Naomba sana yule ambaye anakuja na hoja hii aje na vielelezo vyake kwamba kaona nchi gani duniani inakausha karafuu kwa kutumia *radiation* au kuzikaanga au kutumia njia nyengine, lakini sisi tumefanya utafiti dunia nzima hakuna hata mtu mmoja ambaye anakausha karafuu kwa kutumia njia nyengine, kuna hatari sisi tukafanya mambo hayo tukapoteza hadhi ya karafuu zetu.

High breed ni karafuu, utafiti ulifanyika hapo zamani Zanzibar, ulifanywa hapo Kizimbani na kubainika kuwa karafuu zinapoteza uhalisia wake. Wako watu sasa hivi karafuu wamezitia mbolea nyingi zizae kwa wingi, lakini karafuu za Zanzibar ni *organic spice. Organic spice* zina bei kubwa kuliko mkarafuu unaoutilia mbolea za chumvi na mbolea za kemikali. Kwa hivyo, unapoanza kufanya *high breeding* na kuweka mbolea za kemikali katika miti ya viungo tayari unapoteza bei za bidhaa hiyo. Nawanasihi sana ndugu zangu Wawakilishi kwamba mikarafuu ya Zanzibar tukianza kuichakachua tutapoteza *origination* za karafuu, tutapoteza *grade* za karafuu na tutapoteza umaarufu wa karafuu za Zanzibar.

Hatuko *conservative* lakini bado karafuu zina hadhi, *production* yake iko *very high* na kila mkarafuu ukizeeka ukichawanyika ukawa mkubwa zaidi unatoa karafuu zaidi. Mkarafuu mkongwe na mkubwa unaweza kuchuma mpaka pishi 200, mkarafuu uliodhofu na mwembamba, mfupi, kila mkarafuu ukiwa mfupi unakuwa na karafuu pishi tano, sita au kumi. Kwa hivyo naomba hili suala tulizingatie kwa makini. Ukiwa una maarifa mengine Mhe.

Mwakilishi tuletee tutayachukua tutayafanyia kazi, lakini kwa sisi tumeona hakuna njia mbadala isipokuwa ni uchakuaji.

Bima ya wanaoanguka mikarafuu. Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wawakilishi naomba wawe na subira ikija sheria ambayo itakuja mwaka huu huu katika sheria hiyo kuna Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu, katika Mfuko huo kutakuwa na bima ambayo ita-*cover* mtu yeyote ambaye ataanguka mkarafuu au ataathirika kwa njia moja au nyengine kwa ajili ya karafuu. Hiyo ndio njia pekee ambayo itaondosha mzozo huu wa bima ya karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Asha Bakari dada yangu alitaka kujua wafanyakazi wangapi wako *ZSTC*. *ZSTC* mpaka sasa hivi ina wafanyakazi 228, kiwango hiki ni kikubwa sana tunajua, lakini katika mageuzi yetu wafanyakazi hao watapunguzwa kidogo kidogo mpaka watabakia ambao wataweza kuli-*sustain* shirika hili.

ZSTC kununua mwani. Ndio, tungeomba sana *ZSTC* inunue mwani na mazao mengine sio mwani tu, lakini kwa sasa *ZSTC* imo katika mageuzi makubwa hivyo ni vyema tusiiongezee majukumu mengine. Lakini hata hivyo, suala hilo linazingatiwa na limo katika mkakati wa kuliingiza katika mazao muhimu ya Zanzibar ambayo *ZSTC* itanunua hapo baadae.

Sasa tunakwenda katika Shirika la *Motor Trade Corporation* (Shirika la Magari). Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Magari lina wafanyakazi 34 na linafanya kazi ya kuuza *scooter*, baiskeli na vyarahani. Serikali imeamua kwa makusudi kulifunga shirika hili kutokana na kushindwa kujiendesha kibiashara na kutoka katika malengo yake ya kuundwa. Shirika hili liliundwa kwa malengo ya kuuza vipando vya moto pamoja na *spare* zake. Baada ya ushindani mkubwa ulioko kwa *private sector* na shirika hili, kwa hivyo serikali imeamua shirika hili lifungwe. Taratibu za kisheria zinafuatwa za kulifunga shirika hilo pamoja na kuzingatia kwa kina maslahi ya wafanyakazi wake 34. Nataka niwahakikishie wananchi wote na Wawakilishi kwamba, Shirika la Magari litafungwa hivi karibuni na wafanyakazi wote watahakikishiwa kuwa wamepata haki zao zote bila kudhulumiwa, kwani sababu moja iliyofanya tukasubiri hili tusilifunge ilikuwa ongezeko la mishahara.

Wafanyakazi wa *MTC* tungelifunga shirika hili mwezi mmoja tu kabla ya watu kupata nyongeza ya mishahara wangetulaani laana kubwa. Kwa sababu na wao wanastahiki vile vile kupata ongezeko la mshahara ili mapato yao watayopata katika kustaafishwa yawe mazuri zaidi. Sasa hivi mishahara imesharekebishwa na kwa hivyo watastaafishwa kutumia vigezo vya mishahara mipya na sio ile mikongwe. Kwa hivyo, hilo tu ndilo lililotuweka tukilisubiri, hata wale waliotaka kustaafishwa katika Shirika la *ZSTC* vile vile hatukuwastaafisha mpaka marekebisho ya mishahara yao irekebishwe ili wanapostaafishwa wapate fedha za kuwasaidia baada ya kutoka katika kazi. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wawakilishi mtufahamu kuwa tumefanya haya kwa maslahi ya wafanyakazi wa Mashirika haya, na kwa sababu ya kuwahurumia na kuona kwamba wanakokwenda sasa hivi wanakwenda katika maisha mengine.

Waheshimiwa kuna Kiwanda cha Sukari Mahonda. Kwa kweli mtihani mkubwa uko katika kiwanda kile cha Mahonda, kwa sasa hivi kiwanda hiki hakitoi kitu, hakitoi sukari, hakitoi sukari guru wala hakitoi ulevi au spiriti hata umeme umekatwa haumo. Hiki kiwanda serikali imeunda Kamati Tatu; kamati ya wataalamu, kamati ya wanasiasa na kamati ya wanasheria; zote kamati hizo zimeshawasilisha ripoti zake serikalini. Serikali sasa hivi imo katika mchakato wa kuwasiliana na mwekezaji namna gani itamalizana nae. Serikali inafanya kazi hii kwa umakini mkubwa kama walivyoshauri kamati ya biashara kwamba tusije tukageuza suala hili kama vile kule Dar es Salaam. Kwa hivyo, sisi serikali tunafanya kazi kwa umakini mkubwa kuona kwamba hatutoipa hasara serikali, lakini vile vile hatutomuachia mwekezaji akafanya anavyotaka.

Sasa ningewaomba ndugu zangu Wawakilishi tuachie serikali iwasiliane na mwekezaji na mwekezaji atakaposhindwa tu kutekeleza yale ambayo tumemwambia atekeleze basi serikali itawaeleza wananchi wote kwamba kiwanda kile nini mustakabali wake na nini hatma yake.

Mhe. Bi Panya kasema kuwa huyu akinyang'anywa je, hapana wako wawekezaji ambao wameleta maombi yao ikiwa yule atashindwa wao wako tayari kiwanda kile kukiendeleza. Ninachotaka kuwaambia wananchi wafahamu wazi kwamba ardhi iliyotengwa kwa ajili ya kiwanda cha Mahonda ardhi ile ni kwa ajili ya Kiwanda cha Mahonda si vyenginevyo, wavumilie tuangalie mwekezaji huyu kashindwa akija mwekezaji mwengine mpaka pale itakapotoka amri nyengine. Mwananchi kuchukua hatua katika mikono yake kuingia katika shamba lile ni makosa, lile shamba ni mali ya Kiwanda cha Mahonda, kwa hivyo vyengine vyovyote kuchukua hatua nyengine ni makosa

na mtu yeyote akifanya hivyo sheria itachukua mkondo wake. Naomba wananchi wote wawe wastahamilivu, wavumilivu, serikali hairidhishwi na namna ya kiwanda kile kinavyoendeshwa na serikali inafanya kazi kuona kwamba suala hili linamalizika lakini kwa njia ya usalama bila ya kuathiri serikali au mtu yeyote yule.

Kiwanda cha Nungwi. Kiwanda cha Nungwi cha kukausha dagaa na samaki serikali kupitia Wizara ya Biashara kimefanya kazi kubwa kile kiwanda, kimetoa taaluma kubwa ya wale wanajumuia pale wa kikundi kile na tunawapa kila aina ya msaada wanaoutaka na bado msaada wa kisheria, msaada wa mafunzo wizara yetu ipo tayari kuwapa wakati wowote.

Lakini suala la usajili ni suala la kikundi chenyewe. Kisheria kikundi hakisajiliwi na Wizara ya Biashara, kikundi kinasajiliwa na Msajili wa vikundi vya ushirika. Kwa hivyo sisi hatuwezi kumshika mkono mpaka kwa usajili hapana. Wenyewe ndio wakajisajili. mimi binafsi nimewaambia nimewapa changamoto. Mara tu baada ya kujisajili mimi nitakupeni milioni tatu muanzie kazi. Mara wanasema Sheha hataki, Sheha anatukwamisha, wanaume hawataki lakini masuala ya kujisajili ni masuala ya wananchi wa Nungwi wenyewe na sio wizara yangu.

Waheshimiwa Wajumbe viwanda. Wawakilishi wengi wamezungumzia masuala ya viwanda, mimi kama Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ni mmoja kati ya ninayesononeka, nimo katika adhabu kubwa kuwa nina Wizara ya Viwanda lakini viwanda sina. Si peke yangu tu mpaka wafanyakazi wangu wote tumo katika kusononeka kuona kwamba kwa nini viwanda havijengwi Zanzibar.

Lakini suala hili ni suala kubwa, muhimu lakini ni gumu. Serikali imejiondoa katika suala la kufanya biashara na kufanya viwanda. Baada ya viwanda vyake vyote kushindwa kuendelea na kuvifunga na vyengine vimeuzwa, vilivyobakia havifanyi kazi. Kwa hivyo tunachofanya serikali ni kuwashajihisha wawekezaji na wafanyabiashara wawekeze katika viwanda. Serikali haijengi viwanda wala serikali haiendeshi viwanda lakini serikali inashajihisha wafanyabiashara na wawekezaji wengine waje kuwekeza katika viwanda.

Kwa bahati mbaya maeneo ambayo yametengwa kwa sababu ya viwanda kama EPZ hayana miundombinu. Vile vile nchi yenyewe nzima haina miundombinu ya kuweza kustawisha viwanda au ya kuweza kuvutia wawekezaji katika viwanda.

Moja katika suala muhimu sana ni kuwa na Bandari kubwa ambayo itaweza meli itapakia angalau tani laki moja inaegesha pale. Mwenye kiwanda anaingiza malighafi kuji-*process* halafu mwenye kiwanda anaondoa mali safi kuzipeleka nje. Hawezi kukaa pale na mrundikano wa makontena yale pale Malindi akasubiri mwezi mmoja mzigo uje au uondoke, *order* yake yeye anataka mzigo tarehe kadha mpaka tarehe kadha mzigo ule haukwenda o*rder* imefeli. Kwa hivyo hapana mwekezaji atakayekuja hapa kuwekeza kwa Bandari tuliyonayo ya Malindi *no way* tusidanganyane.

Kwa hivyo mimi wizara yangu tunafanya kazi nzito ya kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuona kwamba Bandari ya Zanzibar inajengwa. Kwa hili nasema mimi binafsi ninakwenda mbio kutafuta wawekezaji kwenye mpango wa PPF au BOT kuona kwamba tunashirikiana wizara mbili hizo; Wizara ya Fedha na Wizara ya Miundombinu kuona Bandari inajengwa Zanzibar. Kwa hivyo naomba kwamba tuwe na uvumilivu mkubwa.

Vile vile Uwanja wa ndege unatakiwa uwe unachukua *cargo* na sio vi-*cargo plane* hapa zinasafirishwa na kuhifadhiwa na vyengine vinataka kuingia kwa DHL, hivyo tunataka uwanja wa ndege wa kuleta *cargo* nchini. Vile vile kuwe na barabara na sio barabara *one way*, barabara ambazo zitahimili kuchukua mizigo mizito ya makontena, sio mizigo ya kuchukua kwa vi-*carry* aah! Barabara zinazohimili kuchukua makontena ya mizigo mizito ya bidhaa inayotoka viwandani mpaka bandarini au bandarini mpaka viwandani.

Tena barabara sio za njia moja *may be* njia nne; mbili huku mbili huku au tatu huku tatu huku. Sio mzigo kutoka hapa mpaka Bandarini unachukua siku nne haujafika. Kwa hivyo ndugu zangu ili tuwe na viwanda lazima Wizara ya Miundombinu ifanye kazi kubwa ili viwanda viwepo hapa.

Mutailaumu Wizara ya Viwanda usiku na mchana, wizara yangu haiwezi kufanya kitu kama Wizara ya Miundombinu haikuamka kisawa sawa, ikafanya kazi zake kisawa sawa. Mukitaka viwanda tuibane Wizara ya Miundombinu ifanye hiyo miundombinu kisawa sawa tuweze kufanya viwanda, bila ya hivyo tunadanganyana.

Kiwanda cha Kuku kiliopo Mtoni. Kiwanda hiki ni ubia baina ya serikali na watu binafsi, lakini kwa bahati mbaya serikali ina hisa ndogo na wale *private sector* wana hisa dume. Kwa hivyo serikali kwa hisa ndogo ile madaraka yake ni madogo ya maamuzi katika kampuni ile. Hivi sasa kiwanda kile mimi mwenyewe nimekitembelea mwezi mmoja kabla ya bajeti na kuona kuwa maghala yake yanawekwa saruji, nikahoji wakasema kwamba sisi tuna walinzi hapa, mishahara ya walinzi ndio tunakatia kodi ya kukodisha ghala.

Madhumuni ya jengo hili ni kiwanda, kwa nini munafanya hivi. Ni uamuzi wao wameamua kuuza kile kiwanda na kuuza ile *plant* ya kule Kizimbani ya kuangulia vifaranga. Jambo hili vile vile mimi linanisikitisha sana lakini sina ubavu wa namna ya kugeuza.

Bei waliyouzia ni kubwa sana, serikali si rahisi kwenda kukinunua kile kiwanda. Kwa hivyo hiyo ndio hali halisi ya kile kiwanda. Hiki kiwanda watu binafsi wana hisa kubwa, serikali ina hisa ndogo, kwa hivyo serikali haina meno kwenye kampuni ile.

Usafirishaji wa mchele na sukari kupeleka nje ya Zanzibar. Mawazo ya wachangiaji kuhusu suala hili ni mazuri. Wanasema kwamba kwa nini wafanyabiashara hawaachiwi hii biashara wakaweza kuitoa nje. Sisi hatuna *problem*. *Problem* yetu ni kwamba mchele, sukari na unga tumetoa *exemption*, tumetoa kodi maalum kwa ajili ya Wazanzibari kwa wananchi wetu na sio kwa ajili ya watu wa Kenya, Tanga au Dar Es Salaam, tumetoa kwa ajili ya watu wa Zanzibar.

Kwa hivyo ikiwa wewe unataka kupitisha mzigo wako hapa Zanzibar ukalipa ada zote zinazotakiwa na serikali, tutakuruhusu rasmi utoke na mzigo wako ukauze unapotaka. Na hilo ndilo lengo, tunataka Zanzibar iwe ndio *transit trade* au pawe na biashara za mpito na ndio maana tukaweka pale *free port*. Kwa hivyo wewe ndugu yangu usipate shida, sukari yako iteremshe ipeleke Maruhubi, itie katika ghala uza unapotaka sisi hatukuingilii, kwa sababu hiyo ndio lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba pawepo na transit trade na mimi ninaamini kabisa kama wafanyabiashara wa Zanzibar watachangamka, magari waache waagize bidhaa za chakula. Chakula ni bidhaa muhimu inayotakiwa katika nchi za jirani waende wakauze.

Kenya kilo ya sukari ni shs.1600/=, utoe sukari pelekeni Kenya sio tatizo. Lakini sukari iliyokusudiwa kwa Zanzibar musiitoe nje mukaipeleka nje ya Zanzibar, itakuwa munawadhulumu Wazanzibari ambao wamepewa *privilege* ile.

Hivyo basi wafanyabiashara wote wanaotaka kufanya biashara hii, nawaomba wafike wizarani tutakaa pamoja wizara yangu, Wizara ya Fedha na TRA kuangalia utaratibu gani mzuri utumike ili kuona kwamba wale wenye *interest* hii wanafanya biashara hii bila ya bughudha na bila ya kushukiwa. Tunataka kuimarisha biashara, biashara zije, matumizi ya tani 60,000 za mchele Zanzibar basi, zikija tani laki au laki mbili na zije na zitoke nje, sisi hatuna *problem*. Matumizi ya sukari Zanzibar ni tani arobaini elfu kwa mwezi, hapana matatizo, lete sukari tani elfu tatu peleka nje sisi hatuna matatizo. Matumizi ya unga wa ngano Zanzibar ni tani arobaini elfu, leteni tani ya unga laki tatu pelekeni nje ya nchi hakuna matatizo. Zanzibar ni kisiwa *transit trade* ni muhimu, kwa hivyo karibuni sana. (*Makofi*).

Kupeleka mchele Pemba. Dada yangu Bi. Asha amesikitika sana kwamba kuna mpango mbaya ambao kwamba wameshapeleka bidhaa zao Pemba wanapata usumbufu wa hapa na pale. Ingekuwa wafanyabiashara ni waaminifu, hawatoroshi bidhaa hizi kupeleka nje ya Zanzibar basi pasingehitajika kibali. Pemba na Unguja ni moja wala mtu asingeambiwa achukue kibali upeleke Pemba. Lakini kwa bahati mbaya wale wote waliokamatwa na magendo ya sukari au mchele kupeleka nje ya Zanzibar wana kibali cha kupeleka bidhaa hizo Pemba. Akifika njiani na kibali chake cha Pemba anageuza njia, anageuza tanga upande wa pili anaelekea Tanga.

Kwa hivyo kutokana na hali hiyo ndio maana kila mtu anayetaka kupeleka bidhaa yake Pemba inabidi lazima apate kibali cha Wizara ya Biashara, kwa sababu gani. Kwa sababu kikitoka pale kitakuwa kinakwenda kwa Afisa Mdhamini Pemba, na Afisa Mdhamini anatoa taarifa kwamba leo kunakuja meli ina tani mia tano za mchele. Kwa hivyo pale Bandarini tunaangalia jee, bidhaa inayotoka Unguja imekwenda Pemba au haikwenda Pemba.

Kwa hivyo kuna kitu *monitoring* na tusipofanya hivyo bidhaa yote itaondoka itakwenda zake Tanga na sehemu nyengine ambako si inapokusudiwa na Pemba itakosa mpaka bidhaa ya kula. Kwa hivyo ninataka nimuhakikishie kwamba Wizara yangu muombaji kibali cha kupeleka mchele au sukari Pemba hatozidi masaa matatu atapata kibali

hicho. Anaomba saa tatu, saa sita kibali kile ameshakipata. Hili ni agizo la Waziri wa Biashara kwa wafanyakazi wake wote. (*Makofi*).

Vile vile Jumamosi si siku ya kazi lakini wizara yangu itakuwa ofisi ipo wazi kwa yule ambaye kwamba atakuwa mpaka siku ya Jumamosi hapana kazi, *still* tutakuwepo kutoa vibali kwa bidhaa za Pemba. Hili ni agizo kwa wafanyakazi wa Wizara ya Biashara kuanzia leo. Kibali hakitozidi masaa matatu na mpaka Jumamosi kibali kitatoka.

Hukumu kwa wasafirishaji wa magendo kupeleka Pemba. Ushauri aliotoa ndugu yetu na mpenzi wetu Mwakilishi Salmin tunauchukua. Ni ushauri mzuri kwamba kila atakayepatikana na magendo ya kusafirisha bidhaa kupeleka nje ya Zanzibar, atahukumiwa kwa mujibu wa sheria ziliopo na watu wote watakuwa *treated equally*, hakuna mtu atakayepata *favour*.

Lakini ninasema hivi Wawakilishi musije mukatuomba tena, asije Mwakilishi huyu ni ndugu yangu itakuwa hakuna, tuachieni tufanye kazi. Tusiombane ombane, huyu kakamatwa na bidhaa hukumu yake atalipa shilingi milioni nane basi iwe hivyo hivyo milioni nane, isiwe tena kupiga simu, kuja kuombewa, tusiwaombee.

Kwa sababu hukumu hii hatufanyi kwa kuwakomoa, tunataka wakome kusafirisha bidhaa hizi. Hii ni haki ya watu wa Zanzibar tusiwanyang'anye kwa kutaka kujitajirisha. Lipa ushuru peleka mali yako unapotaka.

Ndugu yangu Mohamedraza kasema msamaha ule ulinung'unikiwa kidogo kwamba watu hawakuja kuwa kutakuwa kutakuwa na msamaha wa kodi kwa ajili ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mimi ninaamini kwamba wafanyabiasahara wote wanajua kwamba kila inapofika Ramadhani kunakuwa na exemption ya bidhaa hizi muhimu, na hii ni kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar wapate bidhaa kwa bei rahisi.

Hilo ni lipo kila pahali duniani. Haikuwa mji wa Makka wakati wa Hijja vitu vyote vinapanda bei. Ukienda wakati wa kawaida vitu rahisi lakini wakati wa Hijja vitu vinapanda bei. Umra Ramadhani vitu vinapanda bei na mji wa Makka ni mji mtakatifu na wote pale ni watu watakatifu wafanyabiashara. Lakini ikifika wakati wa Ramadhani wanapandisha bei, kwa sababu ni wakati wa msimu. Kwa hivyo ili kukata makali ya kupandisha bei wakati wa mwezi wa Ramadhani ndio serikali imeweka *zero tariff*, yaani mchele usilipiwe ushuru wala unga na tende ili wananchi wapate bidhaa kwa bei rahisi na ili kuweka katika *order* mfanyabiashara asipandishe bei katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Kwa hivyo mimi ninasema kwamba ushauri ni mzuri, tutawaarifu wafanyabiashara mapema lakini kila mfanyabiashara kwa mwezi huu wa Ramadhani, kunahitajika tende, unga, sukari na mchele, akilete anapata *exemption*. Unapotangaza mpaka alete nguo ataakhirisha atakwenda kuleta mchele kwa sababu gani, anafuata *facility* sio biashara yake hiyo. Hata hivyo sisi tutangaza mapema ili watu wajue kwamba kutakuwa na *exemption*.

Lakini kwa faida tu ya ukumbi huu, ninataka niwaambie kwamba serikali imefanya maamuzi haya na kwa kweli faida kubwa imepatikana katika nchi yetu. Kwanza wale ambao kwamba maana isionekana kuna wengine wanasema aah! Imefanywa hivi kwa kuwa-*favour* watu maalum, si kweli. Wafanyabiashara ambao wameleta bidhaa ya mchele na unga wa ngano ni wafanyabiashara 16. Nao ni:-

1. Bombay Bazaar
2. Yasir Provision
3. Bopar
4. Mohamed Hemed
5. Omar Ali Hassan
6. Zanzibar Milling
7. Saleh Rashid
8. Muhiddin Suleiman
9. Said Ahmed Abeid
10. Homat
11. Pan East Food
12. Idarous
13. Issa Ramadhan

14. Hilal Khalfan
15. Sub Sahara
16. Zenj el

Hawa 16 wameleta tani elfu 23 za mchele na tani 20 za unga.

Vile vile waagiziaji 41 wameleta tende. Tende tani 801. Ni *list* ndefu siwezi kuisoma kwa sababu ya muda. Lakini bado Mjini Unguja mchele uliokuwa ukiuzwa kilo moja elfu moja mia moja mpaka elfu moja mia mbili. Baada ya msamaha unauzwa shilingi elfu moja.

Unga ulikuwa ukiuzwa shilingi elfu moja mia mbili, sasa hivi unauzwa shilingi elfu moja. Tende iliyokuwa ikiuzwa shilingi elfu tatu mia tano, hivi sasa shilingi elfu mbili mia nne, elfu mbili mia tano, elfu mbili mia tatu *everywhere*. Kwa hivyo ninawashukuru sana wafanyabiashara kwamba wameitikia wito wa kupunguza bei za bidhaa.

Hapa kuna Wawakilishi wamewananga wafanyabiashara. Mimi sikufurahi hata kidogo. Wakifanya vizuri tuwasifu wakifanya vibaya tuwaponde. Tani moja ya mchele ushuru unatozwa shilingi elfu thalathini na mbili. Polo moja la mchele ushuru wake ni shilingi elfu moja na mia sita. Kwa hivyo kilo moja ya mchele ushuru ni shilingi thalathini na mbili.

Kwa hivyo serikali imepunguza nini elfu thalathini na mbili lakini wafanyabiashara wamepunguza shilingi mia mbili bado sisi hatuwashukuru sisi. Tende ushuru wake kilo moja ni shilingi mia tatu, wafanyabiashara wamepunguza shilingi elfu moja na mia tano, bado sisi hatuwashukuru wafanyabiashara.

Kwa hivyo ningeomba kwamba wakifanya vizuri tuwapongeze na tuwashukuru. Mimi kwa niaba ya wizara yangu, ninawashukuru sana wafanyabiashara wamejitahidi kupunguza bei za bidhaa. Waendelee kuwahurumia wananchi wa Zanzibar kwa sababu ndio sisi kwa sisi.

Mimi Mheshimiwa ninapenda kuwa mkweli, kwa hivyo naomba radhi kwa hili pengine wengine litakuwa halikuwafurahisha. Lakini kwa kweli wafanyabiashara mara hii wamejitahidi sana kupunguza bei za bidhaa.

Wengine wanasema kama mchele nyinyi munapunguza bei katika mwezi wa Ramadhani wakati mwezi huu hawali mchele. Si kweli kila nilipoalikwa mimi ninakuta pilau tena basmati nikienda katika futari kwa sababu hivi sasa mchele ni rahisi kuliko muhogo, ndizi na kitu chochote cha matunda. Kwa hivyo kama sisi hatuli mchele lakini wenzetu wanakula mchele sana.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tunakwenda kwenye maghala ya Mtoni. Zimetoka hoja hapa mbona maghala ya Mtoni tumesikia kauziwa mtu. Waheshimiwa Wajumbe mimi nilipokabidhiwa wizara, nilikabidhiwa wizara na *furniture* zake na majengo yake yote ya wizara. Katika waraka wangu niliokabidhiwa wizara sijaona maghala ya Mtoni bahati mbaya. Kwa hivyo ninasikitika sana kwamba sina hadithi yoyote au kumbukumbu yoyote ya maghala ya Mtoni.

Mimi nilipokwenda katika wizara hii sikutaka kuchimba makaburi. Maana ingekuwa mpaka leo nisingefanya kazi yoyote, ingekuwa kazi yangu ni kuchimba makaburi tu ambao watu wamezika maiti zao. Mimi sina nafasi ya kwenda kufanya uchunguzi au kuchimba makaburi ya makosa ambayo kwamba walifanya waliotangulia nyuma yangu. Mimi ninachukua nilichokabidhiwa na ninafanya kazi kwa kile nilichokabidhiwa. Mambo ya kesi za nyuma naomba munisamehe, siwezi kuzishughulikia.

Uwanja maonesho. Waheshimiwa Wajumbe kweli mimi ndugu yangu Mhe. Hamza ninamfahamu sana, mwaka jana alichangia suala hili na mara hii kachangia tena kwamba kweli mpaka hivi sasa kukaa bila ya maonesho, tunataka tuwe kituo cha biashara. Kwa kweli tunaidhulumu Zanzibar. Kwa hivyo mimi binafsi naomba nimuhakikishie Mhe. Hamza kwamba suala hili mimi nimelisimamia nilipokuwa mwenyekiti wa Chamber of Commerce. Mimi ndio niliotoa wazo kwa Dk. Salmin la kutaka tufungue maonesho Tunguu na nikalisimamia, na mimi akanifanya ndio kinara kule Tunguu. Kwa kweli nikasimamia mpaka maonesho yale yakafanyika.

Mimi vile vile ndiye niliyemshauri Dk. Salmin tufanye shopping festival, akaniambia hili jengo la Beit el Jaib palibakia only twenty one days, unaweza wewe ukali-change hili tukaweza kufanya maonesho hapa. Mimi nilikuwa ninalala pale pale kuhakikisha siku ishirini na moja na ikafanyika shopping festival kwa muda wa mwezi mzima pale Beit el Jaib.

Kwa hivyo mimi ni mmoja mkereketwa mkubwa wa maonesho. Hivyo ninakuhakikishia Mhe. Hamza kwamba hili nitafanya kazi mimi na wewe, nitakapokwama nitahitaji msaada wako nitakufuata kwa sababu mengine mimi bosi wangu siwezi kumwambia lakini wewe unaweza kumwambia.

Mhe. Jussa alizungumzia mradi wa BEST na maonesho. Kwa bahati mbaya tumechunguza kwamba ule mradi wa BEST pesa kabisa hazikutoka visiwani wala Bara. Sababu hasa za pesa zile kuzuiwa mpaka hivi sasa hatujazijua. Lakini umetupa changamoto nzuri tutazifuatilia kuona kwa nini fedha zile za BEST ambazo zimeiweka miradi yetu solemba mpaka leo haikufanywa.

Kuhusu *Sunday Market* ni ushauri mzuri tumepata na sisi tutafanya kila liwezekanalo kushirikiana na Wizara ya Uwezeshajai kuhakikisha tunafungua the real Sunday market ambayo itakidhi haja na itasaidia wananchi na wafanyabiashara.

Biashara ya mafuata Waheshimiwa Wawakilishi sijui kwa nini ile wizara inayohusika na mafuta inajifichaficha sijui kwa nini, haijitangazi wazi kwamba sisi ndio wahusika wa biashara ya mafuta. Lakini mim ninasema wizara yangu haihusiki hata kidogo na biashara ya mafuta.

Mimi mafuta yanapochatuliwa hapo ninapigiwa simu kila wakati, Mazurui utatuuwa na kelele moja kwa moja. Mimi ningependa hii biashara ya mafuta ikaja katika wizara yangu lakini haipo katika Wizara ya Biashara ipo katika wizara nyengine. Kwa hivyo sina mamlaka nayo mimi. Kazi yangu kubwa mimi sasa hivi niliyonayo ni kuhakikisha kwamba kila ile pump akenda mteja kutia mafuta anatiliwa mafuta ujazo unaostahiki, sio ananunua lita kumi anatiliwa tisa moja jamaa wanamuibia, aah!

Kwa hivyo kazi ya wizara yangu mimi kupitia kile kitengo cha kumlinda mtumiaji au kitengo kile cha mezani na vipimo ni kuhakikisha kwamba ile *pump* inayo-*pump* mafuta kumtilia yule mteja ni sahihi, kama mbovu tunaiondosha tunampiga *penalt* asidhulumu wananchi. Hiyo ndio kazi kubwa ya Wizara ya Biashara si jengine lolote.

Lakini ZBS ikianza kazi, hicho kifaa ni ghali lakini tunakwenda mbio tukipate ili tuweze ku-*test* mafuta yanayoingia nchini, jee mafuta haya ndio mafuta yenye uhalisia wa kutumia kwenye magari yetu.

Faida gani tunayopata Zanzibar katika ushirikiano wa kikanda. Wengine wamesema kwamba tunatumia pesa nyingi sisi kwenda huko kuweka mikutano hiyo hapana faida yoyote, wengine wanasema hamushirikishwi sijui hivi na vile. Mimi ninasema kwamba Serikali ya Zanzibar tupo *very aggressive*, hatukubali wenzetu wasitushirikishe katika masuala ya sera.

Kwa hili tumewabana kisawasawa. Katika mikutano ya kisera mikutano yote tumehudhuria na tunakwenda nao sambamba. Ijapokuwa hivi sasa hatufaidiki sana na masuala haya kwa sababu hatuna viwanda, madhali huna viwanda huwezi kufaidika. Kwa sababu kama una kiwanda mali yako unapeleka Rwanda hailipwi ushuru, unapeleka Kenya hailipwi ushuru, Uganda hivyo hivyo lakini sisi hatuna viwanda. Hatuna cha kuuza isipokuwa mwani na karafuu. Bahati mbaya mwani hawatumii hawa jamaa na karafuu pia hawatumii.

Sasa basi lakini hatuwezi kuwaachia tu hawa, kwa sababu gani ipo siku masoko haya tunayataka sisi. Kama si miaka mitano ijayo miaka kumi lakini masoko haya tunayahitajia. Tukiacha sisi hatuhudhurii katika mikutano ya sera au ya kikanda, ikifika baada ya miaka kumi itakuwa tumeshasahauliwa. Kwa hivyo ninataka niwaambie wazi kwamba tunashirikiana bega kwa bega na Tanzania Bara katika masuala ya kikanda.

Mkutano ya mwisho wa *summit* tulifuatana mimi na Mhe. Dr. Mwinyihaji huyu hapa, tukaenda zetu Jordan. Kule kile kikao Tanzania ilikuwa inaongozwa na Mhe. Dr. Mrisho Kikwete. Mhe. Kikwete alipoondoka pale akaniambia Mazrui ninakupa kiti ukae wewe hapa na mimi ndiye niliyekuwa ninaongoza kile kikao kwa niaba ya Dr. Kikwete. Hata Museveni akanichokoza "*who are you*?". Nikamwambia mimi ni fulani tena tukaanza *communication* mpaka

leo tunawasiliana. Lakini kwa kweli tukifika kule wanatupa nafasi zetu tunazichukua kwa sababu hatukuzubaa sisi. Tunakwenda kule mimi ni Waziri, aliyekuja Naibu Waziri wa Bara ninamuweka nyuma, ninakaa mimi Waziri mbele. (*Makofi*).

Masuala haya ni masuala ya *personality*, ukienda pale ukajiweka nyuma ni mwenyewe umejiweka nyuma. Mimi sitokwenda katika kikao cha Tanzania, Naibu waziri akajiweka mbele atakaa nyuma yangu. Akija Waziri atakaa hapa na mimi nitakaa hapa, hakuna yeye akae mbele mimi nikae nyuma. Kwa hivyo masuala haya ni masuala ya kwamba wewe unayekwenda kule ujue unafanya nini.

Malalamiko ya wafanyabiashara katika bandari ya Dar es Salaam. Kweli Dar es Salaam kuna usumbufu mkubwa sana wa TRA unawasumbua wafanyabiashara wa Zanzibar. Hili suala ni kweli na hili ni donda sugu halipoi. Dawa yake Zanzibar ifungue milango ya kuwa na masoko huria na mambo haya yote yatamalizika.

Kwa hivyo ni kweli na serikali inafanya mazungumzo kama kawaida lakini bado wenzetu hawajataka kutupa nafasi. Hivyo ninaamini kwamba suala hili katika mchakato wa Katiba wananchi wasilisahau kwamba biashara baina ya Bara na Zanzibar haiendi ipasavyo na kwa hivyo basi ni lazima Katiba irekebishwe, ili biashara baina ya Bara na Zanzibar iende kisawa sawa. Lakini mimi sioni kuwa kuna nia ya dhati ya kuweza kuondoa suala hili. Huo ndio ukweli ulivyo na ninasema bila ya kificho wala kigugumizi.

Chengine kuhusu chakula la msaada na maghala ya akiba. Waheshimiwa Wawakilishi tunasahau mara moja sisi. Mwaka jana hapa tulipitisha sheria maghala yote ya akiba tumeyapeleka Kilimo. Kwa hivyo Wizara ya Biashara imeosha mikono katika masuala ya maghala ya akiba haihusiki.

Sasa basi, chakula kinachotoka cha msaada kutoka Tanzania Bara, chakula kile kinakuwa katika Wizara ya Kilimo Bara. Bara vile vile masuala haya ya maghala ya akiba yapo katika Wizara ya Kilimo. Kwa hivyo sasa Wizara ya Kilimo Bara ikishirikiana na Wizara ya Kilimo Zanzibar wanawauzia mchele au bidhaa ile Wazanzibari, haimuuzii mtu wa Bara. Lakini mtendaji yule sasa alikuwa na roho mbaya, mchele ule anamuuzia mfanyabiashara pale pale Dar es Salaam, akachukua chake akaondoka.

Sasa basi mchele ule ule unatoka Dar es Salaam ukaja Zanzibar ukaja ukauzwa kwa bei ya juu. Hili ni jambo baya sana. Lakini mimi kama wizara yangu sina meno. Kwa hivyo ninawaomba Wizara ya Kilimo suala hili wasilifanyie mchezo, Wizara ya Kilimo ifanye njia ya wazi kabisa mtu yeyote atakayenunua biashara hii kutoka Tanzania Bara aje nayo moja kwa moja Zanzibar asimuuzie mtu Bara na akimuuzia mtu Bara awajibike. Lakini sasa hili kila siku inalaumiwa Wizara ya Biashara. Wizara ya Biashara haihusiki na masuala haya.

Hapa kuna jengine habari ya *agencies*. *Agencies* ni kweli kama ukenda katika ulimwengu huko ukisema unatoka Zanzibar mtu hakuelewi, huo ndio ukweli ulivyo. Ukitoa *passport* yako Tanzania, kwa hivyo anajua kwamba wewe ni Mtanzania. Sasa katika sheria za biashara Mhe. Jussa kama yeye ndio *agent* wa matairi Tanzania, kiwanda kile hakiruhusiwi kumpa u-*agent* mtu mwengine Mtanzania isipokuwa Mhe. Jussa. Kama *agent* anatoka Isuzu Tanzania ni Mhe. Jaku. Basi Mhe. Jaku ndiye atakayekuwa *agent* wa biashara ile.

Kwa bahati mbaya Zanzibar tulikaa nyuma sana hatuchukui u-*agent*. Kwa hivyo *agents* nyingi zinatoka Bara. Kwa hivyo mimi nikitaka *agent* tayari yupo Dar es Salaam au Tanga. Sasa na sisi vile vile tuwe *aggressive* kwenda kuchukua *agents* za bidhaa kule nchi za nje ili asipewe *agent* mtu aliyepo Bara.

Lakini hili kimataifa si jambo rahisi. Ukienda kule ukimwambia Zanzibar ni nchi hakuelewi yeye, anajua Tanzania ni nchi moja na Zanzibar ni sehemu ya Tanzania, hajui vyengine. Kwa hivyo tusijidanganye kule biashara ni vitu vya wazi si vitu vya siasa. Katika biashara hakuna siasa. Anaanglia Tanzania, akiangalia mimi ni Mtanzania, akiangalia *list* ni Tanzania, kompyuta zile akitoa nchi ni Tanzania hakuti nchi Zanzibar. Kwa hivyo tumeungana tumepoteza masuala hayo ya biashara hayawezekani. *I am very sorry*. Tuwe *aggressive* kuchukua *agents* kabla ya wenzetu Bara kuchukua, lakini mtu mmoja akipewa Zanzibar basi Bara hapewi, na mtu mmoja akipewa Dar es Salaam, Zanzibar hapewi.

Jengine hapa kuna mfuko ambao ndugu yangu Mhe. Mohamedraza ameutoa wa milioni mia mbili. Mhe. Mohamedraza tunamshukuru sana na tunampongeza sana. Mhe. Mohamedraza kwa kweli ni mkereketwa wa maendeleo ya Zanzibar. Mhe. Mohamedraza ninamuelewa sana, anapenda maendeleo ya Wazanzibari. Mhe.

Mohamedraza na mimi binafsi tumeanza biashara ndogo ndogo hizi za kudondoadondoa hizi, hakuja tu juu akazuka, mimi ninamkumbuka alikuwa akichuuza chuuza humu, ananunua hapa anauza hapa mpaka kafika hapa.

Kwa hivyo akiona ile hali aliyotokea nyuma anahisi ipo haja ya kuwasaidia wafanyabiashara ndogo ndogo. Mimi ninampongeza sana na ninamuunga mkono sana. Sasa basi wizara yetu itafungua mfuko ambao utakuwa ni *resolving fund*, utaitwa Mohamedraza Fund.

Kwa hivyo Mhe. Mohamedraza namuomba asichelewechelewe, katika kipindi cha wiki mbili tatu aje pale tuzungumze tufungue akaunti benki hizi fedha aziingize, tuanze kuwapa wananchi mkopo watakaostahiki wafanye kazi. (*Makofi*).

Taratibu za kupata namba kwa wizara Zanzibar *bar code*, anasema Mwakilishi hapa kwani sisi Zanzibar *bar code* hizi lazima zitoke kule Bara, kwani sisi hatuwezi kuwa na zetu. Ninasema inawezekana na hiyo kazi tunaifanya Zanzibar inaweza ikawa na *bar code* yake. Yupo mmoja kasema kwamba jee Zanzibar haiwezi kwenda bila ya TRA. Hili ninamuachia Mhe. Waziri wa Fedha akija hapa katika wizara yake mumuulize, mimi jawabu sina kuhusu TRA. Waziri wa Fedha atajibu suala hilo atakapokuja katika bajeti yake.

Bidhaa zilizopita wakati tunaangamizwa. Waheshimiwa Wajumbe mimi ninasema tena tangu nilipoingia katika wizara hii sipo tayari kuona kwamba bidhaa mbovu zinaingizwa nchini. Ingawaje suala hili lipo katika sehemu mbili; Wizara ya Afya na Wizara ya Biashara. Wizara ya Afya hii ndio inayohusika kuona mzigo pale bandarini hauingii ambao umeshapitwa na muda. Wizara yangu mimi inakwenda kuangalia katika *shelves like*, inawezekana bidhaa imekuja kufika pale baada ya mwaka mmoja ika-*expire* ndio kazi yangu mimi.

Inawezekana mtu kaagiza mchele kautia katika ghala, ukenyeshewa na mvua mchele ule ukabadilika rangi yake na ladha yake na ukawa haufai kuliwa na binadamu. Inawezekana ghala yake huyu bwana aliyeitia hii bidhaa ina unyevunyevu ikaharibika bidhaa ile ingawaje ina-*expire* mwakani lakini inaweza ika-*expire* leo kutokana na uchafu ule wa mazingira.

Kwa hivyo wizara yangu mimi inahusika ikitokeze bidhaa ile imeharibika kwa mazingira au imepita muda wake, huchukua hatua lakini bandarini pale ni Bodi ya Vyakula, Madawa na Vipodozi ndio inayohusika.

Kwa hivyo mimi ninasema kwamba hatukubali kuona kwamba kuna mtu anauza bidhaa iliyokwishaharibika. Ninasema tena kwamba naomba kwa wananchi wote waunde NGO moja ya *consumer*, yaani ya NGO ya watumiaji, mukiunda NGO hiyo ndio mutakapoweza kwenda kuwashtaki wale wanaowauzia vitu vilivyokuwa vimesha-*expire* au vitu feki.

Sasa hivi ukimwambia mtu anakwambia mimi nimenunua *juice* hii ime-*expire*. Ukimwambia twende tukamshtaki huyo aliyekuuzia hataki kwenda kumshtaki. Kwa hivyo dawa ni kuundwa hizi NGOs za watumiaji ili ziweze kulinda maslahi ya watumiaji.

Waheshimiwa Wawakilishi tumeambiwa kwamba jee bidhaa gani tumeziangamiza. Tumeangamiza maharagwe tani tano *points* tano, thamani ni milioni tatu laki nane hamsini elfu, tumeangamiza mchele tani moja na nusu, milioni mbili na ishirini na tano elfu, unga wa sembe tani mbili, tende tani moja, milioni mbili na laki sita.

Bidhaa za makopo zenye thamani ya milioni nne mia nne na ishirini na tano. Kwa hivyo kwa mwaka uliopita tumeangamiza bidhaa za milioni kumi na tano kutokana na uchunguzi tuliofanya.

Waheshimiwa tunaambiwa vipi habari za mezani zilizokutikana hazifai na hatua gani tumechukua. Mezani zote zilizokaguliwa ni mezani elfu mbili mia moja na thamanini na moja na mezani zilizokuwa hazifanyi kazi ni mia moja na ishirini na tatu. Kwa hivyo mezani mia moja na ishirini na tatu zimekuwa-condemned na mezani elfu mbili zimeonekana kuwa zinafanya kazi na zimeruhusiwa kufanya kazi.

Hili ni zoezi la kila siku. Kila mwaka tunapitia mezani kuziangalia na mezani inayodhulumu tunaiweka upande isitumike na mezani yenye matatizo tunamtengenezea ili itumike.

Vituo vilivyokutikana havifai navyo vimechukuliwa. Mimi ninasema kwamba sisi tunafanya kazi ya kuangalia zile sehemu za maghala na vile vituo wanavyofanyia kazi watu, na ikiwa havikukidhi haja tunavichukulia hatua na kila mmoja anayepigwa faini na wakupigwa warning anapewa warning lakini hatua zinachukuliwa, hapana mmoja anayeachiwa bila ya kuchukuliwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwahakikishie ndugu zangu Wawakilishi kwamba nimejaribu sana kujibu masuali yao, lakini kama nilivyoeleza katika kitabu changu kwamba zile fedha ambazo Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete ametuahidi bado hazijafika lakini jitihada inafanywa kubwa na kiasi miezi miwili nyuma Naibu Waziri wangu Mhe. Thuwaybah ameonana na Mhe. Kikwete uso kwa macho na kumkumbusha suala hili, na pale pale Mhe. Kikwete akamuita msaidizi wake akampa maagizo ya kutekeleza.

Kwa hivyo nina imani kwamba fedha hizi zitapatikana hivi karibuni. Masuala mengi tumeambiwa ya SZ, naomba tusubiri baada ya muda mfupi SZ tutapata mambo yote yanayohusu SZ.

Suala la Zanzibar Bureau Standard, mamlaka haya ilikuwa hatuna ofisi yake, hatuna pa kufanyia kazi. Ninashukuru serikali imetupatia maeneo ya kufanya kazi kwenye maeneo ya Kiwanda cha Sigara Maruhubi. Tumepewa pale majengo mawili. Mwaka huu katika bajeti hii tutafanya ukarabati na kitengo hiki kitaanza rasmi.

Tunashirikiana na TBS Dar Es Salaam na tunashirikiana na watu mbali mbali katika kuona namna tunaweza kupata kitengo kizuri kinachoweza kusaidia kukidhi haja.

Habari ya Jua Kali, Saateni na Darajani, kama alivyoeleza Mhe. Mwinyihaji tumo katika mazungumzo, tunakaa kitako kuona namna gani kuweza kuwasaidia. Kwa kweli wanafanya biashara katika mazingira magumu, mabaya, hayaridhishi lakini si muda mrefu suala hili litatatuka na matatizo haya yote yataondoka.

Ninataka nimuhakikishie Mhe. Hamza kwamba sisi hatukukaa kitako, hao wamekuja ofisini kwetu na wanakuja kila siku wanatukera na wanavyokukera wewe. Sisi vile vile tunakereka kwamba hawa jamaa hawajapata bado mustakbali wao, na hatupendi wateseke, hao ni wananchi wa nchi hii, wana haki ya nchi hii na wanafanya kazi kwa mikono yao na jasho lao, hawaendi katika kuvunja nyumba za watu wakaiba, hawafanyi utapeli. Kwa hivyo ni lazima wasaidiwe ili wapate *income* zao kwa njia za halali na waweze kuendesha maisha yao.

Kuhusu makontena ya Darajani, namuomba Mkurugenzi wa Manispaa awape leseni, asiwatese wala asiwaadhibu. Hawa ni wananchi wetu wanafanyabiashara leseni awape. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie hapo na nitowe hoja.

Samahani Mhe. Mwenyekiti, nimesahau kumtaja Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, alichangia na katika orodha yangu nimekosa kumtaja, namuomba radhi sana. Vile vile alichangia kwa maandishi Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kojani na yeye alichangia. Kwa hivyo, wachangiaji wa maandishi watakuwa sita na wachangiaji wa mdomo watakuwa ni 18. Naomba radhi kwa haya, nawaomba mnisamehe. Ahsanteni sana, Wabillah Tawfiq.

Waheshimiwa Wajumbe: Bado hajatoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Alikwishatoa.

Wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako tukufu limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa naliomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu, ahsante.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU – 21 WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Kifungu 0601 Idara ya Biashara Sh. 60,000,000

Jumla ya Fungu Sh. 60,000,000

FUNGU – 21 WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba Sh.339,829,000

Kifungu 0401

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili nikapata ufafanuzi kwa jambo dogo kabisa. Lakini namuomba Mhe. Waziri asiwe na wasi wasi kwa sababu buti hii ni sawa sawa na chura kumpiga teke unakuwa unamzidishia mwendo. Hivyo, asiwe na wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilizungumzia kadhia iliyomkumba ndugu yetu Ali Haji mkaazi wa Kijiji cha Chaani, ambaye alipata athari katika uvunaji wa zao la karafuu, alianguka katika mkarafuu mwaka 2002 ni muda mrefu sana. Alijitahidi kufuatilia haki zake za kimsingi ili kupata angalau kufidiwa kwa ule ulemavu ambao ameupata. Hivi sasa ndugu huyu amepoteza mawasiliano baina ya sehemu ya juu na ya chini ya mwili wake. Kwa hivyo, yupo kitandani karibu huu mwaka wa nane au zaidi ya miaka minane, kwa sababu ni tokea mwaka 2002.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema jana Mhe. Waziri tunashukuru sana Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia kitengo cha habari, wao walikwenda kumuona kama mwaka mmoja uliopita, wakamsikiliza na wakarusha mpaka katika vyombo vya habari vya televisheni ya Zanzibar. Hivi sasa kwa kweli hali yake ni mbaya sana, kutokana na jitihada za wenzetu hawa wamejitahidi wamepata fedha wamemfungulia *account*. Tunashukuru *Zanzibar Park* wametusaidia karibu shilingi laki 300,000 ameingiziwa kwenye *account* yake. Kuna benki ya DTB wao wamejitolea wamemfungulia *account* bure.

Sasa nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini sikupata ufafanuzi ni namna gani Wizara yake kwa kupitia Shirika la ZSTC wataweza kumsaidia ndugu huyu ili angalau na yeye aweze kufaidi matunda ya dunia. Yeye wakati wake karafuu ilikuwa bei ya chini, lakini sasa hivi wenzake wanafaidika. Lakini bado alikuwa katika jitihada ya kujenga nchi hii.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa haya maelezo nayatoa kwa urefu, ili Mhe. Waziri azione zile jitihada za wenzetu walioanza kufuatilia kwa kupitia idara za watu wenye ulemavu. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri angetutolea kauli angalau tukasikia na yeye wizara yake itajitahidi vipi katika kumsaidia ndugu huyu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma ameliuliza swali hili kweli, katika michago yake na mimi naelewa *concern* yake, kwamba huyu mwenzetu ni muhanga mmoja wa zao la karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mazungumzo jana usiku mimi na wafanyakazi wangu, tulisema kwamba kwanza huyu mtu tumtembelee ili na sisi tujuwe ni namna gani tunaweza kumsaidia. Hili la kwanza.

Lakini katika ile sheria tutakayotunga ya mfuko tuone ni namna gani itaweza kuwasaidia wahanga ambao wamepata ulemavu kutokana na zao hili la karafuu. Kwa hivyo, kazi hiyo ni ngumu haiwezi kufanywa. Lakini mimi namuahidi kwamba wafanyakazi wangu watakwenda kumuona huyu bwana kabla ya sikukuu na bila shaka watakwenda na sikukuu nzuri kumpa huyu bwana na tutamtia katika orodha tutakayoorodhesha na yeye atakuwemo na kwa kweli sisi tuko *very sorry* na suala hili.

Hata miezi mitatu nyuma alikuja mtu vile vile aliumia mkarafuu, tukamchukua wizara tukampeleka Dar es Salaam Muhimbili akafanyiwa dawa, ilikuwa mguu ukatwe, lakini tukamsaidia na mguu *Alhamdulillah* umehifadhika. Kwa hivyo, hili ni jukumu letu namuahidi kwamba tutalifanyia kazi wala asiwe na wasi wasi wowote. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama kawaida yangu namshukuru sana Mhe. Waziri na nimefarijika zaidi kwamba mimi nilitegemea pengine baada ya skukuu, kumbe yeye atamuona kabla ya skukuu, basi naamini ndugu yetu huyu ataweza kufarijika. Nakushukuru sana Mhe. Waziri, lakini naomba sana vijana wako wawasiliane na idara ile ya yule Afisa Habari wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa sababu yeye ndiye anayeshughulika sana na mtu huyu, nafikiri ataweza kupata taarifa na atawapeleka mpaka hapo alipo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwa majibu yake mazuri ya wazi na ya kina kabisa. Lakini naomba anisaidie kidogo. Nilipohoji maeneo ya Mtoni kwenye maghala na maeneo ya viwanja. Mhe. Waziri nilimfahamu kwamba yeye hapendi kufukua makaburi, lakini wataalamu wakihitaji mafupa ya mtu wa kale basi hufukua kaburi wakaangalia mtu huyu ana umuhimu gani. Kwa hivyo, ninachotaka kujua mimi sio kufufua kaburi, bali aniambie kwamba lile eneo kweli lilikuwa ni mali yao, ili kumbukumbu zangu mimi Mwakilishi pengine na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo zinaoana na wizara. Je, ile mali ilikuwa ni yao na kama ni yao basi imekwenda wapi, kwa sababu kumbukumbu zetu sisi kama Wawakilishi kwamba ile mali ilikuwa ni ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo lakini wamekabidhiwa wao. Sasa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ilichukua mali yake pengine ikahaulisha, ikauza au vipi. Angalau tupate kumbukumbu. Je, kumbukumbu anayo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, mpaka jana yeye alivyouliza swali pale mahala mimi nilikuwa sijapashughulikia. Kwa sababu mimi nilipokabidhiwa haikuwemo katika orodha ya vitu nilivyokabidhiwa, lakini baada ya jana yeye kuuliza swali lile basi nikawauliza watendaji wangu pale kwamba hii mali ilikuwa ni ya wizara au ilikuwa ni ya mtu gani. Wakasema kweli ilikuwa ni ya wizara lakini imeuzwa. Kwa hivyo, hivyo ndivyo ninavyojua mimi kauli kuwa imeuzwa, lakini kwa mimi nilipoingia pale wizarani ile mali haimo tena imeshauzwa zamani haipo tena sio mali ya wizara. Lakini inaonesha kwamba kweli ilikuwa ni ya wizara kutokana na maneno ya wawekezaji.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kidogo leo mitambo yako ina matatizo, mimi Mhe. Waziri hanisikii wala mimi simsikii vyema, lakini

Mhe. Mwenyekiti: Alichosema Mhe. Waziri ni kwamba yeye ile mali alipofika pale hakuikuta, amesikia tu kwamba imeuzwa kwa mtu binafsi, lakini hana yakini na hilo. Katika vitu alivyokabidhiwa suala hili halimo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kukabidhiwa ni jambo moja, lakini mali kuwa ni yao ni jambo jengine vile vile. Sasa kwa kuwa hakukabidhiwa, mimi nashukuru kuwa hakukabidhiwa, lakini kumbukumbu za Wazanzibari wakiwemo Wawakilishi, ile mali ilikuwa chini ya wizara yao.

Kwa hivyo, naomba anisaidie atafanya vipi angalau ajue kwamba kweli ilikuwa ni mali yao na je, ikiwa ilikuwa ni mali yao, ilikuwaje ikawatoka ghafla. Maana yake ile mali ninavyojua mimi iliwatoka mwaka 2010, wakati huo watu wanakwenda kwenye uchaguzi basi ile mali ikawatoka. Sasa angalau atuambie iliwatoka vipi.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiria Mhe. Waziri alikuwa muwazi sana, alizungumza katika majumuisho. Hili ndio tatizo ambapo anazungumza inakuwa wengine hatusikilizi. Mhe. Waziri alisema mwanzo kwamba yeye mambo ambayo ameyakuta wakati yametokezea kabla ya yeye kukaa pale hayajui na hataki kuyatolea ufafanuzi, anachoweza kuzungumza ni kile ambacho amekikuta kwa wakati ule ambapo alikuwa yuko katika madaraka.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, samahani. Mhe. Mwenyekiti, nchi hii mtu wa mwanzo aliyeongoza ni Rais Karume Marehemu. Lakini mambo yake hadi leo sisi tunatumia hatuwezi kusema kwamba mambo ya Karume tuyaache. Kwa hivyo, kama yeye hakuyakuta sio hoja kwamba tusimuhoji, yeye ni Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko mwenye kumiliki wizara nzima na kama hivyo ndivyo, basi yale ya Karume tuyaache jambo ambalo sio sahihi.

Kwa hivyo, ninachosema mimi ni kuwa angalau kama Waziri alihadithiwa na anasema hakuambiwa, basi anisaidie kama Waziri. Kwa sababu ile mali ni yake angalau aniambie atafanya vipi ili awaulize watendaji wake. Yeye amekuja juzi mwezi wa Novemba, lakini kuna watendaji pale wakongwe, angalau wamuambie kuwa ile mali ni yetu na imekwenda wapi, hilo tu anisaidie.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, namfahamu sana Mhe. Hija Hassan. Mhe. Hija Hassan anataka kunitia mimi katika matatizo. Kwa sababu mimi nimeingia pale ile mali sio ya wizara, unasikia na sio hiyo tu. Hapa Unguja kulikuwa na magodauni kibao ya wizara hayapo tena, viwanda tele vya wizara havipo tena. Sasa mimi nilipokuwa Waziri nikaambiwa kazi yako ya kwanza, maana yake kila Waziri anapewa kazi zake. Mimi nimepewa hadidu rejea za kazi zangu. Sikuambiwa niende nikafuatilie maghala au mali zile zilizokuwa zimechukuliwa. Katika hadidu rejea za kazi zangu kama Waziri ufuatilie maghala yote ya biashara.

Mhe. Mwenyekiti, kazi hiyo ningeifanya, maana ningetaka bajeti hapa nikataka fungu la kuajiri polisi na wapelelezi wakenda kuifanya hiyo kazi. Lakini sasa akinihoji maghala ambayo siku niliyoingia katika hiyo wizara nikakabidhiwa ni haya hapa. Kama katika maghala hayo liko lililovunjika au liko lililouzwa basi mimi anihoji. Ghala la nyuma sina ushahidi wala sioni ushahidi.

Kwa maana hiyo, naomba radhi sana na pia naomba anielewe kwamba mimi kwa bahati mbaya hayo mambo ya nyuma siyajui na wala sitaki kuyajua, kwa sababu hayamo katika hududi rejea ya kazi zangu za uwaziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan Hija, nadhani utusaidie katika hili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi namuelewa Mhe. Waziri. Lakini pale kwa utafiti wangu nilioufanya kuna maghala na nyumba mbili za serikali. Nyumba ambazo serikali ingezipata, basi zingewasaidia wafanyakazi wengine wa serikali badala ya kuwapangisha.

Kwa kweli mimi nilikwenda mwenyewe kwa ajili ya kufanya utafiti na nilimchukua Dkt. Mhe. Hamza Hassan Juma kwa lengo la kwenda kunisaidia. Mwenyekiti, zipo nyumba mbili za serikali ambazo ni nzuri na nyumba yenyewe pengine badala ya Mhe. Naibu Waziri kupangishwa basi angepewa ile kwa ajili ya kutumia. Kwa hivyo, angalau nataka kujua kwamba maghala pengine yamekodishwa au yameuzwa, lakini Mhe. Waziri anasema hadi anakabidhiwa yeye hajaambiwa.

Sasa mimi nilitegemea tokea jana watendaji wake wamemuambia kwamba yalikuwa yetu, lakini hilo hawajamwambia au tuliyauza, kwa sababu Mhe. Waziri wa Fedha ile ni mali ya serikali, pengine pia angefanya mawasiliano na Mhe. Waziri wa Fedha pengine akamwambia je, mwenyewe niliyachukua.

Mhe. Mwenyekiti, naomba labda Mhe. Waziri wa Fedha anisaidie, kwa sababu ile mali ni ya Mhe. Waziri wa Fedha ndio mali yake, lakini alimpa Wizara ya Biashara, kwamba ayatumie siku hizo na mwaka 2010 yakaondoshwa Wizara ya Biashara, sasa je alichukua mwenyewe au kuna mjanja ambaye alifanya ujanja wake, mimi nataka nisaidiwe hicho tu, tena ni Jimboni kwake Mtoni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, mimi nafikiria meza kubwa mtusaidie. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi naiona *concern* ya Mhe. Hija Hassan Hija, pia naiona *concern* ya Mhe. Waziri. Kwa hivyo, kama Mhe. Waziri alipokabidhiwa afisi yale maghala hayamo, kwa hiyo si rahisi Mhe. Waziri kuweza kuyashughulikia.

Lakini *concern* ya Mhe. Hija Hassan Hija nayo ninaiona kwamba kama zile ghala ni mali za serikali, basi ni vyema serikali ikawa inaelewa haya maghala yanafanya shughuli gani, anayo nani na kwa utaratibu gani? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimwambie Mhe. Hija Hassan Hija, kwa sababu amelileta na tumemsikia, basi atupe nafasi mimi nikimaliza kikao hichi cha leo nitatafuta taarifa za maghala haya na nitaweza kumpatia Mhe. Hija Hassan Hija ni *writing*, kwamba yale maghala shughuli zilizokuwa zinafanya chini ya nani na kama yamerudishwa serikali basi tuweze kujua kuwa hivi sasa yako serikalini.

Vile vile nataka nimthibitishie Mhe. Hija Hassan Hija pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wote, kwamba hivi sasa serikali tuko katika zoezi kubwa sana la kuhakiki mali za serikali.

Kwa hivyo, haya maghala kama bado yako ndani ya serikali yatakuwemo katika orodha za mali za serikali na kama hayapo pia hayatakuwemo na tutaweza kupata taarifa kamili. *Concern* ya Mhe. Hija Hassan Hija tumeifahamu, hivyo nataka atukubalie kwamba tutampa taarifa hata kabla ya Baraza hili halijamalizika nitampatia taarifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kwa kweli Mhe. Hija Hassan Hija hoja yake haikwenda kwenye ghala peke yake alisema na nyumba mbili pia.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, ndio kwa zote.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri wa Fedha na nimsaidie tu kwamba, hadi mwezi wa Machi, 2012 maghala yale yalikuwa na mpangaji ambaye alikuwa amepangishwa na serikali, sasa sijui nani aliyempangisha, kwa sababu kuna mpangaji ambaye amepangishwa kwa mikataba, lakini baadaye akaambiwa maghala yake yalikuwa tayari yameshauzwa tangu mwaka 2010.

Kwa hivyo, namsaidia *point* hiyo, pia kuna mpangaji akitaka mimi nitamwambia kwamba mpangaji huyu amepewa na kwa bahati nzuri huyu mpangaji amepewa na Wizara yenyewe ya Biashara.

Kwa maana hiyo, ningetegemea watendaji wangemuambia Mhe. Waziri kwamba jengo hili alikodishwa mtu, lakini Mhe. Waziri kwa ufupi kuna mpangaji ambaye amepangishwa lakini hatimaye ameambiwa aondoke, kwa sababu mali imeuzwa. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tuendelee. Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake ambao ameutoka katika hoja mbali mbali, yaani ni ufafanuzi wa wazi na umeeleweka. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anisaidie mambo mawili. Wakati nilipokuwa nikichangia bajeti yake Mhe. Waziri nilitaka ufafanuzi juu ya maofisa wale waliokwenda nje kwa kutumwa na serikali kama alivyotueleza. Sasa alipokuwa akitoa ufafanuzi juu ya jambo lile, alieleza kwamba maofisa hawa walitumwa na serikali kwenda kutafuta Soko la Karafuu na wala sio kuuza karafuu kama walivyofanya na ndio maana yeye kama ni Waziri akazuia mauzo yale.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuuliza Mhe. Waziri je, Mhe. Waziri mbali ya sababu hiyo ambayo ametueleza ya kwenda kule kwa ajili kutafuta soko, hivi kuna sababu nyengine ambayo imesababisha ayakatae mauzo hayo ambayo yamefanywa na hilo moja.

Pili taarifa tulizonazo mauzo kule tayari yameshafanyika na mauzo maana yake ni kupokea fedha, yaani tayari fedha zimeshaingizwa katika *Account* ya *ZSTC*. Je, fedha zile zitarejeshwa kwa aliyeuziwa au utaratibu gani ambao utatumika. Namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi juu ya mambo hayo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa maelezo yake kuhusiana na suala hili. Kwa kweli serikali haikuwaagiza waende wakatafute Soko la Karafuu, ipokuwa limewaagiza waende wakatafute bei za karafuu za mwaka 2012/2013.

Kwa hivyo, si soko wala si kuuza, kwa bahati mbaya watendaji hawa wameteleza na kuuza karafuu bila ya idhini ya serikali. Sisi serikali tuna mtindo wa kwamba hata mtu binafsi au hata kama mimi ninayo kampuni yangu pamoja na bodi yangu ninapotuma watu waende wakatafute uchunguzi wa masoko na wakirudi pale basi bodi inakaa na kuamua ndipo tunapouza.

Kwa maana hiyo, ni bahati mbaya binadamu wameteleza. Sasa wao ni kama watendaji lakini mimi ni msimamizi wa wale watendaji. Mhe. Mwenyekiti, wameteleza na kuuza fedha zimeingia kweli na hapa kuna taratibu za kinidhamu na za kiofisi zitakazotumika. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Salmin Awadh Salmin anataka tuzitoe hapa.

Mimi ningeomba atuachie kama wizara na serikali tuangalie hatua gani za kuchukua, ili kuona kwamba tunarekebisha kasoro hizi, kwa sababu hizi karafuu zimenunuliwa kwa fedha za umma na ukiuza lazima kile kitu kiwe cha uwazi kabisa na wala hakuna kuficha ficha.

Kwa kweli hakuna sababu nyengine yoyote iliyonifanya mimi nizuie mauzo yale, isipokuwa kukiuka taratibu za kiserikali. Kwa hiyo, mimi kama msimamizi basi lazima nihakikishe kwamba taratibu za kiserikali zinafuatwa kikamilifu na wala sio kipungufu.

Vile vile namuomba atupe muda, ili wizara ikae pamoja na serikali kuona hali hii itaweza kutatuliwa kwa namna gani, kwa sababu watu wenyewe tangu warejee leo ni ya pili tu, basi ni vyema tuwasikilize na wao, ili tujue hali ya huko na halafu tupate kujua namna hatua za kuchukua. Mhe. Mwenyekiti, naomba atupe muda na tutamuarifu na wala asiwe na wasi wasi hakuna cha kuficha.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa maelezo ya Mhe. Waziri pamoja na ufafanuzi ambao ameutoa. Lakini nataka nimuulize swali moja tu la mwisho na akinijibu basi nitasema tuendelee. Mhe. mwenyekiti, kwa mara ya mwisho karafuu zimeuzwa kama sikosei zimeuzwa nje kwa bei ya tani 1 *Dollar* 12 elfu. Je, hizi karafuu ambazo hawa watu wamekwenda kuziuza kule nje ameuza kwa bei gani?

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Salmin Awadh Salmin hataka kustahamili. Kwa bahati mbaya karafuu hizi zimeuzwa kwa tani 1 kwa *Dollar* 8500.

Mhe. Salmin Awadh Salim: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Kifungu 0401 – Idara ya Mipango na Sera Sh.384,790,000/=
Kifungu 0501 – Idara ya Viwanda

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu waliotangulia kumsifu, kumpongeza pamoja na kumshukuru Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa umakini wake na kwa jinsi alivyojibu hoja zetu mbali mbali naamini imepunguza mjadala katika mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, jambo moja ninalomsifu Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa lugha ya mtaani tunasema yeye ni kaniki hafichi uchafu. Kwa hivyo, linalokuwa suala hata kama linahusu serikali yeye huwa haoni tabu na wala hatafuti maneno kusema.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ya Viwanda kwenye mchango wangu mimi nilikuwa ni mmoja wapo ninayezungumzia juu ya changamoto zinazotukabili katika maendelo ya sekta hii. Katika majibu yake ukiondoa yale mambo mengine yanayohusu Muungano, ambayo mimi naamini wananchi wa Zanzibar watayamaliza karibu tukijaaliwa *Inshaallah* ndani ya miaka miwili. Vile vile yalikuwa pia masuala yanayohusu sekta nyengine ambazo zingekuza uwekezaji katika Sekta ya Viwanda ikiwemo uimarishaji wa miundombinu.

Mhe. Mwenyekiti, alipolijibu hili Mhe. Waziri nilimfahamu, yeye kama yeye amejivua, kwa sababu alisema ili Sekta ya Viwanda iimarike katika Sekta ya Miundombinu yeye hana madaraka, kwa sababu masuala haya wenye dhamana ya kusimamia miundombinu ikaimarika ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na ametaja hapa kuanzia bandari, uwanja wa ndege na huduma zake, barabara zinazoweza kuhimili mambo haya pamoja na huduma nyengine.

Sasa kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, serikali inawajibika kwa pamoja katika Baraza hili, basi nataka kauli ya serikali, kwamba hizi changamoto ambazo Mjumbe wa Baraza la Mawaziri amezitaja hapa kuwa zinakwamisha utendaji wa wizara yake katika kukuza Sekta ya Viwanda.

Serikali kwa ujumla wake ina mpango gani kuyashughulikia maeneo hayo, ili kuona sekta hii inaimarika na sisi tuingie katika ushindani kwenye eneo hili la Afrika Mashariki na masoko mengine kama vile *COMESA* na *SADC* kama ilivyokuwa wazalishaji wengine walivyowekeza katika Sekta ya Viwanda. Mhe. Mwenyekiti, naomba kauli ya serikali. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, katika kutoa ufafanuzi hasa katika eneo

hili la changamoto zinazoikumba biashara zetu hapa Zanzibar. Pili vile vile nataka nimpongeze sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa *concern* yake juu ya jinsi serikali tulivyojipanga katika kuondoa hizi changamoto au kukabiliana nazo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme katika maeneo mawili makubwa. Kwanza kutokuendelea kwa viwanda moja linalosababisha ni kuwa na umeme wa uhakuka. Mhe. Mwenyekiti, narudia kutokukua na kuendelea kwa viwanda hapa Zanzibar ni kutokuwa na umeme wa uhakika. Sasa nataka nieleze jinsi tulivyojipanga.

Kwanza tumeangalia maeneo mbali mbali ya kuweza kupata umeme mbadala kwa upande wetu wa Zanzibar, tumekuwa na wataalamu wengi na kila mtaalamu ameeleza sifa za kila aina ya umeme. Kwa mfano, umeme wa maji, upepo, jua, takataka, gesi, mafuta kwa maana ya *diesel*, yaani kila mtaalamu ameeleza sifa na ubora wake.

Lakini sisi kama wasimamizi wa mipango ya nchi hii tumewaomba wenzetu wa *European Union* waje watushauri ni umeme wa aina gani, ambao kwa kufupi utakuwa ni endelevu na utakuwa na bei nafuu kwa wananchi wetu, kwa maana ya *sustainable and affordable*.

Kwa hivyo, wenzetu wamekaa hapa wataalamu kutoka Ujerumani na kuangalia aina zote za umeme ambazo Zanzibar zinaweza kuzalishwa na kutupa ripoti na tukushauri kwamba umeme *sustainable and affordable* kwa upande wa Zanzibar ni umeme wa upepo. Kwa maana hiyo, tayari tunaandaa waraka, ili tuweze kuuwasilisha serikali.

Sasa kabla ya kuwasilisha waraka huo serikali tayari wameshajitokeza wawekezaji mbali mbali ambao wanataka kuwekeza katika aina tofauti za umeme. Mhe. Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa upande huu ni changamoto moja kubwa tunakabiliana nayo na tuko katika hatua za kuweza kuona mwelekeo wa kuweza kupata umeme.

Vile vile katika hiyo ripoti ya Wajarumani wenzetu wa *European Union* wametushauri kwamba tuwe unao umeme angalau *between five and ten mega watts* kutoka kwenye takataka, kwa maana ya kuweka mji wetu safi. Mhe. Mwenyekiti, pia tayari wataalamu wameshakaa na wenzetu wa *ZECO* kuona jinsi gani kwenda na kuzalisha umeme wa aina hii.

Jambo la msingi kwa upande wa serikali na hapa ambapo namshukuru sana *Attorney General* yumo kwenye ile Kamati ya *Negotiate Committee* ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa maana ya *Power Purchase Agreement*, yaani ni mkataba ambazo serikali tutawekeyana na wale ambao watakaozalisha umeme juu ya ununuzi wa umeme, kwa sababu tunataka umeme wetu uwe ni *affordable*.

Kwa hiyo, lazima kuwe na uwezo wa ku-*negotiate* na hawa wawekezaji na Mwanasheria Mkuu tunaye na wataalamu wengine watafanya hiyo kazi wakati utakapofika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa umeme nataka nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba kazi tunaifanya na kila itakapokuwa kazi inakaribia kuwiva, basi hatutasita kuja kutoa taarifa katika Baraza lako Tukufu. *(Makofi)*

Eneo jengine ambalo nataka nimtoe wasi wasi ambalo amelizungumzia sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hamza Hassan Juma jana amediriki kusema kwamba wizara tatu tukae pamoja na mimi kwanza sikulifikiria kwamba nikae na Wizara ya Biashara na nilifikiria nikae na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Lakini sasa kwa sababu ameingiza na Wizara ya Biashara, basi nimelipokea na kutakata pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa maana ya *development* ya *Port* ya Mpigaduri, yaani ujenzi wa Bandari mpya ya Mpigaduri. *(Makofi)*

Kwa kweli Mhe. Hamza Hassan Juma amesisitiza sana jana kwamba tuangalie *Public Private Partnership* (*PPP*). Mhe. Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe, kwamba tayari wapo wawekezaji ambao wanataka kuwekeza katika ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hivi sasa tunaweka pamoja zile *information* zao, kwa sababu huwezi tu mwekezaji anakuja ukamkabidhi na huwezi kujua uwezo wake, hivyo tunaweka pamoja zile *information* zao. Katika kipindi kifupi tayari nimeshakaa na Mhe. Waziri mpya wa Miundombinu na Mawasiliano na tumeshapitia waraka ambao atauwasilisha kwenye

Cabinet kuona zile *information* zote za mwekezaji ambaye anataka kuwekeza Bandari mpya ziko katika waraka wake.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu pamoja na Mhe. Hamza Hassan Juma wavute busira na hizi changamoto kila tutakapokuwa pamoja wazanzibari, basi naamini kwamba changamoto hizi tutaziondoa. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba namna anavyojibu hoja Mhe. Waziri Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ndivyo ambavyo serikali makini inapaswa ijibu na nadhani kama ingekuwa tunapata majibu kama haya basi hoja nyingi zingepungua. Kwa hivyo, nampongeza kama nilivyompongeza Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi naimani kwa uwezo aliotuonesha Mhe. Omar Yussfu Mzee siku moja namtabiri atashika madaraka makubwa sana katika nchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea. Mhe. Mussa Ali Hassan.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri. Wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la kuwa na viwanda Zanzibar, wakati Zanzibar ni serikali na halafu ni nchi, kwa nini hatuna viwanda kabisa na sababu ya umeme naona hairidhishi, kwa sababu viwanda hapo mwanzo tulikuwa navyo na vilikuwa vinafanyakazi na umeme ndio huu. Kwa hivyo, suala hili bado sijaridhika, kwa nini hatuna viwanda na hii Zanzibar ni nchi? *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Mimi nasema kwamba swali hilo aliuliza Mhe. Mwakilishi. Kwa kweli nataka nimhakikishie kwamba Zanzibar ni nchi nakubaliana na yeye sana na viwanda ni muhimu sana. Lakini kutokana na sababu zile pale serikali ilipokuwa na viwanda vingi tu na viwanda vile vilikufa kwa sababu gani, kwa sababu havikuweza kukidhi haja ndio vikafa.

Kwa hiyo, basi serikali imejitoa katika masuala kufanya biashara ya viwanda na badala yake tunawaita wawekezaji na wafanyabiashara wawekeze katika viwanda. Kwa maana hiyo, serikali kama serikali haifanyi biashara na wala viwanda, isipokuwa tunawaita wawekezaji waje wawekeze. Mhe. Mwenyekiti, wawekezaji masharti yao wanataka kuona miundombinu imekamilika katika nchi ndio waanze kuwekeza, wanataka waone umeme na wala sio huu.

Kwa mfano, pale Mtoni Kiwanda cha Bagharesa umeme ukikatika kwa muda wa dakika tano, kiwanda kinakula hasara si chini ya milioni 2 au 3, kwa sababu ile mitambo au mota wakati wa kuanza zile kama gari wakati wa ku-*start* inatumia mafuta mengi na wakati wa kwenda inapunguza kutumia mafuta. Kwa hivyo, ile mota au mitambo wakati wa kuwashwa ile inatumia umeme mwingi sana.

Kwa maana hiyo, washa zima kwa siku moja mara tano kiwanda kinapata hasara mpaka shilingi milioni 10 kwa siku moja, yaani ile washa zima, kwa sababu *starting* ndio umeme unakwenda mwingi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la umeme wa uhakika na vile umeme wenyewe uwe na bei ya chini. Kwa mfano, ikiwa hapa Zanzibar kuna kiwanda na Kenye kuna kiwanda na Uganda kuna kiwanda na soko la bidhaa ile iko Afrika ya Mashariki, umeme Unguja ukawa ghali kuliko Uganda, basi tayari huyu mtu hawezi kuuza bidhaa ile katika Soko la Afrika Mashariki, hivyo lazima umeme upatikane na wala usiwe wa kukatikakatika tena uwe wa bei ya chini.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi astahamili serikali imejipanga kuona kwamba viwanda sasa vinafufuliwa na *Inshaallah* vitafufuliwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba atufahamu Mhe. Mwakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kuhusu suala la viwanda sijaridhika, kwa sababu uwezo wa viwanda vidogo vidogo katika majimbo yetu vinaweza kufanyika hasa katika Viwanda vya Kufanya Usumba au Kuchonga Mbao kwa vitu vidogo vidogo na hata hivyo vinashinda basi kutokana na umeme, wakati *units* ndogo tu zinaweza kupatikana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba viwanda vidogo vidogo vipo nchini na vinaendelea. Kwa hivyo, ningemuomba na yeye katika jimbo lake aanzishe na afike wizarani kwetu na tumpe kila aina ya msaada, ili katika jimbo lake nako aanzishe viwanda vidogo vidogo. Lakini katika majimbo mengine viwanda vidogo vidogo vipo. Kwa mfano kwa Mhe. Hamza Hassan Juma vimejaa kule tena anatuletea washiriki wengi katika Saba Saba na wanatoa vitu vizuri sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Mwakilishi na yeye aje, ili katika jimbo lake tupate watu wa kuweza kushiriki katika Maonesho ya Saba Saba na viko vitu vizuri tu, kama vile Viwanda vya Sabuni, Seremala *Welding*, hivyo namkaribisha sana Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kwa hiyo katika huu mchango wa Mhe. Mohamdraza Hassanali Mohamedali na yeye atapata.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, na fedha za Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali zipo. Kwa hivyo, yeye aje tu. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kuhusu suala la viwanda kuendesha sisi Wawakilishi wa Majimbo uwezo huo utakuwa haupo. Mimi nafikiri Mhe. Waziri angalau angelitoa misaada ya mikopo hata huo Mfuko wa Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali ukafika huku majimboni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tayari huo mkopo wa Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali anasema Mhe. Waziri ukitolewa tu utapata kwenye jimbo lako. Kwa hivyo, nadhani tuendelee. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Wakati nilipokuwa nikichangia mchango wangu kwa njia ya maandishi nilimuomba Mhe. Waziri kujua ile hatima ya Kiwanda kile cha Mahonda, kwa sababu tumepata mshtuko wananchi wa kuona kile kiwanda siku hadi siku kinaibiwa vifaa na ile ni mali yetu au ya serikali na ni matunda ya Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tulitaka kuona kiwanda kile wananchi wanaendelea kufaidika, lakini tunaona siku hadi siku vitu vinazidi kupotea na mwekezaji yupo, vitu vinaibiwa na walinzi wapo na wala hatuelewi ni kitu gani. Mhe. Mwenyekiti, nataka kujua Mhe. Waziri ana mkakati gani juu ya mwekezaji huyu kuweza kuondoa kadhia hii ya kuondolewa vitu siku hadi siku.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kweli Mhe. Panya Ali Abdalla ameleta hapa kwa maandishi mawazi yake hayo. Lakini nataka nimhakikishie kwamba mimi kama Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko nimechukua *personal interest* kuona kama kile kiwanda hali kilivyo na mambo yaliyopita nyuma hivi sasa yasitokee tena.

Kwa mfano, juzi tu nimesikia kuna wanya wa umeme unafukuliwa katika mashamba ya miwa ya Mahonda. Kwa kweli nimetoka mwenyewe mpaka katika shamba la Mahonda na nimeshuhudia wanya unafukuliwa na nikenda mpaka *store* na hiyo *store* ya Mahonda kuna maghala kumi na 11 na yote nayajua kwa moyo na bidhaa ndani nazijua zote zilivyokaa na kimoja tu kikiondoka basi najua kwamba hapa kimeondoka kitu. Kwa hivyo, ule wanya nimeukuta umefukuliwa na umetiwa store na picha yake ninayo nimeichukua kwa simu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilimwambia mwekezaji kwa nini umechimba huu wanya wa umeme, akaniambiwa kwamba kwa sababu wanya unaibiwa na wananchi wanakwenda usiku na kuchimba mashimo na wanya wanaukata mapande na kuuchukua. Kuna sehemu nyengine wanya iko chini ya nyumba ya mtu na huyo wanya umepita basi nyumba inataka kuangushwa kwa ajili ya kuchukuliwa wanya.

Kwa hivyo, tumeona kwamba wanya huu unaibiwa na wananchi na halafu tunaambiwa sisi ndio tunaouimba, basi tumeichukua na kuuhifadhi katika hii ghala. Kwa maana hiyo mimi nikamwambia basi huu uliobakia ambao uko kwenye hii ghala usiuguse na uache kama ulivyo na serikali yenyewe itaamua namna gani ya kufanya, hivyo wanya huu uache kama ulivyo na ule ambao uko kwenye ardhi basi uachi kama ulivyo mpaka serikali itakapochukua taratibu za kufanya kuhusu wanya huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa habati mbaya ule wanya wa kwenye ghala umo mpaka leo, lakini ule ambao ulioko kwenye shamba basi siku ya pili yake ukachimbwa wote na kumalizwa. Kwa hiyo, ni kweli wanaoiba mali ya kiwanda sio tu wale wawekezaji wa kiwanda, pia kuna wananchi ambao si waaminifu wanachimba zile wanya na kuiba, wanaiba mota na vitu kadha wa kadhaa. Kwa maana hiyo, mwekezaji kwa hapa mimi simlaumu.

Lakini wananchi wa maeneo ya pale wanya unachimbwa wanauona, viongozi wapo na wanaona, polisi wanaona, kwa sababu wanya huwezi kuubeba. Kwa mfano, wanya mita moja uzito wake kama pembe ya tembo na wala mtu hawezi kubeba kirahisi. Kwa hivyo watu wote wanamuona anavyotoka nayo. Nakiri kwamba sio tu muwekezaji lakini na sisi vile vile tunashiriki katika masuala haya. Ningeomba basi hii ni mali ya serikali tuitunze na sisi kama serikali tunamuangalia kwa macho mawili muwekezaji asichukue chochote katika maghala haya. Ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana, namshukuru Mhe. Waziri kwa ufatiliaji, waya wa umeme nimesikia upo lakini hivyo vyengine ndio vimetoweka vimepotea, huo nasikia umechimbwa umewekwa.

Lakini mimi bado nina masikitiko kwa muwekezaji huyu bado serikali ijipange, kwa sababu itaendelea siku hadi siku mpaka kiwanda kitabomoka kile. Bado naomba serikali ijipange kuhusu Kiwanda cha Sukari muwekezaji kama anaweza kuwekeza basi awekeze ili tufaidike serikali inufaike na wananchi wa pale wananufaike.

Baada ya hayo nasema tuendelee.

Kifungu 0501 Idara ya Viwanda Sh. 273,228,000

Kifungu 0601 Idara ya Biashara

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, jana wakati nachangia huku nikiwa makini katika kuangalia kwamba sikiuki kanuni ya 59(3) kwa maana ya kuwa na uhakika wa kile ninachokisema.

Nilisema kwamba wafanyabiashara wa makontena pale Darajani hawapewi leseni, tangu 20011 mpaka sasa hivi hawajapewa leseni. Hapa napenda nimpongeze Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, hapa angalau yeye kwa kutamka kwamba ataiyomba mamlaka inayohusika na leseni iwape leseni. Kwa hili Mhe. Waziri wa Biashara, nampongeza ingawa nitataka anijibu tu ikiwa mamlaka hii itakataa je, kutoa leseni atafanyaje?

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimesikitishwa sana wakati Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mhe. Mwinyihaji, aliposema kwamba hapana anayebaguliwa watu wote wanapewa leseni. Hii si kweli mimi niliijengea hoja yangu nikiwa nimeisimamisha katika misingi miwili kwa kutumia ushahidi wa macho ambayo ninayo barua hii ya wale watoaji wa mada pamoja *circumstantial* na *evidence* ambazo hata Mahakimu wanatumia mahakamani kuwatia watu hatiani kwa kutumia ushahidi wa kimazingira.

Wale watu Mhe. Mwenyekiti, wanabaguliwa mno, hawapewi leseni hawa watu wa Makontena pale Darajani. Sasa ninachotaka nimepata wasi wasi, Mhe. Waziri kanipa matumaini lakini huyo Waziri anayehusika na mambo ya leseni, anayehusika na mambo ya Manispaa kanipa wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika hili nataka nipate maelezo ni lini wale Wazanzibari waliyoko pale watapewa leseni sawa sawa na Wazanzibari wengine walioko Matemwe, walioko Makunduchi, walioko Vitongoji Pemba, wale ni Wazanzibari sawa sawa na Wazanzibari wengine, wasibaguliwe. Ushahidi unaonesha kwamba wanabaguliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kwanza nilimuomba sana Mhe. Nassor ile kauli aliyosema Wapemba wasibaguliwe aiondoe, si nzuri. Sasa hivi hatuko huko. Alilitumia sana neno hilo Wapemba wanabaguliwa, wanaonewa, wana nini. Si neno zuri, hatuko huko wala hatuendi huko.

Pili nikasisitiza wafanyabiashara wanaouza pale sio Wapemba tu, kuna Wamachinga pale, kuna Wadimani, kuna wa sehemu mbali mbali waliopo pale. Kwa nini asisitize Wapemba wanabaguliwa, Wapemba wanaonewa. Sivyo hivyo, hatujengi hivyo tunabomoa.

Sasa Mheshimiwa kulikuwa kuna silaha kibindoni hii hapa sikutaka kuitoa, hapa Mhe. Mwenyekiti nina *ruling* ya Mahakama pale kulikuwa kuna kesi Mahakamani ya wafanyabiashara Mahakamani ya wafanyabiashara wale. Pale wale walikuwa hawapewi leseni makusudi kwa sababu waondoke. Sasa *ruling* ya Mahakama hii hapa Mheshimiwa tukimaliza nitampa aisome, wameshindwa wafanyabiashara wale waondoke. Hiyo ndiyo *ruling* iliyopo.

Namuomba Mheshimiwa asitetee kitu ambacho hakina uhakika, *ruling* ya Mahakama hii hapa inasema wameshindwa *appeal* yao waondoke. Ndio maana wakati wote ule walikuwa leseni hawapewi. Sio kama wanabaguliwa kwa kuwa ni Wapemba. Kauli ile aifute Mheshimiwa. Ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani jana na hata leo nimesema wale ni Wazanzibari, sawa sawa na Wazanzibari wengine, sikusema kama wale ni Wapemba siwezi kufuta neno ambalo sikulisema.

Nataka wizara iniambie ni lini wale wafanyabiashara watapatiwa leseni. Lakini siwezi kufuta neno ambalo sikusema na *hansard* zipo. Sikusema kama wale Wapemba wanabaguliwa sikusema, nimesema kama wale ni Wazanzibari na nikatoa mifano ya Matemwe, Kusini Makunduchi na Vitongoji yaani Kusini Pemba. Kwa maana ya Wazanzibari waliojumuika. Siwezi kufuta neno ambalo sikulisema.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri mkisaidie kiti ili tuweze kwenda vizuri na shughuli yetu inayotukabili mbele. Naomba msaada wetu nyote kwa ujumla wenu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mheshimiwa kama anasema hakusema lakini mimi nimesikia kwa sikio langu sikuwemo humu nilikuwa kwenye redio nasikiliza sana na yaliniuma sana maneno yale mimi Mheshimiwa. Na kwa sababu yameniuma hakujua yeye sababu ya wale kwa nini hawakupewa leseni, angesema ukweli. Wale hawakupewa leseni kwa sababu kadha, kadha, sio kusingiziwa kwamba wanaonewa kwa sababu Wapemba. Hilo ndio lililoniuma sana mie Mheshimiwa.

Sasa nimekuja na *ruling* hii hapa naomba nikukabidhi baadaye umpe Mheshimiwa aisome. Sasa lakini Mhe. Mazrui, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, keshasawazisha. Sasa hivi tunalizungumza hilo, tunalisawazisha tuone tutafikia wapi na leseni watapewa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama kuna kitu ninachokifahamu pale ni uwepo wa wale wafanyabiashara pale. Mimi najua karibu 50% ya wafanyabiashara wa pale ni wa Matemwe na ndio sikutaja Wapemba. Katika hili ni lazima tuweke mambo vizuri. Wazanzibari milioni moja na laki mbili wanatusikiliza sisi. Tunachodai ni haki, ningesema haki sawa kwa wote, lakini naogopa nisije nikaambiwa naleta sera za kichama.

Naomba watu wa serikali katika kuwahudumia wananchi musiwe *bias* mutoe hii *national cake* iwe *evenly distributed through out Zanzibarians* musiweke huyu anatoka Kusini huyu anatoka Kaskazini, sisi sote ni wamoja. Huwezi sasa hivi kumbagua Mpemba na Mtumbatu. Mimi binafsi hivi sasa hivi familia yangu iko Tumbatu, ni Watumbatu, familia yangu iko Kusini, Umakunduchini iko.

Siwezi kusema kitu kama hicho. Ninachosema wale ni Wazanzibari ni lini Mhe. Mwenyekiti, atanieleza kwamba wanataka kutumia *ruling* ya Mahakama au wataendelea kuwaachia wafanyabiashara. Na ikiwa wataendelea kufanya biashara wapewe leseni. Watapewa lini leseni.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kidogo tukumbushane ndugu Wajumbe chombo hiki huwa hakishindani juu ya maneno ambayo tunayoyasema. Chombo hiki kina *hansard* na kama Mjumbe anasema hakusema au kasingiziwa Mwenyekiti, una wadhifa wa kuitisha *hansard*.

Lakini nasema tusifike huko, *concern* ya Mhe. Saleh tumeifahamu na *concern* ya Mhe. Mwinyihaji tumeisikia. Ninachotaka niseme ni kwamba *ruling* ya Mahakama imeshatoka. Kwa hivyo hawa ni Wazanzibari, tuangalie njia muafaka ya kuweza kuwasaidia kufanya biashara zao. Lakini kwa *ruling* ya Mahakama katika maeneo yale serikali sasa hatuwezi. Tunaweza tukawasaidia katika maeneo mengine na kuwapa maelekezo mengine ili waweze kufanya biashara zao, waweze kukidhi mahitaji yao. Hilo namuomba sana Mhe. Saleh Nassor, atuachie sisi serikali tutaliangalia na tutaona jinsi gani ya kuweza kusaidiana baina ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Biashara na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Saleh Nassor, nakuomba sana turuhusu hichi kifungu kipite ili baadaye tuweze kufanya haya majukumu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, penye wengi hapaharibiki jambo, nadhani katika hili nimpongeze sana Mhe. Waziri anayehusiana na mambo ya madukhuli, tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipochangia katika sehemu hii nilimwambia Mhe. Waziri kama wananchi wa Zanzibar wameitikia wito wa kilimo cha mwani na nikamwambia Mhe. Waziri kama kuna haja ya kuona kwamba Shirika la ZSTC wanaingia na wao katika ununuzi huu wa mwani ili kuwasaidia wananchi katika zao hili. Kwa sababu wameitikia wito wa kilimo hichi na wanazalisha kwa wingi lakini bei yao wanayoipata ni ndogo sana.

Nilimshauri Mhe. Waziri katika kuchangia kwangu kwamba kuna haja ya hili Shirika kuingia na wao kununua ili kuwasaidia wananchi. Lakini Mhe. Waziri hakunijibu kwa hiyo nataka nipate hayo maoni vipi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, suala hilo nakumbuka nililijibu lakini nitalijibu tena. Naelewa kwa nini Mhe. Subeit amekuwa bado hajaridhika na jawabu nililompa.

Kwa sababu katika Zanzibar nzima Wilaya ya Micheweni ndio Nambari One kwa kutoa mwani mwingi, kwa hivyo *concern* yake naielewa sana. Nilimwambia kwamba ZSTC imo katika mageuzi tena mageuzi makubwa. Tumeitwika mzigo mmoja tu wa karafuu, bado hatujafika pahala pake. Tutapomaliza karafuu, tutakwenda kwenye mwani na Mhe. Mussa pale amesema anataka pilipili hoho na mambo mengine chungu nzima. Lakini tuende hatua kwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, dhamira nzuri ipo na haturidhishwi hata kidogo na bei ambayo kwamba wanunuaji wa mwani wanawapa wakulima. Tungehisi angalau kilo moja ingefika shilingi elfu moja. Lakini tupe muda kidogo baadaye ZSTC ikishakujishika kisawasawa tutaipa jukumu hilo. Naomba utustahamilie.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nashukuru Mhe. Waziri kanipa moyo kwa hiyo tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia katika sekta ya biashara suala la biashara baina ya Zanzibar na Tanganyika, hasa juu ya suala la usafirishaji wa magari, kwamba mamlaka inayohusika na utozaji ushuru hapa Zanzibar ni mamlaka ile ile inayohusika na utozaji ushuru kwa upande wa pili wa Jamhuri ambayo ni mamlaka ya mapato Tanzania TRA.

Nilitaka kauli, nimemsikia Mhe. Waziri hapa alipokuwa akinijibu na yeye kajumuika na sisi katika kulalamika juu ya hali hii kwamba kila mmoja inamkera. Sasa ikiwa sote hatuna ufumbuzi wananchi wetu tunawachanganya kabisa. Nilikuwa nataka kauli ya serikali juu ya kadhia hii.

Nataka kauli ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa ummoja wa kitaifa inafanya nini kupata ufumbuzi na kama hakuna ufumbuzi wenzetu wamegoma, tunachukua hatua gani juu ya TRA ambayo inaonekana imeundwa ili kuua uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwa kuliona hili tatizo. Lakini vile vile nataka nimpongeze Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba hili tatizo amelifikisha kwangu kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na mimi na

Mhe. Hamza Hassan, Mhe. Ali Salim Haji, tumekutana na hawa wafanyabiashara wa magari ambao wameeleza malalamiko yao.

Kimsingi kila mfanyabiashara alikuwa na sababu zake na maelezo yake yaliyowafanya gari zao, walisema siku hizi karibu 500 kuzuiliwa pale Dar-es-Salaam. Tulichowaomba sisi, kwamba kila mmoja alete zile *entry* zake ambazo zitaonesha ile kodi ambayo amepaswa kulipia kule na baadaye tumekubaliana katika kikao kile na Mhe. Hamza Hassan alikuwepo. Kwamba nitachukua bidii ya kuwafuata wenzangu pamoja na vielelezo kwenda kukaa nao Dar-es-Salaam ili tuwaelezee *concern* za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa wao peke yao tumeona hawataliweza.

Mpaka sasa hivi mimi kama Waziri mwenye dhamana sijapokea bado zile *documents* hata moja. Narudia tena, nimewaahidi baada ya kumaliza bajeti tu nitafanya kazi hiyo. Lakini mpaka sasa hivi bado zijapata vile vielelezo, kwa sababu vile ndio *evidence*. Mhe. Hamza Hassan atakubaliana na mimi kilitolewa kimoja pale tukakiona ambacho kuna hoja nzito ya kuweza kuwambia wenzetu kulingana na kielelezo kile.

Sasa bila ya vielelezo vile mdomo mtupu wa kwangu hautoweza kujenga hoja. Namuomba sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hamza Hassan Juma na Waheshimiwa wote humu ndani ambao wanakereketwa na hili, watutafutie vile vielelezo. Mimi nawaahidi nikimaliza bajeti tu nitakwenda kukaa na wenzangu. Nitaanza na Kamishna Mkuu wa TRA lakini baadaye nitazungumza na Waziri vile vile mwenye dhamana.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Jussa tusaidiane kwa hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niwahakikishie Mawaziri wetu wote kwamba sisi hatuna mashaka juu ya nia yao njema na uzalendo wao katika kusimama kama tulivyosimama sisi katika kuwapigania wananchi wa Zanzibar maslahi yao. Hata siku moja hatutilii mashaka uzalendo wao. Lakini tunajua kuna njama za makusudi za upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano kuua uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kila biashara ambayo inashikwa na Zanzibar basi inaumbiwa mbinu ili ipate kuua maisha ya wananchi wa Zanzibar. Hii ndio faida ya wananchi wa Zanzibar wameivuna katika muungano huu, kuuliwa, kuuliwa, kuuliwa kimaisha mpaka watu waridhike wapate ku- *surrender* tukabidhi kila kitu kwao Zanzibar itoweke, hii ndio Sera ya Muungano huu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa Mhe. Omar (Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo). Nataka nimpe *chance* nyengine lakini tangu zamani haya na hili si la mwanzo, zimeuliwa kila aina ya biashara zilizokuwa zinaonekana zinapita Zanzibar. Sasa imeonekana biashara hii kama nilivyotoa katika mchango wangu jana ndio pekee iliyobakia angalau wananchi wa Zanzibar wanapumulia. Sasa na kwa hili pia wanataka kubakwa koo pia wasipumue katika hili. Tutapumua tu tukijaaliwa mwaka huu *Inshaallah.*

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema nampa *chance* Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Serikali kulifuatilia hili. Lakini tunasema kabisa katika hili ikiwa halipati ufumbuzi, Baraza hili kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar tunaowakilisha humu tutafanya maamuzi magumu ya kuifukuza TRA Zanzibar. Mheshimiwa tuendelee. Ahsante sana.

Kifungu 0601 Idara ya Biashara Sh. 382,700,000

Kifungu 0701 Utumishi na Uendeshaji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kuniona kwa muda huu ingawa nimenyanyuka mara nyingi sikupata fursa hiyo.

Wakati nilipokua nikichangia suala la mafuta na nikategemea katika hichi kitabu angalau tunaweza tukajibiwa humu. Ukaguzi uliofanywa kwenye ukurasa wa 40, “Idara iliendelea na utekelezaji wa lengo la ukaguzi wa maeneo ya biashara kulingana na programu za ukaguzi zilizopangwa kama ifuatavyo:-

(a) Ukaguzi wa vituo vya mafuta, magari ya mafuta na matenki”.

Tulitegemea athari walizopata wananchi wetu kwenye magari yao angalau itatiwa humu kutokana na mafuta machafu yaliyoletwa hapa nchini. Suala hili nimekuwa nalipigia kelele sana mie kuna Wizara tatu msimamizi lakini hatumjui ni nani anayehusika.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Biashara na Masoko kwa kuiomba hii Wizara iwe mikononi mwake na ndio Wizara ya Biashara ndio dhamana.

Huku ZRB wanakushanya kodi, ukienda Idara ya Ardhi, Makaazi, kuna kibali chake mbali. Imekuwa mzunguko mkubwa. Nilikuwa nataka ufafanuzi hapa kama alivyoomba Mhe. Waziri wa Biashara awe dhamana mtu mmoja sio huku ZRB inavuta, Idara ya Ardhi, Upimaji inavuta, huku Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inavuta. Mzunguko umekuwa mkubwa, mafuta yanayoletwa machafu na magari sasa yapo kwenye boda yamekaa muda mrefu. Nataka ufafanuzi wa suala hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika ufafanuzi wangu pale nilieleza na naona Mhe. Jaku Hashim, hajaridhika nafikiri anataka maelezo zaidi.

Nilisema kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inashughulika na suala la kuhakikisha kwamba pampu zote zinazopampu mafuta kutia katika magari zinatoa vipimo sahihi. Lakini suala la mafuta kwamba yanayokuja kuwa machafu, pindipo tukianzisha Shirika letu la ZBS basi tutafanya kila mpango tupate chombo cha kupimia mafuta yanayokuja nchini, ingawa chombo chenyewe ni ghali sana.

Kwa hivyo ZBS itakuwa na jukumu la kuyapima mafuta yote yatakayoingia nchini. Kwa sasa hivi hatuna chombo cha kupimia. Sasa hivi kwa mujibu wa sheria naamini kwamba Wizara ya Ardhi, Nishati, ndio kwahala ambapo kuna sheria ya kuangalia viwango vya mafuta. Mimi naamini kwamba Mhe. Jaku Hashim ikiwa atavumilia kidogo baadaye katika siku zijazo ZBS ikianza kazi basi suala hili litadhibitiwa, kwa sasa hivi si rahisi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hili suala la ZBS tumepitisha muda mrefu, utekelezaji wake bado imekuwa kilio. Mhe. Hamza Hassan Juma, huwa anasema hapa kwamba tunapitisha sheria nyingi lakini utekelezaji wake haupo. Hili shirika lipo, vyakula vinauzwa madukani hali ya kuwa vimekwisha muda wake, sasa bado, bado, bado. Mimi aniambie kuna wataalamu wangapi walioajiriwa kuhusu suala hili la ZBS na lini itaanza kazi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ZBS ilikuwa haina majengo, sasa hivi majengo tumeshapewa na bajeti hii ikipita kuna *funds* hapa tutafanya *repair* na mwaka huu huu tuaanza kazi *inshaallah*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka ufafanuzi kuhusu hili suala la mafuta tukamate Wizara moja tu kulikuwa na watu watatu wote mzunguko kama Wizara ya Biashara basi iwe ni biashara tu hilo suala la biashara lipo. Leo Wizara ya Fedha dhamana yeye, leo Wizara ya Ardhi, Upimaji dhamana yeye, leo Wizara ya Upimaji dhamana yeye. Serikali yote ipo hapa watupe dhamana mtu mmoja tukamate mmoja tu kuliko mzunguko wote huu.

Mhe. Waziri Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri wa Biashara kwa maelezo yake mazuri. Lakini vile vile nataka nimsaidie tu kidogo Mhe. Jaku, Hashim Ayoub.

Kila taasisi, kila Wizara ina majukumu yake katika sekta hii ya mafuta. Majukumu haya Mhe. Mwenyekiti, wewe ni shahidi na Wajumbe hawa wote ni mashahidi kwamba yapo kwa mujibu wa sheria zetu tulizozitunga ndani ya

Baraza hili. Jukumu nililonalo mimi kama Wizara ya Fedha ni kusimamia kodi. *Interest* yetu sisi katika upande wa mafuta ni suala la kodi na wala huwezi ukaliondoa kwa kupitisha vifungu, unaweza ukaliondoa kwa kubadilisha sheria.

Jukumu walilonalo Wizara ya Biashara ni kuangalia ubora wa mafuta na viwango. Kwa hivyo kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba chombo kimeshaundwa na mimi nakubaliana sana na *concern* ya Mhe. Jaku Hashim, kwamba chombo hiki basi kisimamishwe haraka ili kuweza kuchukua majukumu yake. Jukumu walilonalo Wizara ya Nishati ni suala zima la kuweka Sera ya Mafuta (*Exploration*) na kuangalia jinsi watakavyosimamia upatikanaji wa mafuta ndani ya visiwa vya Zanzibar.

Kwa hivyo haya majukumu ni majukumu tofauti. Mimi naamini kwamba Mhe. Waziri wa Biashara akishakiweka kile chombo huu utata alionao Mhe. Jaku Hashim, utaweza kuondoka. Nimuombe tu Mhe. Waziri wa Biashara asimame na ahadi yake katika kipindi cha mwaka huu hicho chombo kiweze kufanya kazi ili haya matatizo yaweze kuondoka.

Vile vile namuomba sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ana tatizo lolote ambalo linalohusiana na masuala ya mafuta, kama alivyokuwa anafanya asichoke kushauriana na serikali, nikiwa mimi Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Waziri wa Biashara na Mhe. Waziri wa Nishati vile vile, tutaweza kusaidiana naye katika kutatua hayo matatizo ya msingi anayoyaona yeye.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa hekma za Mhe. Waziri wa Fedha, naomba tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia niliuliza vile vile sababu za kuendelea kukwama kwa miradi ambayo inafadhiliwa kupitia mradi wa *BEST*. Katika Wizara hii nilizungumzia *specifically* suala ambalo lipo katika ukurasa wa 26 kwenye hotuba ya Mhe. Waziri wa Biashara, juu ya suala la ule mradi wa kuendeleza eneo la Uwanja wa Kimataifa wa Maonesho ya Kibiashara.

Katika majibu yake amesema kwamba wao walivyokuwa wanaelewa ni kwamba fedha hizi kwa ujumla wake hazikupatikana kwa upande wa Zanzibar lakini hata upande wa Bara.

Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya kazi zetu tuliwahi kupata maelezo kwamba wanaotoa fedha hizi waliwahi kushauri Zanzibar kwamba ingeweza kuomba kwa sababu kabla ya mwaka huu wa fedha tunaoumaliza mwezi uliopita haujamalizika. Lakini kwa sababu wanaoratibu ni kwa upande wa Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano suala hili likakwama.

Mimi maelezo ya Mhe. Waziri nimeyasikiliza kwa makini nilikuwa nataka kauli ya serikali tu. Hivi kwa sababu mradi huu unaitwa B*usiness Environment Strengthening* in Tanzania, unahusu zaidi uimarishaji wa mazingira ya kibiashara, na kwa sababu biashara si suala la muungano hivi Zanzibar kupitia kwa Waziri wetu mahiri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, hatuwezi kuja utaratibu ambao mimi niliwahi kuupendekeza hapa, kuwe na utaratibu wake wa kuanzisha mazungumzo ya moja kwa moja na washirika wa maendeleo haya yasiyokuwa ya muungano. Ili Zanzibar ikawa inapata fungu lake moja kwa moja na ikawa na mradi wake wenyewe. Ili miradi kama hii sio kwa Wizara hii tu, yote ambayo iliyokuwa inafadhiliwa kupitia mradi wa *BEST* isiwe inakwama katika utekelezaji wake kama ilivyojitokeza katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo ya serikali katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, labda nimsaidie tu kidogo Mhe. Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe kama ifuatavyo. Tumeshakubaliana na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaweza tukafanya mazungumzo na wafadhili katika yale maeneo ambayo tunataraji tuombe au kutafuta misaada. Hilo wameshaturuhusu na tunaendelea nalo. Lakini katika maeneo ya mikopo ni lazima tuwe pamoja nao ili tuweze kushauriana na hatimaye tuweze kusaidiana kwa kufanikisha.

Mhe. Naibu Spika, *concern* ya Mhe. Ismail Jussa nataka nimuhakikishie kwamba tumeshaianza, lakini unajua na wenzetu wafadhili nao kuna *coordination team*, ambayo mara zote inakuwa ni *UN*. Nadhani mambo haya yakishaiva basi ataweza kupata hiyo taarifa. Ni wazo zuri na mimi nimelipokea siku nyingi kidogo na tunalifanyia kazi, naamini kwamba tutaweza kufanikisha katika upande huu, hasa katika upande wa kuweza kupata misaada, sio kule katika upande wa mikopo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kukumbuka kwamba suala hili nililisimamia kidete sana katika Baraza hili mara tu baada ya uchaguzi, juu ya suala la kuanzisha utaratibu wa kuwa na *consultative group meeting* yaani *(CGM)* kwa ajili ya Zanzibar peke yake kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka kwamba niliwahi kusaidiana naye hata katika kuzungumza na baadhi ya washirika wa maendeleo, kupitia Wawakilishi wao waliopo Tanzania ambao walikuwa tayari kuanzisha utaratibu kama huu kwa upande wa Zanzibar kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano.

Kwa hivyo, imechukua muda mrefu pamoja na kwamba aliwahi kutuahidi katika Baraza hili kwamba lingeanza Oktoba mwaka jana, lakini sasa hivi tunakaribia Oktoba mwaka huu halikuanza. Baadhi ya washirika wa maendeleo hawa walishaonesha utayari katika kulisimamia na hata kuliratibu kwa niaba ya Zanzibar. Kwa hivyo, nashukuru kwamba kaniambia analifanyia kazi.

Isipokuwa nataka aniweke sawa kitu kimoja tu. Sikuridhika na lugha yake aliyoniambia kwamba tumeruhusiwa, yaani kwa maeneo haya yasiyokuwa ya Muungano mpaka turuhusiwe na kuumeni. Lugha hii mimi sikuipenda Mhe. Mwenyekiti. Mimi naamini msingi wa Muungano huu umetajwa vizuri katika katiba ya Zanzibar kwamba huu ni Muungano wa nchi mbili na katika hili hakuna moja aliyetaka ruhusa ya mwenzake, ni makubaliano ya pamoja. Kwa hivyo, nataka ile lugha tuirekebishe kwamba tumeamua kwa pamoja hatungoji ruhusa ya mume ili kuendelea na suala hili, baada ya hapo tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea, wale Wajumbe ambao wanatoka hii kazi yetu itaweza kukwama ikiwa *quorum* haitimii ili tukakamilisha kazi hii. Nawaomba basi wale Wajumbe ambao wako nje wote warejee ndani ili tuendelee na kazi yetu kwa ufanisi zaidi. Tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana na *concern* za Mhe. Ismail Jussa Ladhu, lakini nataka nimwambie tu kwamba kuna sheria ya *Grant Loan and Guarantees*, ambapo hii ni sheria ya Muungano, lakini nataka niseme kwamba basi nirudishe kwa kumkubalia au kwa kusema kwamba tumekubaliana na wenzetu kwamba katika masuala ya misaada tunaweza tukaendelea.

Kifungu 0701 Utumishi na Uendeshaji Sh. 1,072,453,000

Kifungu 0702 Baraza la Biashara Zanzibar Sh. 250,000,000

Kifungu 0703 Mamlaka ya Mizani na Vipimo Sh. 200,000,000

Kifungu 0704 Kamisheni ya Kusimamia Ushindani wa Biashara Sh. 200,000,000

Kifungu 0705 Mamlaka ya Viwango Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Alipokuwa akinijibu Mhe. Waziri aliniambia hiki kitengo kitaanza mwaka huu huu. Mimi nataka anieleze tu katika mwezi gani basi.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiria jawabu lilikuwa tayari limeshatolewa katika suala lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nilichouliza Mhe. Naibu Spika, ni mwezi gani. Yeye ananiambia katika mwaka huu. Kuna mwezi Januari, Februari umeshapita, kuna Oktoba, Novemba na Disemba. Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, sijamsikia vizuri Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mwenyekiti: Ni kuhusu ZBS.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Kuhusu ZBS tukipata bajeti hii tutaanza miezi sita ya ukarabati, halafu ndio shughuli zitaanza. Lakini ni muda mrefu, sio kwamba mkianza kazi mambo yote yatafanyika hapo hapo. Baada ya kupata majengo kuna kununua vifaa hatua kwa hatua. Kwa hivyo, namuhakikishia kwamba ZBS itaanza kazi miezi sita kuanzia hivi sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ofisi yake itakuwa wapi hapo hapo Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Maruhubi Kiwanda cha Sigara.

Kifungu 0705 Mamlaka ya Viwango ZanzibarSh. 250,000,000
Jumla ya Fungu Sh.3,353,000,000

FUNGU 21 - WIZARA YA BIASHARA VIWANDA NA MASOKO

Kifungu 0601 Idara ya Biashara Sh.2,227,000,000

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya matumizi, imejadili na kupitisha makadirio ya fedha za wizara yangu bila mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja Bazara liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji basi wale wanaokubali hoja wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwe na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kutoa taarifa kwamba hotuba ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imepitishwa rasmi kabisa.

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunawashukuru kwa kazi nzuri ya kuweza kupitisha Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa naomba mashirikiano yetu kwa kuanza wizara mpya. Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Tunamwita Mhe. Waziri ili awasilishe hotuba yake.

RASIMU YA KWANZA

HOTUBA YA BAJETI YA OFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO KWA MWAKA 2012/2013

I: UTANGULIZI

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na hatimae kuzingatia Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya na uzima wa kuweza kukutana leo hii katika kikao hichi cha kuwasilisha Bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Aidha, napenda nimshukuru kwa kipekee Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake imara kwa nchi yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu afya njema ili aweze kutuongoza Wazanzibari kwa hekima na busara zaidi.

Mhe. Naibu Spika, napenda niwashukuru Makamo wa Kwanza wa Rais – Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kumsaidia Mhe Rais katika uongozi wa nchi yetu. Aidha napenda nikushukuru wewe kwa kuliongoza vyema Baraza hili Tukufu na kupitia kwako kuishukuru kamati ya kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo inayoongozwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa mashirikiano na miongozo yao.

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa kwamba katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyofanyika tarehe 03 Mei, 2012, ilipelekea kuteuliwa kwa aliekuwa Kamishna wa Fedha za Nje wa Ofisi yangu Nd. Saada Mkuya Salum kuwa Mbunge na hatimae Naibu Waziri wa Fedha wa Muungano. Naomba kupitia Baraza lako Tukufu kumpongeza Mhe. Saada kwa kuteuliwa kwake. Hii inadhihirisha utendaji wake bora uliopelekea mafanikio hayo. Tunamuombea mafanikio katika majukumu yake hayo mapya.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba yangu ya Bajeti ya Serikali mwezi uliopita nilitoa mkono wa pole kwa wananchi wote walioathirika na ajali ya kuzama kwa meli ya MV *Spice Islander II* tarehe 10 Septemba mwaka jana. Serikali haikutarajia kuwa nchi yetu ingekumbwa tena na janga jengine la kuzama kwa meli. *Alipangalo Mungu haliepukiki*. Tarehe 18 mwezi wa Julai mwaka huu, jamii yetu ikakumbwa tena na simanzi na majonzi kufuatia kuzama kwa Meli ya *MV Skagit* kulikopoteza maisha ya watu 144. Naomba kwa mara nyengine tena, kwa niaba yangu, uongozi na wafanyakazi wote wa Ofisi yangu, kuwapa pole na kuwatakia moyo wa subira wananchi wenzetu wote walioathirika na walipoteza ndugu, wapendwa wao na mali zao katika ajali ile.

Mhe. Naibu Spika, mengi yamesemwa kufuatia ajali hii; ya kupeana pole, ya kukosoa na ya kushauri Serikali juu ya hatua za kuchukua ili nchi yetu iimarishe uwezo wa kujihami na kushughulikia majanga. Tayari hatua kadhaa zimeshachukuliwa ili kuimarisha usalama wa usafiri wa baharini ambao ni muhimu kwa wananchi wetu walio wengi.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa hatua hizo, Serikali imeamua kuharakisha utekelezaji wa uamuzi wake wa kununua meli mpya za abiria na mizigo zinazoweza kutoa huduma za uhakika na ufanisi katika visiwa vyetu na mwambao wa Tanzania na Afrika ya Mashariki. Baadae nitaeleza zaidi juu ya mapendekezo ya Serikali juu ya ufanikishaji wa ununuzi huo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa niendelee kwa kusema kwamba Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kimsingi inatekeleza majukumu yake kupitia maeneo matatu makubwa: Tume ya Mipango, Fedha na Utawala na Taasisi zinazojitegemea za SMZ na SMT.

II: MUUNDO NA MAJUKUMU MAKUU YA OFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO

Mhe. Naibu Spika, Kimuundo Ofisi hii inajumuisha Idara 11, Taasisi tisa zinazojitegemea na taasisi tatu za kifedha za Jamhuri ya Muungano. Kati ya Idara hizi 11, Idara tatu na taasisi moja zipo katika muundo wa Sekretariat ya Tume ya Mipango na zilizobakia zinasimamiwa na Fedha na Utawala. Aidha, kati ya taasisi tisa zilizopo, tano zinapata fedha zake kwa njia ya ruzuku kutoka serikalini. Ofisi hii imeendelea kuwa na majukumu ya Kitaifa na yale ya kisekta kama wizara nyengine.

a. Majukumu ya Kitaifa

i. **Mipango:** inaratibiwa na Tume ya Mipango kupitia Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleao ya Kisekta na Kupunguza Umasikini; Idara ya Ukuzaji Uchumi; na Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.
ii. **Mapato:** yanakusanywa na kuratibiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar; Mamlaka ya Mapato Tanzania na Idara ya Fedha za Nje.
iii. **Matumizi:** yanasimamiwa na Idara ya Bajeti na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.
iv. **Mali za Serikali na Mitaji:** zinasimamiwa na Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma na Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi Zanzibar.

b. Majukumu ya Kisekta

Majukumu haya yanasimamiwa na:

i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
iii. Ofisi Kuu Pemba
iv. Ofisi ya Uratibu wa shughuli za SMZ Dar-es- salaam
v. Taasisi nyengine ni Benki ya Watu wa Zanzibar, Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Chuo cha Uongozi wa Fedha na Shirika la Bima.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inafanya kazi kwa karibu na Taasisi za Muungano zikiwemo Tume ya Pamoja ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, Taasisi ya Kudhibiti na Kuzuwia Fedha Haramu, Mamlaka ya Kusimamia Shughuli za Bima Tanzania na Benki ya Posta Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, Utekelezaji wa majukumu haya ya Ofisi unaongozwa na Katiba ya nchi, Sheria za Kodi za Fedha, Sheria ya Manunuzi, Sheria ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Sheria ya Tume ya Mipango na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010, DIRA ya Maendeleo ya 2020, *MKUZA II* pamoja na maelekezo mbali mbali ya Baraza la Mapinduzi na miongozo ya Baraza la Wawakilishi.

III MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI NA YALE YA JUMLA

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kusimamia mapato ya nchi kwa jumla, Ofisi pia inawajibu wa kuangalia na kukusanya mapato ndani ya Idara zake. Baada ya kukusanywa mapato huingia moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na hatimae kutumika katika kazi mbalimbali za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa Mapato ya Serikali, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Serikali ilipanga kukusanya TZS 613.08 bilioni ikiwemo bakaa ya TZS 4.0 billioni iliyoletwa kutoka 2010/2011. Mapato yote yaliyopatikana yalifikia TZS 468.7 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 77 ya makadirio. Mapato ya ndani yalifikia jumla ya TZS 220.82 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya TZS 221.24 bilioni. ZRB ilikusanya jumla ya TZS 109.9 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya TZS 109.6 bilioni.

Mapato yaliyokusanywa na TRA-Zanzibar yalifikia TZS 91.7 bilioni sawa na asilimia 90.5 ya makadirio ya TZS 100.58 bilioni, mapato ya mawizara yalifikia jumla ya TZS 19.2 bilioni sawa na asilimia 175 ya makadirio ya TZS 11.0 bilioni. Mapato haya yanajumuisha TZS 7.8 bilioni zilizopokelewa kama ni Gawio la BOT. Pia serikali ilipokea mkopo wa muda mrefu kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) wenye thamani ya TZS 10.00 bilioni sawa na asilimia 60 ya makadirio ya TZS 16.60 bilioni.

Mhe. Naibu Spika, Fedha zilizopokelewa kama ni misaada ya kibajeti GBS zilifikia jumla ya TZS 32.6 bilioni sawa na asilimia 108 ya makadirio ya TZS 30.3 bilioni na TZS 205.3 bilioni ni misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya Programu na miradi mbali mbali ya maendeleo, fedha hizi ni sawa na asilimia 60.2 ya makadirio ya TZS 340.96 bilioni (Kiambatisho i).

Mhe. Naibu Spika, Katika kipindi cha mwaka 2011/12, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kama Wizara nyengine za serikali, ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 3.91 bilioni kutoka vyanzo mbali mbali. Mpaka kufikia Juni 30, 2012, Ofisi ilikwishakusanya jumla ya TZS 12.7 bilioni, sawa na asilimia 325 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali ilipanga kutumia TZS 613.08 bilioni, ambapo matumizi halisi yalifikia jumla ya TZS 444.4 bilioni sawa na asilimia 73 ya makadirio. Kati ya matumizi hayo, matumizi ya kazi za kawaida yalifikia jumla ya TZS 233.9 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya TZS 234.2 bilioni na matumizi kwa kazi za Maendeleo yalifikia TZS 210.5 bilioni. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo Serikali ilichangia TZS 34.2 bilioni sawa na asilimia 91 ya makadirio ya TZS 37.9 bilioni na jumla ya TZS 176.3 bilioni zilichangiwa na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya Programu na Miradi ya Maendeleo (Kiambatisho ii).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2011/12, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 174,860.0 milioni zikiwemo TZS 47,020.0 milioni kwa kazi za kawaida, TZS 80,217.0 milioni kwa kazi za maendeleo, ikiwemo TZS 7,240.0 milioni mchango wa Serikali na TZS 72,977.0 milioni ikiwa ni misaada kutoka nje. Mfuko Mkuu wa Serikali ulikadiriwa kutumia TZS 47,620.0 milioni.

Katika utekelezaji wake, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeweza kutumia jumla ya TZS 32,586.03 milioni sawa na asilimia 69.3 kwa kazi za kawaida (Kiambatisho iii) na TZS 40,880.46 milioni kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 51.0 (Kiambatisho iv) ambapo mchango wa Serikali ni TZS 5,718.24 milioni(Kiambatisho v). Matumizi ya TZS 31,391.0 milioni yalifanyika kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 66 ya makadirio ya mwaka 2011/12.

IV UTEKELEZAJI WA MALENGO YA KI-IDARA KWA MWAKA 2011/12 NA MWELEKEO KWA MWAKA 2012/13

A: UKUSANYAJI WA MAPATO, HUDUMA ZA BAJETI NA UHASIBU SEREKALINI

Mhe. Naibu Spika, Jukumu hili linasimamiwa na idara tatu na taasisi tatu kama ifuatavyo:

A 1. IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2011/12 iliendelea na kazi zake za kusimamia mapato na matumizi ya Serikali kwa kushirikiana na Idara ya Bajeti, kusimamia mifumo ya Kihasibu na Ukaguzi na kusimamia Deni la Taifa. Katika utekelezaji wa majukumu hayo, Idara imeweza;

i. Kukamilisha ufungaji wa hesabu za mwaka 2010/11 na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
ii. Kulipa mishahara Serikalini na matumizi mengineo kwa wakati,
iii. Kulipa TZS 7,580.0 milioni mafao ya pencheni na TZS 6,850.0 milioni kiinua mgongo kwa wastaafu 860 hadi kufikia mwezi wa Juni 2012,
iv. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu za Ndani 40,
v. Kusimamia na kuendeleza mfumo wa pamoja wa Usimamizi wa fedha (*Integrated Financial Management System - IFMS*), na
vi. Kusimamia deni la Taifa.

Mhe. Naibu Spika, **kwa** mwaka wa fedha wa 2011/12, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 1,677.5 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 20.0 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Juni 2011/12, Idara imetumia jumla ya TZS 1,551.89 milioni sawa na asilimia 92.5 ya makadirio kwa kazi za kawaida na jumla ya TZS 15.0 milioni sawa asilimia 75 kwa kazi za Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka 2012/13, Idara itaendelea na majukumu yafuatayo:-

i. Kusimamia mapato na kuendelea kuimarisha udhibiti na usimamizi wa matumizi ya Serikali,
ii. Kutoa mafunzo ya Uhasibu na Ukaguzi kwa wafanyakazi wa kada ya uhasibu na ukaguzi wa fedha wapatao 55,
iii. Kufunga hesabu za Serikali za mwaka 2011/12,
iv. Kusimamia na kuuhudumia mfumo wa fedha wa IFMS,
v. Kuchapisha vitabu vya Risiti za Serikali,
vi. Kuzijengea uwezo kamati za ukaguzi,
vii. Kusimamia Deni la Taifa,
viii. Kuratibu vikao vya kila mwezi vya kamati ya ukomo wa matumizi na

ix. Kuhudhuria vikao mbali mbali vya Wataalam kama vile vya Kamati ya Kitaifa ya madeni na kamati ya ukomo vinavyofanyika huko Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu haya, Idara imepangiwa kutumia jumla ya TZS 2,782.58 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 2,527.34 milioni kwa kazi za maendeleo zikiwemo TZS 40.00 milioni kama mchango wa Serikali katika kugharamia Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

IDARA YA BAJETI

Mhe. Naibu Spika, majukumu makuu ya idara hii ni kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, kutayarisha na kusambaza maelekezo yanayohusu mbinu bora za kupanga na kudhibiti matumizi ya rasilimali fedha kwa taasisi mbalimbali za umma. Aidha, idara ina jukumu la kuandaa mikakati na mbinu bora za kibajeti zinazofaa na kuwaelimisha wadau wengine katika sekta ya umma pamoja na kushirikiana na taasisi zinazohusiana na taarifa za watendakazi katika sekta za umma kwa lengo la kudhibiti malipo ya mishahara.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2011/2012, Idara imeweza;

i. Kusimamia, kufuatilia na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti, ambapo kwa kushirikiana na Wizara mbali mbali imeweza kukamilisha matayarisho ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa 2012/2013 kwa wakati,
ii. Kuratibu shughuli za kibajeti kwa kuhakikisha kwamba Wizara na Taasisi zinatekeleza bajeti zao kulingana na mfumo wa *MTEF*,
iii. Kuratibu utayarishaji wa Bajeti zenye kuzingatia Programu Maalum (*PBB*) katika wizara sita za majaribio,
iv. Kuweka alama (*Codes*) vifungu vyote vya matumizi kwa kuzingatia majukumu ya Serikali (*Classification of Functions of the Government-COFOG)*,
v. Kutoa mafunzo kwa Maofisa Bajeti wa wizara sita za majaribio, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Makatibu Wakuu, na Wakurugenzi juu ya Bajeti inayozingatia programu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara ilipangiwa kutumia Shilingi 19,666.57 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 20.00 milioni kwa kazi za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 19,424 milioni ni kwa ajili ya marekebisho ya Mishahara Serikalini na Shilingi 242.57 milioni ni matumizi ya idara. Hadi mwisho wa mwezi wa Juni 2012, Idara ilitumia Shilingi 163.95 milioni sawa na asilimia 67.6 ya makadirio kwa kazi za kawaida. Kwa upande wa maendeleo, Idara ilipanga kuweka '*module'* mpya ya bajeti katika mtandao wa *IFMS* ili kuleta ufanisi zaidi wa utekelezaji wa bajeti. Hata hivyo, Idara haikuweza kutumia Shilingi 20 milioni zilizopangwa ili kwanza kuruhusu uimarishaji unaotarajiwa wa mtandao wa *IFMS* kuhamia katika modeli ya kisasa ya "*Epicor 9*".

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara kupitia jukumu lake mahsusi kwa mwaka huu la kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uhalisia wa bajeti ya Serikali, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mageuzi ya mfumo wa bajeti nchini imepanga mambo yafuatayo:

i. Kuanzisha mfumo mpya wa *PBB* kwa wizara zote kumi zilizobakia,
ii. Kutoa mafunzo kivitendo kwa maofisa bajeti wa wizara hizo,
iii. Kuwapatia Mafunzo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi za Kijamii (*CSO*) juu ya muundo na mfumo huo mpya wa bajeti,
iv. Kuzidisha mashirikiano ya kiutendaji kati ya idara zinazohusiana na uratibu wa shughuli za kibajeti ndani na nje ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo,
v. Kuimarisha uwezo wa watendaji wa Idara hasa katika maeneo ya uandaaji na uchambuzi wa taarifa na vitendea kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013, Idara inaombewa jumla ya Shilingi 5,553.838 milioni kwa kazi za kawaida zikiwemo Shilingi 5,010 milioni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara serikalini. Marekebisho hayo ni kutokana na utekelezaji wa muundo wa utumishi, nyongeza za mwaka na ajira za lazima, kama zinavyoonyeshwa katika kifungu 211122 katika kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali cha mwaka 2012/13. Kwa kazi za maendeleo, idara itatekeleza mradi mmoja wa Uimarishaji wa Mchakato wa Bajeti ya Serikali. Mradi huu uliotengewa jumla ya Shilingi 390.1 milioni. Kupitia Idara hii Taasisi za Wizara zinazopatiwa ruzuku zimetengewa Shilingi 16,891.0 milioni.

UKUSANYAJI WA MAPATO NA RASILIMALI NYENGINE

Mhe. Naibu Spika, jukumu la ukusanyaji wa mapato linasimamiwa na Taasisi mbili na Idara moja kama ifuatavyo:

BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ndio wakala Mkuu wa Serikali katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya Muungano yanayotokana na vianzio vya ndani vya kodi. ZRB pia ina jukumu la kuishauri Serikali kuhusiana na Sera za Kodi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, *ZRB*:

i. Ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 119,800 milioni kutoka vianzio vyake mbalimbali.
ii. Kutengeneza Mfumo wa Usimamizi wa Ukusanyaji Kodi ambao umerahisisha mfumo mzima wa usimamizi wa ukusanyaji kodi.
iii. Kuandaa na kutoa taarifa ya utafiti kuhusu kiwango cha chini cha kusajiliwa mlipa kodi wa *VAT*.
iv. Kukamilisha na kuhamia jengo lake jipya la Makao Makuu hapo Mazizini.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2012, *ZRB* imeweza kutekeleza yafuatayo:

i. Imekusanya Shilingi 120,500 milioni sawa na asilimia 100.6 ya makadiro ya mwaka.
ii. Imetengeneza mfumo wa usimamizi wa ukusanyaji kodi Kodi ambao umerahisisha mfumo mzima wa usimamizi wa ukusanyaji kodi.
iii. Imeandaa na kutoa taarifa ya utafiti kuhusu kiwango cha chini cha kusajiliwa mlipa kodi wa *VAT*
iv. Imekamilisha na kuhamia katika jengo lake jipya la Makao Makuu liliopo Mazizini.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013 Bodi ya Mapato imepangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 162,000.0 milioni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 35 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka 2011/2012. Ili kufikia lengo hili mikakati ifuatayo inatarajiwa kutekelezwa ikiwemo ya:

i. Kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote wanasajiliwa na wanalipa kodi ipasavyo;
ii. Walipa kodi wote wanapofanya mauzo katika maeneo ya biashara wanatoa Ankara za kodi kwani hivi sasa walipa kodi hawatoi stakabadhi wanapofanya mauzo;
iii. Kuongeza ukusanyaji wa mapato yatokanayo na sekta ya utalii kwani hivi sasa kuna baadhi ya hoteli ambazo ziko kwenye kiwango cha juu duniani (nyota ya 4 na 5) hutumia viwango vidogo sana kulipa kodi ikilinganishwa na hoteli nyengine zenye ukubwa na sifa zinazofanana.

Aidha, Bodi inakusudia kuendelea kulisimamia kikamilifu suala la magendo ya mafuta hadi kuhakikisha kuwa suala la magendo ya mafuta linatoweka hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, ili kukamilisha malengo haya, Bodi ya Mapato inaombewa ruzuku ya Shilingi 7,500.0 milioni kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (*TRA*)

Mhe. Naibu Spika, Jukumu kubwa la *TRA* ni kukusanya mapato yatokanayo na vianzio vya ushuru wa forodha, ushuru wa bidhaa, kodi ya mapato na kodi nyengine zinazotokana na biashara ya kimataifa kama kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) na Ushuru wa Biashara (*Trade levy*).

Katika mwaka 2011/2012, *TRA* ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 100,580.0 milioni zikiwemo Shilingi 18,000.0 milioni kutokana na kodi ya mapato kwa wafanyakazi wa Taasisi za Muungano wanaofanya kazi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Mpaka kufikia tarehe 30 Juni *TRA* iliweza kukusanya jumla ya Shilingi 91,170.0 milioni sawa na asilimia 91 ya lengo.Kiwango hicho cha makusanyo kinaashiria ukuaji wa mapato wa asilimia 20 ikilinganishwa na mapato halisi ya Shilingi 76,360.0 milioni yaliyokusanywa mwaka 2010/11. Mapato haya hayahusishi Kodi ya

Mapato ya Wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar kwa sababu ambazo nimeshazieleza katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, *TRA* Zanzibar imepangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 106,700.0 milioni kwa mgawanyo wa Idara ya Forodha kukusanya Shilingi 67,080.0 milioni na Idara ya Kodi za Ndani Shilingi 39,650.0 milioni.

IDARA YA FEDHA ZA NJE

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Fedha za Nje ina jukumu la kutafuta, kusimamia, kuratibu na kutathmini misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa MKUZA II na Malengo ya Milenia. Kwa mwaka wa fedha 2011/12, idara:

i. Ilitarajiwa kuratibu na kusimamia upatikanaji wa jumla ya Shilingi 371,200.0 milioni za misaada (ruzuku na mikopo). Fedha hizo zinajumuisha Shilingi 30,280.0 milioni za Misaada ya kibajeti (*GBS*) na Shilingi 340,960.0 milioni kwa ajili ya Programu mbali mbali na Miradi ya Maendeleo. Aidha, kati ya Shilingi 340,960.0 milioni, Shilingi 124,960.0 milioni ni ruzuku na Shilingi 216,000.0 milioni ni mikopo. Idara imeweza kukusanya jumla ya Shilingi 237,910.0 milioni sawa na asilimia 64.09 ya makadirio kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Mashirika ya Kimataifa. Kati ya Fedha hizo, Shilingi 32,570.0 milioni ni misaada ya kibajeti sawa na asilimia 107.6 ya makadirio. Kwa upande wa programu na miradi ya maendeleo idara imeratibu upatikanaji wa Shilingi 205,330.0 milioni kati ya hizo Shilingi 94,810.0 milioni ni ruzuku sawa na asilimia 75.9 za makadirio na Shilingi 110,520.0 milioni ni Mikopo sawa na asilimia 51.2 za makadirio.
ii. Imeendeleza juhudi za kuimarisha mahusiano mazuri na washirika wa maendeleo.
iii. Kupitia vikao vya uratibu wa misaada vya kila mwezi imeweza kufuatilia fedha ili kuhakikisha upatikanaji wake kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 109.57 milioni kwa kazi za kawaida na imeweza kutumia jumla ya Shilingi 108.85 milioni sawa na asilimia 99.3 ya makadirio kwa kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Idara inatarajiwa kutekeleza yafuatayo:
i. Kufuatilia, kusimamia na kuratibu upatikanaji wa Shilingi 293,200.0 milioni ambapo Shilingi 105,400.0 milioni ni ruzuku, Shilingi 187,800.0 milioni ni mikopo na Shilingi 38,100.0 milioni Misaada ya kibajeti (*GBS*),
ii. Kuendeleza mahusiano mazuri na Washirika wa Maendeleo,
iii. Kufuatilia fedha ili ziweze kupatikana kwa wakati pamoja na kuhakikisha kuwa matumizi yanaendana na malengo yaliyokusudiwa,
iv. Kutayarisha Ripoti ya mwaka ya misaada, na
v. Kujenga uwezo kwa wafanyakazi wa kukusanya na kuzifanyia uchambuzi taarifa za misaada.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara inaombewa jumla ya Shilingi 206.688 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 1,382.0 milioni kwa kutekeleza miradi miwili ya maendeleo ambayo ni Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora awamu ya pili na Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Misaada Zanzibar.

MFUKO WA BARABARA

Mhe. Naibu Spika, Mfuko wa Barabara unaendelea na majukumu yake ya uratibu wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Katika mwaka wa fedha wa 2011/12, Mfuko wa Barabara ulitarajia kupokea jumla ya Shilingi 6,432.0 milioni. Kati ya fedha hizo Shilingi 5,463.0 milioni ni kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara na Shilingi 969.0 milioni zilitengwa kwa ajili ya kazi za uendeshaji.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 jumla ya Shilingi 5,569.0 milioni zimekusanywa. Matumizi halisi yaliyofanywa ni Shilingi 4,230.0 milioni**,** ambapo kati ya hizo Shilingi 3,327.0 milioni ni kwa kazi za matengenezo ya barabara. Aidha kazi zenye thamani ya Shilingi 701.0 millioni bado zinaendelea na malipo yake

yatafanywa mara zitakapokamilika. Vile vile Shilingi 903.0 milioni zimelipwa kwa ajili ya uendeshaji wa Mfuko zikijumuisha malipo ya mwisho kwa ujenzi wa ofisi ya Mfuko.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Mfuko umeweza kutekeleza yafuatayo;

i. Kusimamia ukamilishaji wa mradi maalumu wa utafiti wa hali ya barabara *"Roads Maintanance Management Systems" (RMMS)*. Mradi huo umeshakamilika na uko tayari kwa kutumika;
ii. Kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi ya Mfuko hapo Kikwajuni,
iii. Kukamilisha ripoti za ukaguzi wa fedha na ule wa kazi ili kuona thamani ya kazi inalingana na fedha iliyotolewa,
iv. Kuandaa ripoti ya mwaka 2010/11 ya utendaji wa Mfuko,
v. Kuwapatia mafunzo watendaji wanne wa Mfuko na wafanyakazi watatu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano,
vi. Kuhudhuria mikutano ya Jumuiya ya Afrika ya Mifuko ya Barabara (ARMFA), na
vii. Kutoa mafunzo ya utunzaji wa barabara kwa wafanyakazi watano wa Mfuko, wajumbe watatu wa Bodi, wataalamu ishirini na nne kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na wadau mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/13, Mfuko wa Barabara unaombewa ruzuku ya Shilingi 6,320.0 milioni kwa matengenezo ya barabara na uendeshaji wa Mfuko.

URATIBU WA MIPANGO, UCHUMI NA MAENDELEO YA SEKTA

Mhe. Naibu Spika, jukumu hili la Uratibu wa Mipango, Uchumi na Maendeleo ya Sekta linasimamiwa na Idara tatu na taasisi moja.

IDARA YA MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI

Mhe. Naibu Spika, idara hii ina jukumu la kuratibu, kufuatilia na kutathmini mipango ya kitaifa, programu na miradi ya maendeleo pamoja na mapitio ya sekta mbali mbali kwa kushirikiana na sekta husika.

Mhe. Naibu Spika, mpaka kufikia mwezi Juni 2012, idara imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kukamilisha mapitio ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020 na kutayarisha muelekeo wa Dira hiyo kwa kipindi kilichobakia,
ii. Kukamilisha utayarishaji wa Sheria mpya ya Tume ya Mipango Namba 3 ya mwaka 2012,
iii. Kukamilisha mapitio na matayarisho ya Mpango Mkuu wa Ufuatiliaji na Tathmini wa MKUZA II,
iv. Kuandaa na kuchapisha Mapitio ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo (2011/2012) ambao unaonesha utekelezaji wa sekta na program/miradi yote ya maendeleo na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/13,
v. Kutayarisha Mpango wa Miaka Mitano wa Utekelezaji wa MKUZA II ambao umeainisha vipaumbele vya kiuchumi, kijamii na kiutawala vitakavyotekelezwa kwa kipindi chote cha utekelezaji wa MKUZA II,
vi. Kusimamia Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) zikiwemo kazi za urasimishaji ardhi na utambuzi wa wafanyabiashara wadogo wadogo,
vii. Kusimamia sehemu ya malipo ya fidia yaliyofanyika kwa barabara ya Mzambarau Takau-Pandani na Finya zinazofadhiliwa na programu ya Changamoto za Milenia – Tanzania – (*MCA-T*),
viii. Kuratibu Mpango wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA) ambapo vikao viwili vya Kamati ya Ufundi vimefanyika.
ix. Kuratibu Programu ya *UNDAP* inayojumuisha miradi yote inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa kwa kuwapatia fedha katika sekta ya afya, elimu, maji, mabadiliko ya tabia ya nchi, mageuzi ya sheria, UKIMWI, maafa, jinsia na maeneo mengine ya mtambuka.
x. Kusimamia mafunzo ya uchambuzi wa masuala ya mipango na miradi ya kitaifa katika kuandaa mipango ya kazi ya kiwizara, utayarishaji wa bajeti, utekelezaji, taratibu za mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya maendeleo.
xi. Kuwapatia mafunzo maafisa wanne katika masuala ya ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kitengo cha ufuatiliaji na tathmini.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2011/2012, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 262.97 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 23,651.39 milioni kwa programu tatu za MKUMBITA, *UNDAP* na *MCC* na miradi miwili ya maendeleo ambayo ni Kuimarisha Jitihada za Kupunguza Umasikini na Kuifanyia Mabadiliko na Kuimarisha Tume ya Mipango. Mpaka kufikia mwezi Juni 2012, Idara ilitumia jumla ya Shilingi 122.12 milioni sawa na asilimia 46.4 ya makadirio kwa kazi za kawaida na Shilingi 5,211.89 milioni sawa na asilimia 22.0 ya makadirio kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara imekusudia kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kutayarisha na kuchapisha vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo (2012/13) na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo (2013/14),
ii. Kuratibu utekelezaji wa mipango ya kitaifa, program na miradi ya maendeleo,
iii. Kufanya mapitio ya sekta (*Sector Review*) za Fedha na Nishati,
iv. Kuoanisha viashiria vya sekta na viashiria vya MKUZA II,
v. Kutayarisha na kuchapisha ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa MKUZA II (MKUZA AIR 2011/2012),
vi. Kutayarisha Mpango Mkakati wa utekelezaji na kuandaa kanuni za Sheria ya Tume ya Mipango,
vii. Kuandaa maadhimisho ya wiki ya kupunguza umasikini (*Poverty week*), na
viii. Kutoa mafunzo ya muda mfupi juu ya kuandaa dhana, mapendekezo ya mradi na uchambuzi wa sera (*Concept note, Project Proposal & Policy analysis*).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013, Idara inaombewa jumla ya Shilingi 397.35 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 2,318.2 milioni kwa programu tatu na miradi minne ya maendeleo.

IDARA YA UKUZAJI UCHUMI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ukuzaji Uchumi ina jukumu la kufuatilia na kutathmini mwenendo wa uchumi wa Zanzibar kwa lengo la kuhakikisha utulivu wa uchumi mpana na wenye kuhimili ushindani wa kimataifa na unaozingatia maskini na kuimarisha ustawi wa hali za wananchi.

Mhe. Naibu Spika, idara kwa mwaka 2011/12 imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Kukamilisha maandalizi ya Modeli ya Uchumi (MacMod) ambayo itasaidia kukadiria kwa ufanisi zaidi mwenendo wa uchumi na viashiria vyake kwa kila mwaka,
ii. Kutoa wataalamu wa kiuchumi ambao wameendelea kushiriki katika vikao vya matayarisho na majadiliano ya kikanda,
iii. Kuchambua na kutoa taarifa ya Pato la Taifa kwa kila robo mwaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (*OCGS*),
iv. Kukamilisha Modeli ya Kodi (*Tax Modeli*) ambayo itasaida katika kufanya makadirio ya kiataalamu na viashiria yake,
v. Kuratibu mapendekezo ya marekebisho ya kodi kupitia kitengo cha sera za kodi na kutoa ushauri juu ya mwenendo wa kodi,
vi. Kuchambua na kutoa taarifa za hali ya mfumko wa bei na mwenendo wake na kutoa mapendekezo ya hatua kadhaa za kuthibiti hali hiyo,
vii. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi wake kwa lengo la kuijengea uwezo Idara,
viii. Kuandaa tafiti mbali mbali za kiuchumi zitakazosaidia kukabili changamoto zetu za maendeleo, na
ix. Kufanya mapitio ya Takwimu za Fedha (*GFS*) ambazo zinapelekea kufanya uwiano mzuri wa kiuchumi baina ya nchi yetu na nchi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2011/12, idara ilipangiwa kutumia Shilingi 175.82 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Juni 2011/12, Idara ilitumia Shilingi 154.08 milioni sawa na asilimia 87.6 ya makadirio kwa kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika Kwa mwaka 2012/13 idara ya Ukuzaji Uchumi inakusudia kutekeleza yafuatayo:

i. Kutoa taarifa ya Pato la Taifa kwa kila robo mwaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (*OCGS*) na Benki Kuu,
ii. Kuchambua na kutoa taarifa za hali ya mfumko wa bei na mwenendo wake na kutoa mapendekezo,

iii. Kuandaa tafiti za kiuchumi zitakazosaidia kukabili changamoto mbali mbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii,
iv. Kuimarisha kitengo cha Takwimu za Kifedha za Serikali (*GFS*) kwa lengo la kukiwezesha kufanya uchambuzi muwafaka wa takwimu hizo ili zisaidie katika kufanya maamuzi ya kiuchumi na kifedha,
v. Kuupitia na kuufanyia marekebisho mfumo mpya wa utoaji wa taarifa za bei za bidhaa,
vi. Kuzifanyia mapitio Modeli za Uchumi na Mapato kwa kuziwekea takwimu sahihi zitakazosaidia kutoa utabiri muwafaka wa kiuchumi,
vii. Kuandaa kongamano la kiuchumi kwa lengo la kupata mawazo juu ya uimarishaji uchumi kutoka kwa wadau wa taasisi na asasi mbali mbali,
viii. Kuratibu mapendekezo ya marekebisho ya kodi kupitia kitengo cha sera za kodi na kutoa ushauri juu ya mwenendo wake,
ix. Kupata taaluma ya mfumo wa programu ya kifedha (*financial programming*) ambao hutumika kufanya utabiri na udhibiti wa uchumi wa kila robo mwaka pamoja na kuangalia uwezekano wa kuutumia kwa uchumi wetu,
x. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi wa Idara juu ya fani mbali mbali za kiuchumi, na
xi. Kuandaa Sera, Sheria na Mkakati wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/13, idara ilipangiwa kutumia shilingi 175.82 milioni kwa kazi za kawaida, hadi kufikia Juni, 2011/2012 idara ilitumia Shilingi 154.08 milioni sawa na asilimia 87.6 ya makadirio kwa kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013, Idara ya Ukuzaji Uchumi inakusudia kutekeleza mambo yafuatayo:
i. Kutoa taarifa ya pato la taifa kwa kila robo mwaka kwa kushirikiaa na ofisi y Mtakwimu mkuuserikali na Benki Kuu.
ii. Kuchambua na kutoa taarifa za hali ya mfumko wa bei na mwenendo wake na kutoa mapendekezo.
iii. Kuandaa tafiti za kiuchumi zitakazosaidia kukabili cangamoto mbali mbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.
iv. Kuimarisha kitengo cha takwimu za kifedha za serikali kwa lengo la kukiwezesha kufanya uchambuzi muwafaka wa takwimu hizo ili zisaidie katika kufanya maamuzi ya kiuchumi na kifedha.
v. Kuupitia na kuufanyia marekebisho mfumo mpya wa utoaji wa taarifa za bei za bidhaa.
vi. Kuzifanyia mapitio modeli za uchumi na mapato kwa kuziwekea takwimu sahihi zitakazosaidia kutoa utabiri muwafaka wa kiuchumi.
vii. Kuandaa kongamano la kiuchumi kwa lengo la kupata mawazo juu ya uimarishaji uchumi kutoka kwa wadau wa taasisi na asasi mbali mbali.
viii Kuratibu mapendekezo ya marekebisho ya kodi kupitia kitengo cha sera za kodi na kutoa ushauri juu ya mwenendo wake.
ix Kupata taaluma ya mfumo wa programu za kifedha ambao hutumika kufanya utabiri na udhibiti wa uchumi kwa kila robo mwaka pamoja na kuangalia uwezekano wa kuutumia kwa uchumi wetu.
x Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi wa idara juu ya fani mbali mbali za kiuchumi na
xi Kuandaa sera, sheria na mkakati wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013 Idara ya Ukuzaji Uchumi imeombewa kutumia jumla ya shilingi 335.58 millioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 150.00 milioni kwa Mradi wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

IDARA YA MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi ina jukumu la kusimamia uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Watendakazi Kitaifa, uratibu wa mipango ya idadi ya watu pamoja na uratibu wa programu ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara imetekeleza yafuatayo:
i. Kufanya Utafiti wa Mazingira ya Ustaafu Zanzibar ambapo rasimu ya ripoti ya utafiti huo imewasilishwa kwa wadau Unguja na Pemba na itafikishwa Serikalini kwa hatua za utekelezaji,

ii. Kuendelea na mchakato wa matayarisho ya utafiti wa hali ya utumishi na kuandaa tathmini juu ya hali ya mahitaji ya wataalamu nchini iliyoiwezesha Serikali kutambua vipaumbele katika mahitaji ya wataalamu na mafunzo,
iii. Kuwapatia mafunzo maafisa mipango juu ya uingizaji viashiria vya idadi ya watu katika mipango na bajeti,
iv. Kutayarisha ripoti ya mwanzo ya mwaka 2011 juu ya masuala ya idadi ya watu nchini yenye kubeba ujumbe wa athari za kasi ya idadi ya watu katika maendeleo;
v. Kushiriki katika maadhimisho ya siku ya idadi ya watu Duniani ambayo kwa mwaka 2011 yalifanyika Mkoani Tanga;
vi. Kukamilisha mapitio ya mkakati wa utekelezaji wa sera ya idadi ya watu kwa mwaka 2011 na kuwasilisha kwa wadau Unguja na Pemba, pamoja na kuzindua rasmi Baraza la idadi ya watu na Maendeleo Zanzibar mwezi Mei 2012 ikiwa ni chombo cha juu cha kusimamia utekelezaji sera ya idadi ya watu;

Mhe. Naibu Spika, kwa programu ya Uhai, Hifadhi, Maendeleo ya Mama na Mtoto, Idara imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Kufanya tathmini juu ya utekelezaji wa program hiyo katika ngazi ya Shehia, Wilaya na Taifa.
ii. Kushirikiana na *UNICEF* imewasilisha ripoti ya hali halisi ya wanawake na watoto Zanzibar kwa wadau wa sekta mbali mbali, na
iii. Kuandaa muongozo maalum utakaosaidia katika Uingizaji masuala ya watoto katika bajeti zetu kwa kushirikiana na *UNICEF* na wadau wa sekta mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2011/12, idara ilipangiwa kutumia Shilingi 136.24 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 130.00 millioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Juni 2012, idara imetumia jumla ya Shilingi 87.84 milioni sawa na asilimia 64.5 ya makadirio kwa kazi za kawaida na Shilingi 127.44 milioni sawa na asilimia 98.0 ya makadirio kwa kazi za maendeleo kupitia mradi wa Uhai, Hifadhi, Maendeleo ya Mama na Mtoto, Mradi wa Utafiti wa Watenda kazi, na Mradi wa Kuoanisha masuala ya Idadi ya Watu katika afya ya uzazi, Jinsia na Kupunguza Umasikini.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/13, idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi inakusudia kufanya yafuatayo:

i. Kuendelea na zoezi la utafiti wa hali ya utumishi kwa moduli tatu za msingi,
ii. Kuandaa tafiti ndogo ndogo zinazohusiana na masuala ya rasilimali watu,
iii. Kuratibu mipango ya idadi ya watu kwa kuandaa ripoti ya mwaka 2012 juu ya masuala ya idadi ya watu,
iv. Kuandaa mikutano ya kila robo mwaka, na
v. Kutoa mafunzo juu ya uingizaji viashiria vya idadi ya watu katika mipango na bajeti awamu ya pili kwa wadau mbali mbali na kushiriki katika maadhimisho ya siku ya idadi ya watu Duniani kwa mwaka 2013.

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na *UNICEF*, Idara itaendelea:

i. Kuratibu program ya pamoja ya Kuimarisha Hifadhi ya Mtoto kwa kufanya tathmini ya utekelezaji program katika ngazi mbali mbali, na
ii. Kuratibu utekelezaji wa uingizaji masuala ya watoto katika bajeti za sekta kwa kutumia muongozo uliotayarishwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Idara kwa mwaka 2012/13 imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 188.47 millioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 1,437.73 millioni kwa kazi za maendeleo.

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, jukumu la Taasisi hii ni kukusanya, kuchambua na kutoa takwimu za kitaifa kwa watumiaji mbali mbali hapa nchini na kimataifa. Katika mwaka wa fedha 2011/12, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Kufanya utafiti wa hali ya Uchumi kwa mwaka 2011 na kutoa takwimu za ukuaji wa pato la Taifa na viashiria vyengine vya kiuchumi na kijamii kwa wakati uliotakiwa,

ii. Kufanya utafiti wa Hali ya Demografia, Afya ya Mama na Mtoto, Hali ya Uwekezaji nchini, tafiti nyengine katika sekta za kiuchumi kama vile usafirishaji, utalii n.k.
iii. Kukamilisha uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa katika tafiti zilizofanywa na kuwasilisha matokeo yake kwa wadau, miongoni mwa takwimu zilizowasilishwa ni zile za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya, Ufafiti wa Hali ya Demografia, Afya ya Mama na Mtoto;
iv. Kuendelea na matayarisho ya Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012 kwa kufanya sensa ya majaribio, kukamilisha kazi za utengaji wa maeneo ya kuhesabia na kukamilisha utayarishaji wa nyenzo zote zinazohitajika katika utekelezaji wa kazi hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa, na
v. Kuwapatia maafisa kumi mafunzo katika ngazi mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imekuwa ikiendeleza kazi za miradi ya uimarishaji wa mfumo wa takwimu Zanzibar kwa kutekeleza kazi za mradi wa *ZANSTAT* na mradi wa *Tanzania Statistical Master Plan (TSMP)* ambapo miongozo ya kuendesha kazi za kitakwimu imetayarishwa, maafisa takwimu kutoka Idara na Taasisi mbalimbali wamepatiwa mafunzo ya kitakwimu, na vifaa vya kompyuta na usafiri.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2011/2012 jumla ya Shilingi 1,510.00 milioni zilipangwa kutekeleza majukumu haya, ambapo Shilingi 860.0 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 650.0 milioni kwa kazi za maendeleo ambazo ni mchango wa Serikali. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2012, jumla ya Shilingi 1,469.0 milioni zilitolewa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Ofisi hii imepanga :
i. Kufanya utafiti wa hali ya Uchumi kwa mwaka 2012 na kutoa takwimu za hali ya Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2012 ikiwa ni pamoja na kutoa takwimu za pato la Taifa kwa kila robo mwaka,
ii. Kuendelea na kazi za tafiti na sensa mbalimbali zilizoainishwa katika Mpango Tafiti na Sensa,
iii. Kufanya sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012 ifikapo tarehe 26 Agosti 2012 na kutoa matokeo ya awali ifikapo tarehe 31 Disemba 2012,
iv. Kuwapatia mafunzo maafisa wake katika fani za takwimu, Teknohama, na nyenginezo, ndani na nje ya nchi,
v. Kuimarisha elimu na mawasiliano na wadau ili takwimu zinazozalishwa ziweze kutumika ipasavyo na ziwafikie wadau mbalimbali,
vi. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya uimarishaji takwimu ya *TSMP* na kukamilisha mradi wa *ZANSTAT* kwa awamu ya mwanzo na kuanza mchakato wa matayarisho ya awamu ya pili.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi inatarajia kutumia jumla ya Shilingi 4,230.00 milioni ambapo kati ya fedha hizo Shilingi 1,330.0 milioni zitatumika kwa kazi za kawaida na Shilingi 500.00 millioni ni mchango wa Serikali katika kugharamia Mradi wa Uimarishaji Takwimu. Bakaa ya Shilingi 2,400.0 milioni itachangiwa na Washirika wa Maendeleo ambapo Shilingi 400.00 milioni ni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa *ZANSTAT* na Shilingi 2,000.00 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa *TSMP* kwa upande wa Zanzibar.

USIMAMIZI WA MALI ZA SERIKALI NA MITAJI

Mhe. Naibu Spika, jukumu la usimamizi wa mali za Serikali na mitaji linasimamiwa na Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (ZIPA).

IDARA YA UHAKIKIMALI NA MITAJI YA UMMA

Mhe. Naibu Spika**,** Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma ina jukumu la kusimamia Mali za Serikali ikihusisha ununuzi, utunzaji na uondoaji wake. Mali hizo ni pamoja na majengo, vifaa, mitambo, mashamba na zana mbali mbali. Kwa upande mwengine, idara pia ina jukumu la kusimamia mitaji, hisa na uwekezaji wa rasilimali katika mashirika na kampuni za umma na binafsi.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2011/12 idara imefanya yafuatayo:
i. Kukamilisha utiaji thamani kwa mali za kudumu zilizo chini ya Wizara ya Afya, Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Elimu na Mafunzo ya Amali, Miundombinu na Mawasiliano, (OR) Fedha,

Uchumi na Mipango ya Maendeleo ili kukamilisha uandaaji wa daftari la mali za kudumu za Serikali (Fixed Asset Register).

ii. Imeendelea na zoezi la kuzifanyia uchambuzi wa hesabu kwa Mashirika ya Serikali. Taswira inayojitokeza ni kuwa Mashirika yaliyo mengi yanashindwa kujiendesha kibiashara, yapo katika hali mbaya kifedha na yanashindwa kulipa gawio kama Sheria ya Mitaji ya Umma inavyoelekeza.

iii. Kufanya ukaguzi wa manunuzi katika Wizara zote 16 na Taasisi zake. Kazi iliyopo sasa ni kuandaa ripoti ya mwaka ya manunuzi.

iv. Kupitia semina za mafunzo, idara ilijenga uwezo wa taasisi na wadau mbalimbali kuhusiana na sheria ya manunuzi na uondoshwaji wa mali za Serikali Unguja na Pemba.

v. Kuanzisha daftari la kuorodhesha makampuni yanayoweza kutoa huduma katika taasisi za serikali kama inavyolezwa na Sheria. Tayari kampuni 100 zimeshajiandikisha kwa ajili ya kazi ya kutoa huduma Serikalini.

vi. Kuratibu program ya ujenzi wa Ofisi za Serikali Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 197.60 milioni na imeweza kutumia 174.47 milioni sawa na asilimia 88.3 ya makadirio kwa kazi za kawaida. Kwa upande wa kazi za maendeleo idara ilipangiwa kutumia TZS 5,628 milioni na imeweza kutumia TZS 4,568.35 milioni sawa na asilimia 81.2 ya makadirio kwa Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali pamoja na Mradi wa Kutathmini Mali za Serikali na program ya kuimarisha utawala bora awamu ya pili.

Mhe. Naibu Spika**,** kazi kuu za Idara kwa mwaka 2012/2013 ni zifuatazo;

i. Kuendelea na daftari la kumbukumbu la mali za Serikali pamoja na kufanya tathmini ya mali katika Wizara za Katiba na Sheria, Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto,

ii. Kuendeleza usimamizi wa mitaji na hisa za Serikali;

iii. Kuwajengea uwezo watendaji katika masuala ya manunuzi na uondoshaji wa Mali za Serikali;

iv. Kufanya ukaguzi wa manunuzi pamoja na uhakiki wa Mali za serikali katika Wizara na taasisi zote za Serikali;

v. Kuwapatia mafunzo wahakiki (Stock Verifiers) ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa taaluma zaidi pamoja na kuendelea kusimamia na kufanya tathmini katika Mashirika yote ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara imepangiwa kutumia jumla ya TZS 359.012 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 6,000.0 milioni kwa kazi za maendeleo ikiwemo TZS 5,800.0 milioni kwa Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali na TZS 200.0 milioni kwa mradi wa kufanyia tathmini mali za Serikali.

MAMLAKA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (ZIPA)

Mhe. Naibu Spika**, j**ukumu kubwa la Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) ni kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini. Kwa mwaka 2011/2012 Mamlaka iliweza kutekeleza yafuatayo:

i. Kuidhinisha jumla ya miradi 24 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 139.38 milioni,

ii. Kutangaza fursa mbali mbali za uwekezaji kwa kufanya ziara za uenezi, Kushiriki katika mikutano ya kanda na ya kimataifa ya uhamasishaji, kutangaza kweye makala ya magazeti kama vile SADC

directory na Tanzania Review, Kuchapisha 'diary' na kalenda. Tayari tovuti ya *www.zanzibarinvest.org* imetafsiriwa kwa lugha ya kichina, muelekeo pia ni kuwa na ukurasa na tovuti kwa lugha ya kituruki na kirusi.

iii. Kufanya ziara katika nchi zenye viwanda vya usindikaji samaki (Sychelles na Maldives) ili kujifunza na kushajihisha wenye viwanda kuja Zanzibar.

iv. Kuwaendeleza wafanyakazi wanane katika mafunzo ya muda mrefu kwenye fani mbali mbali kwa kiwango cha shahada ya pili, shahada ya kwanza, diploma na cheti.

v. Kufanya matengenezo ya maghala kwa njia ya kushirikiana na wawekezaji, pamoja na matengenezo ya barabara inayoingia eneo la Bandari Huru kwa kiwango cha lami sehemu ya nje na kiwango cha kifusi sehemu ya kuegeshea magari.

vi. Kuufanyia mapitio Mpango wa Matumizi ya Eneo Huru la Uchumi la Fumba uliofanywa hapo kabla ili kupendekeza matumizi mchanganyiko ya eneo hilo kwa manufaa zaidi.

vii. Kuifanyia mapitio Sheria ya Mamlaka ya Vitega Uchumi.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2012/2013, Mamlaka itafanya kazi zifuatazo:

i. Kuendelea kushajiisha wawekezaji wa ndani kuwekeza katika sekta za uchumi hasa uvuvi na viwanda,

ii. Kuendelea kuwavutia wawekezaji wa nje kuja kuendeleza juhudi za Serikali katika kuinua uchumi wa nchi na kupunguza umasikini,

iii. Kuwaendeleza wafanyakazi kielimu pamoja na kuwajengea uwezo katika kupitisha miradi na sekta nyengine mbalimbali za Mamlaka,

iv. Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Ukuzaji Vitega Uchumi,

v. Kuendelea na tafiti za kuangalia mwenendo wa mitaji binafsi (PCF) na kuangalia fursa mpya za uwekezaji kwa lengo la kusaidia wawekezaji wa kati na wadogo wadogo wa ndani kuweza kuwekeza na kuendelezwa,

vi. Kusimamia ushirikishwaji wa wananchi katika uendelezaji wa maeneo huru ya uchumi, na

vii. Kuendelea kutayarisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi katika eneo la Fumba, ili kuweza kuvutia miradi ya makaazi na ya viwanda katika Maeneo Huru ya Uchumi.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2012/2013, Mamlaka inaombewa kupatiwa ruzuku ya TZS 300.00 milioni kuendesha kazi zake za kawaida.

C: URATIBU WA MIPANGO, UCHUMI NA MAENDELEO YA SEKTA

Jukumu hili la Uratibu wa Mipango, Uchumi na Maendeleo ya Sekta linasimamiwa na Idara tatu na taasisi moja.

C 1. IDARA YA MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI

Mhe. Naibu Spika**,** Idara hii ina jukumu la kuratibu, kufuatilia na kutathmini mipango ya kitaifa, programu na miradi ya maendeleo pamoja na mapitio ya sekta mbali mbali kwa kushirikiana na sekta husika.

Mhe. Naibu Spika**,** mpaka kufikia mwezi Juni 2012, Idara imetekeleza yafuatayo:

xii. Kukamilisha mapitio ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020 na kutayarisha muelekeo wa Dira hiyo kwa kipindi kilichobakia,

xiii. Kukamilisha utayarishaji wa Sheria mpya ya Tume ya Mipango Namba 3 ya mwaka 2012,

xiv. Kukamilisha mapitio na matayarisho ya Mpango Mkuu wa Ufuatiliaji na Tathmini wa MKUZA II,

xv. Kuandaa na kuchapisha Mapitio ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo (2011/2012) ambao unaonesha utekelezaji wa sekta na program/miradi yote ya maendeleo na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/13,

xvi. Kutayarisha Mpango wa Miaka Mitano wa Utekelezaji wa MKUZA II ambao umeainisha vipaumbele vya kiuchumi, kijamii na kiutawala vitakavyotekelezwa kwa kipindi chote cha utekelezaji wa MKUZA II,

xvii. Kusimamia Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) zikiwemo kazi za urasimishaji ardhi na utambuzi wa wafanyabiashara wadogo wadogo,

xviii. Kusimamia sehemu ya malipo ya fidia yaliyofanyika kwa barabara ya Mzambarau Takau-Pandani na Finya zinazofadhiliwa na program ya Changamoto za Milenia – Tanzania – (MCA-T),

xix. Kuratibu Mpango wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA) ambapo vikao viwili vya Kamati ya Ufundi vimefanyika.

xx. Kuratibu Programu ya UNDAP inayojumuisha miradi yote inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa kwa kuwapatia fedha katika sekta ya afya, elimu, maji, mabadiliko ya tabia ya nchi, mageuzi ya sheria, UKIMWI, maafa, jinsia na maeneo mengine ya mtambuka.

xxi. Kusimamia mafunzo ya uchambuzi wa masuala ya mipango na miradi ya kitaifa katika kuandaa mipango kazi ya kiwizara, utayarishaji wa bajeti, utekelezaji, taratibu za mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya maendeleo.

xxii. Kuwapatia mafunzo maafisa wanne katika masuala ya ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kitengo cha ufuatiliaji na tathmini.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2011/2012, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 262.97 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 23,651.39 milioni kwa programu tatu za MKUMBITA, UNDAP na MCC na miradi miwili ya maendeleo ambayo ni Kuimarisha Jitihada za Kupunguza Umasikini na Kuifanyia Mabadiliko na Kuimarisha Tume ya Mipango. Mpaka kufikia mwezi Juni 2012, Idara ilitumia jumla ya TZS 122.12 milioni sawa na asilimia 46.4 ya makadirio kwa kazi za kawaida na TZS 5,211.89 milioni sawa na asilimia 22.0 ya makadirio kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara imekusudia:

ix. Kutayarisha na kuchapisha vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo (2012/13) na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo (2013/14),

x. Kuratibu utekelezaji wa mipango ya kitaifa, program na miradi ya maendeleo,

xi. Kufanya mapitio ya sekta (Sector Review) za Fedha na Nishati,

xii. Kuoanisha viashiria vya sekta na viashiria vya MKUZA II,

xiii. Kutayarisha na kuchapisha ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa MKUZA II (MKUZA AIR 2011/2012),

xiv. Kutayarisha Mpango Mkakati wa utekelezaji na kuandaa kanuni za Sheria yaTume ya Mipango,

xv. Kuandaa maadhimisho ya wiki ya kupunguza umasikini (Poverty week), na

xvi. Kutoa mafunzo ya muda mfupi juu ya kuandaa dhana, mapendekezo ya mradi na uchambuzi wa sera (Concept note, Project Proposal & Policy analysis).

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2012/2013, Idara inaombewa jumla ya TZS 397.35 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 2,318.2 milioni kwa programu tatu na miradi minne ya maendeleo.

C.2 IDARA YA UKUZAJI UCHUMI

Mhe. Naibu Spika**,** Idara ya Ukuzaji Uchumi ina jukumu la kufuatilia na kutathmini mwenendo wa uchumi wa Zanzibar kwa lengo la kuhakikisha utulivu wa uchumi mpana na wenye kuhimili ushindani wa kimataifa na unaozingatia maskini na kuimarisha ustawi wa hali za wananchi.

Mhe. Naibu Spika**,** Idara kwa mwaka 2011/12 imetekeleza kazi zifuatazo:

x. Kukamilisha maandalizi ya Modeli ya Uchumi (MacMod) ambayo itasaidia kukadiria kwa ufanisi zaidi mwenendo wa uchumi na viashiria vyake kwa kila mwaka,

xi. Kutoa wataalamu wa kiuchumi ambao wameendelea kushiriki katika vikao vya matayarisho na majadiliano ya kikanda,

xii. Kuchambua na kutoa taarifa ya Pato la Taifa kwa kila robo mwaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS),

xiii. Kukamilisha Modeli ya Kodi (Tax Model) ambayo itasaida katika kufanya makadirio ya kiataalamu na viashiria yake,

xiv. Kuratibu mapendekezo ya marekebisho ya kodi kupitia kitengo cha sera za kodi na kutoa ushauri juu ya mwenendo wa kodi,

xv. Kuchambua na kutoa taarifa za hali ya mfumko wa bei na mwenendo wake na kutoa mapendekezo ya hatua kadhaa za kuthibiti hali hiyo,

xvi. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi wake kwa lengo la kuijengea uwezo Idara,

xvii. Kuandaa tafiti mbali mbali za kiuchumi zitakazosaidia kukabili changamoto zetu za maendeleo, na

xviii. Kufanya mapitio ya Takwimu za Fedha (GFS) ambazo zinapelekea kufanya uwiano mzuri wa kiuchumi baina ya nchi yetu na nchi nyengine.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2011/12, idara ilipangiwa kutumia TZS 175.82 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Juni 2011/12, Idara ilitumia TZS 154.08 milioni sawa na asilimia 87.6 ya makadirio kwa kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2012/13 idara ya Ukuzaji Uchumi inakusudia kutekeleza yafuatayo:

xii. Kutoa taarifa ya Pato la Taifa kwa kila robo mwaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) na Benki Kuu,

xiii. Kuchambua na kutoa taarifa za hali ya mfumko wa bei na mwenendo wake na kutoa mapendekezo,

xiv. Kuandaa tafiti za kiuchumi zitakazosaidia kukabili changamoto mbali mbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii,

xv. Kuimarisha kitengo cha Takwimu za Kifedha za Serikali (GFS) kwa lengo la kukiwezesha kufanya uchambuzi muwafaka wa takwimu hizo ili zisaidie katika kufanya maamuzi ya kiuchumi na kifedha,

xvi. Kuupitia na kuufanyia marekebisho mfumo mpya wa utoaji wa taarifa za bei za bidhaa,

xvii. Kuzifanyia mapitio Modeli za Uchumi na Mapato kwa kuziwekea takwimu sahihi zitakazosaidia kutoa utabiri muwafaka wa kiuchumi,

xviii. Kuandaa kongamano la kiuchumi kwa lengo la kupata mawazo juu ya uimarishaji uchumi kutoka kwa wadau wa taasisi na asasi mbali mbali,

xix. Kuratibu mapendekezo ya marekebisho ya kodi kupitia kitengo cha sera za kodi na kutoa ushauri juu ya mwenendo wake,

xx. Kupata taaluma ya mfumo wa programu ya kifedha (financial programming) ambao hutumika kufanya utabiri na udhibiti wa uchumi wa kila robo mwaka pamoja na kuangalia uwezekano wa kuutumia kwa uchumi wetu,

xxi. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi wa Idara juu ya fani mbali mbali za kiuchumi, na

xxii. Kuandaa Sera, Sheria na Mkakati wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2012/13, idara ya Ukuzaji Uchumi inaombewa kutumia jumla ya Tshs 335.58 millioni kwa kazi za kawaida na TZS 150.00 milioni kwa Mradi wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

IDARA YA MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI

Mhe. Naibu Spika**,** Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi ina jukumu la kusimamia uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Watendakazi Kitaifa, uratibu wa mipango ya idadi ya watu pamoja na uratibu wa programu ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto.

Mhe. Naibu Spika**,** katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara imetekeleza yafuatayo:

vii. Kufanya Utafiti wa Mazingira ya Ustaafu Zanzibar ambapo rasimu ya ripoti ya utafiti huo imewasilishwa kwa wadau Unguja na Pemba na itafikishwa Serikalini kwa hatua za utekelezaji,

viii. Kuendelea na mchakato wa matayarisho ya utafiti wa hali ya utumishi na kuandaa tathmini juu ya hali ya mahitaji ya wataalamu nchini iliyoiwezesha Serikali kutambua vipaumbele katika mahitaji ya wataalamu na mafunzo,

ix. Kuwapatia mafunzo maafisa mipango juu ya uingizaji viashiria vya idadi ya watu katika mipango na bajeti,

x. Kutayarisha ripoti ya mwanzo ya mwaka 2011 juu ya masuala ya idadi ya watu nchini yenye kubeba ujumbe wa athari za kasi ya idadi ya watu katika maendeleo;

xi. Kushiriki katika maadhimisho ya siku ya idadi ya watu Duniani ambayo kwa mwaka 2011 yalifanyika Mkoani Tanga;

xii. Kukamilisha mapitio ya mkakati wa utekelezaji wa sera ya idadi ya watu kwa mwaka 2011 na kuwasilisha kwa wadau Unguja na Pemba, pamoja na kuzindua rasmi Baraza la idadi ya watu na Maendeleo Zanzibar mwezi Mei 2012 ikiwa ni chombo cha juu cha kusimamia utekelezaji sera ya idadi ya watu;

Mhe. Naibu Spika**,** kwa program ya Uhai, Hifadhi, Maendeleo ya Mama na Mtoto, Idara imetekeleza kazi zifuatazo:

iv. Kufanya tathmini juu ya utekelezaji wa program hiyo katika ngazi ya Shehia, Wilaya na Taifa.

v. Kushirikiana na UNICEF imewasilisha ripoti ya hali halisi ya wanawake na watoto Zanzibar kwa wadau wa sekta mbali mbali, na

vi. Kuandaa muongozo maalum utakaosaidia katika Uingizaji masuala ya watoto katika bajeti zetu kwa kushirikiana na UNICEF na wadau wa sekta mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2011/12, idara ilipangiwa kutumia TZS 136.24 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 130.00 millioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Juni 2012, idara imetumia jumla ya TZS 87.84 milioni sawa na asilimia 64.5 ya makadirio kwa kazi za kawaida na TZS 127.44 milioni sawa na asilimia 98.0 ya makadirio kwa kazi za maendeleo kupitia mradi wa Uhai, Hifadhi, Maendeleo ya Mama na Mtoto, Mradi wa Utafiti wa Watenda kazi, na Mradi wa Kuoanisha masuala ya Idadi ya Watu katika afya ya uzazi, Jinsia na Kupunguza Umasikini.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2012/13, idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi inakusudia kufanya yafuatayo:

vi. Kuendelea na zoezi la utafiti wa hali ya utumishi kwa moduli tatu za msingi,

vii. Kuandaa tafiti ndogo ndogo zinazohusiana na masuala ya rasilimali watu,

viii. Kuratibu mipango ya idadi ya watu kwa kuandaa ripoti ya mwaka 2012 juu ya masuala ya idadi ya watu,

ix. Kuandaa mikutano ya kila robo mwaka, na

x. Kutoa mafunzo juu ya uingizaji viashiria vya idadi ya watu katika mipango na bajeti awamu ya pili kwa wadau mbali mbali na kushiriki katika maadhimisho ya siku ya idadi ya watu Duniani kwa mwaka 2013.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa kushirikiana na UNICEF, Idara itaendelea:

iii. Kuratibu program ya pamoja ya Kuimarisha Hifadhi ya Mtoto kwa kufanya tathmini ya utekelezaji program katika ngazi mbali mbali, na

iv. Kuratibu utekelezaji wa uingizaji masuala ya watoto katika bajeti za sekta kwa kutumia muongozo uliotayarishwa.

Mhe. Naibu Spika**,** katika kutekeleza majukumu yake, Idara kwa mwaka 2012/13 imepangiwa kutumia jumla ya TZS 188.47 millioni kwa kazi za kawaida na TZS 1,437.73 millioni kwa kazi za maendeleo.

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika**,** jukumu la Taasisi hii ni kukusanya, kuchambua na kutoa takwimu za kitaifa kwa watumiaji mbali mbali hapa nchini na kimataifa. Katika mwaka wa fedha 2011/12, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

vi. Kufanya utafiti wa hali ya Uchumi kwa mwaka 2011 na kutoa takwimu za ukuaji wa pato la Taifa na viashiria vyengine vya kiuchumi na kijamii kwa wakati uliotakiwa,

vii. Kufanya utafiti wa Hali ya Demografia, Afya ya Mama na Mtoto, Hali ya Uwekezaji nchini, tafiti nyengine katika sekta za kiuchumi kama vile usafirishaji, utalii n.k.

viii. Kukamilisha uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa katika tafiti zilizofanywa na kuwasilisha matokeo yake kwa wadau, miongoni mwa takwimu zilizowasilishwa ni zile za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya, Ufafiti wa Hali ya Demografia, Afya ya Mama na Mtoto;

ix. Kuendelea na matayarisho ya Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012 kwa kufanya sensa ya majaribio, kukamilisha kazi za utengaji wa maeneo ya kuhesabia na kukamilisha utayarishaji wa nyenzo zote zinazohitajika katika utekelezaji wa kazi hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa, na

x. Kuwapatia maafisa kumi mafunzo katika ngazi mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika**,** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imekuwa ikiendeleza kazi za miradi ya uimarishaji wa mfumo wa takwimu Zanzibar kwa kutekeleza kazi za mradi wa ZANSTAT na mradi wa Tanzania Statistical Master Plan (TSMP) ambapo miongozo ya kuendesha kazi za kitakwimu imetayarishwa, maafisa takwimu kutoka Idara na Taasisi mbalimbali wamepatiwa mafunzo ya kitakwimu, na vifaa vya kompyuta na usafiri.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2011/2012 jumla ya TZS 1,510.00 milioni zilipangwa kutekeleza majukumu haya, ambapo TZS 860.0 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 650.0 milioni kwa kazi za maendeleo ambazo ni mchango wa Serikali. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2012, jumla ya TZS 1,469.0 milioni zilitolewa.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Ofisi hii imepanga:

vii. Kufanya utafiti wa hali ya Uchumi kwa mwaka 2012 na kutoa takwimu za hali ya Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2012 ikiwa ni pamoja na kutoa takwimu za pato la Taifa kwa kila robo mwaka,

viii. Kuendelea na kazi za tafiti na sensa mbalimbali zilizoainishwa katika Mpango Tafiti na Sensa,

ix. Kufanya sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012 ifikapo tarehe 26 Agosti 2012 na kutoa matokeo ya awali ifikapo tarehe 31 Disemba 2012,

x. Kuwapatia mafunzo maafisa wake katika fani za takwimu, Teknohama, na nyenginezo, ndani na nje ya nchi,

xi. Kuimarisha elimu na mawasiliano na wadau ili takwimu zinazozalishwa ziweze kutumika ipasavyo na ziwafikie wadau mbalimbali,

xii. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya uimarishaji takwimu ya TSMP na kukamilisha mradi wa ZANSTAT kwa awamu ya mwanzo na kuanza mchakato wa matayarisho ya awamu ya pili.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi inatarajia kutumia jumla ya TZS 4,230.00 milioni ambapo kati ya fedha hizo TZS 1,330.0 milioni zitatumika kwa kazi za kawaida na TZS 500.00 millioni ni mchango wa Serikali katika kugharamia Mradi wa Uimarishaji Takwimu. Bakaa ya TZS 2,400.0 milioni itachangiwa na Washirika wa Maendeleo ambapo TZS 400.00 milioni ni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ZANSTAT na TZS 2,000.00 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa TSMP kwa upande wa Zanzibar

HUDUMA ZA UTAWALA, URATIBU NA FEDHA

Jukumu hili la Huduma za Utawala na Uratibu wa fedha linasimamiwa na Idara nne:

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ndio msimamizi mkuu wa kuimarisha mazingira bora ya kazi, kuendeleza wafanyakazi pamoja na kusimamia huduma za teknolojia ya habari na sheria. Aidha masuala yote ya utawala, utumishi na kuimarisha utoaji wa huduma kwa watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo yako chini ya Idara hii.

Mhe. Naibu Spika**,** Idara kwa mwaka 2011/12 imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuwapatia watendaji 75 mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya Nchi,

ii. Kuwapatia wafanyakazi 21 mafunzo maalumu ya uandishi wa Ripoti na taaluma juu ya namna nzuri ya kufanya majadiliano, na

iii. Kuwapatia udhamini wanafunzi 1,317 katika vyuo mbali mbali nchini Tanzania katika fani za Uchumi, Uhasibu, Fedha, Manunuzi, na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

iv. Kuendelea na matayarisho ya ujenzi wa ofisi zitakazoshirikisha Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara inakusudia kutekeleza yafuatayo:

i. Kusimamia ujenzi wa jengo la ofisi za Wizara tatu Pemba,

ii. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi 90 wa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani za Uchumi, Uhasibu, Ugavi na Manunuzi, Sheria na Utawala,

iii. Kuandaa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi 50 kwa lengo la kuielewa vizuri Sheria mpya Namba 2 ya Utumishi wa Umma, na

iv. Kuwapatia udhamini wanafunzi 1,200 katika vyuo mbali mbali Tanzania katika fani za Uchumi, Uhasibu, Ugavi na Manunuzi na Mawasiliano ya Habari.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara inaombewa jumla ya TZS 11,246.72 millioni kwa kazi za kawaida zikiwemo TZS 7,516.0 milioni kwa matumizi ya viongozi wakuu wa Kitaifa.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika**,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina majukumu kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango na sera mbali mbali za Wizara, kusimamia shughuli za tafiti ndani ya Ofisi na taasisi zake, kusimamia maeneo yanayohusu sekta ya fedha, kuratibu masuala Mtambuka na kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Sekta ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, Idara kwa mwaka 2011/12 imetekeleza kazi zifuatazo:

i. kuandaa sera na Mkakati wa Taasisi ndogo ndogo za kifedha (Microfinance Policy na Strategy) kwa kushirikiana na BoT na UNDP,

ii. Kusimamia maandalizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2012/2013;

iii. Kuandaa warsha mbili na semina moja za kuhamasisha wafanyakazi kuhusiana na masuala ya mtambuka,

iv. Kuratibu utekelezaji wa programu sita na miradi 12 ya maendeleo ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo,

v. Kushiriki katika mikutano minne huko Tanzania Bara iliyojadili mageuzi ya sekta ya fedha na uimarishaji wa Sekta ndogo ndogo za fedha nchini;

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2011/12, idara ilipangiwa kutumia Tshs 107.80 milioni hadi kufikia Juni imeshatumia TZS 81.52 milioni sawa na asilimia 75.62 ya makadirio kwa kazi za kawaida. Kwa upande wa kazi za maendeleo idara ilikadiriwa kutumia TZS 48,840 millioni ikiwa ni mchango kutoka kwa washirika wa maendeleo na wa Serikali. Mpaka kufikia Juni 2012 Idara imetumia jumla ya TZS 29,601.17 milioni sawa na asilimia 60.6 ya makadirio kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/13, idara inakusudia kutekeleza yafuatayo:

i. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa sera na sheria za Ofisi na taasisi zake, ikiwemo ukamilishaji wa Sera na Mkakati wa Taasisi ndogo ndogo za kifedha,
ii. Kusimamia marekebisho ya Sheria za ZSSF, ZIPA na za taasisi nyengine,
iii. Kusimamia shughuli za utafiti wa Sekta nzima ya fedha nchini na kuratibu masuala ya Mtambuka, na
iv. Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Ofisi, kuratibu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ikiwemo Mpango kazi wa Ofisi na kuratibu utekelezaji wa miradi ya Ofisi.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu hayo kwa mwaka 2012/13, idara inaombewa jumla ya TZS 404.73 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 20,504.69 milioni kwa kazi za maendeleo zikiwemo za program ya ZUSP na Porgram ya Mageuzi ya Uimarishaji wa Fedha za Umma (PFMRP).

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais – Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Pemba ina majukumu ya kuratibu shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka 2011/12 Ofisi imetekeleza yafuatayo:

i. Kuimarisha huduma za mtandao wa IFMS,
ii. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 12,
iii. Kufanya uhakiki wa manunuzi katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Michezo na Utalii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Ofisi ya Rais – Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo,
iv. Kufanya kazi ya ukaguzi wa mali za Serikali ulifanyika katika Ofisi ya Rais – Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo; Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati; Wizara ya Kilimo na Maliasili; Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano; Mamlaka ya Maji pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege;
v. Kutoa mafunzo kwa Maofisa Wadhamini, Maofisa Tawala wa Mikoa na Wilaya pamoja na Maofisa Manunuzi wa Wizara za Serikali juu ya Sheria ya Manunuzi (Public Procurement Act No. 9, 2005).
vi. Kuwapatia mafunzo wahasibu, washika fedha na wakaguzi wa ndani wa hesabu juu ya Sheria Nam. 5 ya 2005 (Sheria ya Fedha). Jumla ya Wahasibu, Washika fedha na Wakaguzi wa ndani 63 wa Mawizara walipatiwa mafunzo hayo;
vii. Kuwapatia mafunzo Maofisa Mipango 24 juu ya uandaaji wa Bajeti. Aidha Kamati za Shehia 34 zimepatiwa mafunzo ya uwekaji kumbukumbu na kuratibu shughuli zote zinazohusiana na Mpango wa YCSPD.
viii. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wote wa Ofisi ya Pemba kuhusiana na njia za kujikinga na maambukizo mapya ya VVU, Upimaji wa damu kwa hiari, na ushauri nasaha na kuwapatia mafunzo kamati ya Jinsia ya Ofisi ya Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 713.66 milioni kwa kazi zake za kawaida. Mpaka kufikia mwezi Juni 2012, Ofisi iliweza kutumia jumla ya TZS 612.6 milioni sawa na asilimia 85.8 ya makadirio kwa kazi za kawaida.
Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013, Ofisi ya Pemba itaendelea na majukumu yake ya;

i. Kuandaa mazingira bora kwa ajili ya kuongeza ufanisi na huduma bora za kazi,
ii. Kufanya uhakiki na kutoa huduma za manunuzi na usimamizi wa mali za Serikali kwenye mawizara /taasisi zake,
iii. Kuratibu na kuimarisha shughuli za uhasibu Serikalini,
iv. Kuratibu miradi ya Kitaifa na kusimamia utekelezaji wa Mipango na Bajeti za Wizara na taasisi zake,
v. Kuratibu shughuli za rasilimali watu pamoja na kuimarisha mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu katika shehia na kuendeleza shughuli Mtambuka kwa Ofisi kuu Pemba, na
vi. Kuendeleza mtandao wa IFMS na huduma nyengine za kiofisi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013 Ofisi inaombewa kutumia jumla ya TZS 962.75 milioni kwa kazi za kawaida.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ DAR ES SALAAM

Mhe. Naibu Spika**,** Idara ya Uratibu Shughuli za SMZ Dar es Salaam inajukumu la kuratibu kazi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa SMT hususan Wizara za Fedha, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Tume ya Mipango ya Serikali ya Muungano. Aidha, Idara inaratibu masuala ya SMZ na Ofisi za Balozi mbalimbali zilizopo Tanzania, wadau wa maendeleo pamoja na mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yenye ofisi Tanzania Bara**.**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2011/2012 Idara iliweza kutekeleza yafuatayo:
i. Kuhudhuria mikutano mbali mbali inayoandaliwa na Wizara za SMT na taasisi zake.
ii. Kushiriki mkutano wa 49 wa mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), mkutano uliofanyika kwa mara ya kwanza nchini Tanzania,
iii. Kuratibu mazungumzo na balozi mbali mbali zilizopo Nchini, na
iv. Kuratibu upatikanaji wa nafasi za mafunzo nchi za nje yaliyotolewa na Serikali za nchi mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2011/12 Idara iliidhinishiwa kutumia TZS 192.37 milioni kwa kazi za kawaida. Mpaka kufikia mwezi Juni 2012, Idara imeweza kutumia TZS 153.22 milioni sawa na asilimia 79.6 ya makadirio kwa kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uratibu itaendelea na kazi zake zifuatazo:
i. Kuratibu na kukuza ushirikiano baina ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na zile za Serikali ya Jamhuri ya Muungano,
ii. Kuratibu ushirikiano wa kiuchumi na kimaendeleo baina ya SMZ na ofisi za Balozi za nje na mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yaliyopo Dar es Salaam,
iii. Kushiriki katika mijadala na mikutano mbali mbali,

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uratibu Shughuli za SMZ inaombewa jumla ya TZS 258.28 milioni kwa kazi za kawaida.

TAASISI NYENGINE ZILIZOCHINI YA OFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO.

MFUKO WA BARABARA

Mhe. Naibu Spika**,** Mfuko wa Barabara unaendelea na majukumu yake ya uratibu wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Katika mwaka wa fedha wa 2011/12, Mfuko wa Barabara ulitarajia kupokea jumla ya TZS 6,432.0 milioni. Kati ya fedha hizo TZS 5,463.0 milioni ni kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara na TZS 969.0 milioni zilitengwa kwa ajili ya kazi za uendeshaji.

Mhe. Naibu Spika**,** hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012 jumla ya TZS 5,569.0 milioni zimekusanywa. Matumizi halisi yaliyofanywa ni TZS 4,230.0 milioni**,** ambapo kati ya hizo TZS 3,327.0 milioni ni kwa kazi za matengenezo ya barabara. Aidha kazi zenye thamani ya TZS 701.0 millioni bado zinaendelea na malipo yake yatafanywa mara zitakapokamilika. Vile vile TZS 903.0 milioni zimelipwa kwa ajili ya uendeshaji Mfuko yakijumuisha malipo ya mwisho kwa ujenzi wa ofisi ya Mfuko.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Mfuko umeweza kutekeleza yafuatayo;

viii. Kusimamia ukamilishaji wa mradi maalumu wa utafiti wa hali ya barabara "Roads Maintanance Management Systems" (RMMS). Mradi huo umeshakamilika na uko tayari kwa kutumika;

ix. Kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi ya Mfuko hapo Kikwajuni,

x. Kukamilisha ripoti za ukaguzi wa fedha na ule wa kazi ili kuona thamani ya kazi inalingana na fedha iliyotolewa,

xi. Kuandaa ripoti ya mwaka 2010/11 ya utendaji wa Mfuko,

xii. Kuwapatia mafunzo watendaji wanne wa Mfuko na wafanyakazi watatu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano,

xiii. Kuhudhuria mikutano ya Jumuiya ya Afrika ya Mifuko ya Barabara (ARMFA), na

xiv. Kutoa mafunzo ya utunzaji wa barabara kwa wafanyakazi watano wa Mfuko, wajumbe watatu wa Bodi, wataalamu ishirini na nne kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na wadau mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha wa 2012/13, Mfuko wa Barabara unaombewa ruzuku ya TZS 6,320.0 milioni kwa matengenezo ya barabara na uendeshaji wa Mfuko.

CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA – CHWAKA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Uongozi wa Fedha (ZIFA) kina jukumu la kutoa mafunzo ya fani ya fedha na fani zinazolingana, kuandaa semina za kiutawala na kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani maalumu.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Chuo kimetekeleza mambo yafuatayo:

i. Kusajili na kufundisha wanafunzi 1,226 wa ngazi mbali mbali,

ii. Kutoa ushauri katika Wizara ya Habari, Utamaduni Utalii na Michezo, Shirika la Umeme (ZECO), Manispaa ya Zanzibar,

iii. Kuanza maandalizi ya kuanzisha Kituo cha Kujifunza (Incubation Center) ndani ya Chuo,

iv. Kuwapeleka walimu 15 katika mafunzo ya muda mfupi ya ndani na nje ya nchi, pamoja na kuwapeleka wafanyakazi saba wasiokuwa walimu katika mafunzo ya muda mfupi;

v. Kupeleka masomoni walimu wanne katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (PhD) na wawili Shahada ya Uzamili (Masters),

vi. Kukamilisha ujenzi wa dakhalia,

vii. Kuendesha mafunzo ya muda mfupi na wadau mbali mbali,

viii. Kuanzishwa shahada ya kwanza ya Fedha na Benki pamoja na Stashahada ya Uzamili katika fani ya Uhasibu, na

ix. Kutengeneza Mitaala ya kuanzisha Shahada ya kwanza ya Ununuzi na Ugavi na Shahada ya kwanza ya Teknohama.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Chuo kiliweza kukusanya jumla ya TZS 2,265.89 milioni kutokana na ada za masomo, ruzuku na huduma nyengine na kutumia jumla ya TZS 1,623.0 milioni kwa kazi za

kawaida na TZS 2,776.0 milioni kwa kazi za maendeleo ambapo TZS 1,800 milioni ni mkopo kutoka ZSSF, TZS 500 milioni ni mchango wa Serikali na TZS 476.53 milioni inatokana na makusanyo ya chuo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo kimepanga kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kusajili na kufundisha wanafunzi 1,400 katika ngazi na fani mbali mbali,

ii. Kujenga ofisi, madarasa, vyumba vya kompyuta, ukuta kwenye jengo jipya la dakhalia pamoja na kutengeneza viwanja vya michezo,

iii. Kukamilisha ununuzi wa samani za jengo la dakhalia,

iv. Kufanya tafiti mbali mbali za kiuchumi na kijamii,

v. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi walimu 24 na wafanyakazi watano wasiokuwa walimu,

vi. Kuwawezesha walimu sita katika mafunzo ya Shahada ya Uzamivu,

vii. Kuwawezesha walimu wawili kufanya mitihani ya kitaaluma ya CPA na ACCA,

viii. Kufanya mapitio ya mtaala wa Diploma ya Uhasibu,

ix. Kuwawezesha wafanyakazi watatu wasiokuwa walimu kwa mafunzo ya muda mrefu, na

x. Kuanzisha na kukiimarisha kituo cha ujasiriamali (incubation center).

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Uongozi wa Fedha kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kinaombewa ruzuku ya TZS 1,641.0 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 750.0 milioni kwa kazi za maendeleo. Chuo pia kimekadiria kukusanya jumla TZS 1,313.88 milioni kutokana na ada na huduma inazozitoa.

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika**,** Shirika la Bima la Zanzibar lina jukumu la kutoa huduma za bima za ajali, majanga na watu binafsi na kukusanya mapato yatokanayo na huduma hizi. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Shirika lilikadiria kukusanya mapato kutokana na ada za bima ya TZS 10,455.60 milioni. Mpaka kufikia mwezi Juni 2012, Shirika limeweza kukusanya jumla ya TZS 9,106.58 milioni sawa na asilimia 87 ya lengo. Aidha katika mwaka huo wa fedha Shirika limelipa fidia ya TZS 4,091.91 milioni kwa wateja mbalimbali kwa mujibu wa mikataba. Shirika pia limekamilisha ujenzi wa Ofisi mpya na ununuzi wa vifaa uliogharimu jumla ya TZS 1,141.10 milioni.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka 2012/2013, Shirika limejipangia kukusanya mapato yatokanayo na huduma inazozitoa yenye thamani ya TZS 11,747.98 milioni, sawa na ongezeko la asilimia 12.4 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2011/2012. Aidha, Shirika limepanga kutumia jumla ya TZS 3,391.75 milioni kwa kazi zake mbalimbali za kawaida na kukadiria jumla ya TZS 1,000.0 milioni kwa kazi za maendeleo.

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ni kupokea mafao ya wafanyakazi na hatimae kuyarejesha kwa walengwa muda unapofikia. Kwa mwaka wa fedha 2011/12 Mfuko umetekeleza kazi zifuatazo:

i. Kusajili waajiri 87 dhidi ya lengo la kusajili waajiri 85 sawa na asilimia 102**.** Wanachama waajiriwa waliosajiliwa ni 4,256 dhidi ya lengo la kusajili Waajiriwa 4,000 sawa na asilimia 106,

ii. Kulipa wanachama 848 mafao yao dhidi ya lengo la kuwalipa wanachama 840**,** fedha zilizotumika kulipa mafao hayo ni TZS 3,800.0 milioni,

iii. Kulipa pencheni ya TZS 919.56 milioni kwa wanachama 4,123 na kurejesha TZS 403.31 milioni kwa wanachama 145 waliokosa sifa za uwanachama,

iv. Kukamilisha matayarisho ya kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kuufanyia mageuzi Mfuko ambapo kampuni ya Muhanna & Co. Actuaries & Consultant imeteuliwa kuifanya kazi hiyo,

v. Kuwekeza katika maeneo ya muda mrefu na yale ya muda mfupi, yakiwemo dhamana za Serikali, hesabu za muda maalum, hati fungate za Serikali, ununuzi wa hisa na utoaji wa mikopo,

vi. Kuanza matayarisho ya ujenzi wa kiwanja cha Kufurahishia watoto Kariakoo na ujenzi wa nyumba za bei nafuu, na

vii. Kukusanya michango ya wanachama yenye jumla ya TZS 19,900.0 milioni dhidi ya lengo la TZS 18,900.0 milioni sawa na asilimia 105**.**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Mfuko unatarajia kufanya kazi zifuatazo:

i. Kuongeza wigo wa kusajili wanachama kutoka katika sekta isiyo rasmi kwa kutumia Mfumo wa uchangiaji wa hiari (Zanzibar voluntary social security scheme),

ii. Kuendeleza matayarisho ya ujenzi wa nyumba za mkopo nafuu huko Tunguu, pamoja na kukamilisha taratibu zinazoendelea kwa ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha UHURU (Kariakoo). Katika uendelezaji huu, zabuni mpya itatolewa na hatimae kumpata mkandarasi atakaeweza kuifanya kazi kama inavyopaswa, na

iii. Kuanza matayarisho ya ujenzi wa nyumba za uwekezaji katika eneo la Mbweni.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza kazi hizo, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Mfuko umetenga jumla ya TZS 10,500.0 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo ya utayarishaji wa Tenda na maandalizi ya ujenzi, maandalizi ya nyumba za Tunguu na maandalizi kwa nyumba za Mbweni.

E.5 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (*PBZ*)

Mhe. Spika, jukumu kubwa la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni kupokea amana za wateja wake na kukopesha kwa wanaohitaji. Kwa mwaka 2011/12 Benki imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Kupokea amana za wateja zenye kima cha TZS 59,950.0 milioni ikiwa ni asilimia 92 ya lengo lililowekwa la TZS 65,430.0 milioni,

ii. Kutoa mkopo wa jumla ya TZS 66,300.0 milioni sawa na asilimia 178 ya lengo lililowekwa la 37,060.0 milioni kwa mwaka, na

iii. Kuweza kuongeza rasilimali ya Benki za TZS 76,450.0 milioni ikilinganishwa na lengo la TZS 100,000.0 milioni.

iv. Kupata mapato ya TZS 18,660.0 milioni yanayotokanayo na huduma mbali mbali za kibenki ambayo ni sawa na asilimia 113.3 ikilinganishwa na makadirio ya TZS 16,480.0 milioni.

Mhe. Spika, Kuhusu maendeleo ya Benki ya Kiislamu Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 imeweza kujipatia jumla ya wateja TZS 12,000. Amana za wateja zimeweza kufikia jumla ya TZS 12,030.0 milioni. Kwa upande wa mikopo benki imeshatoa mikopo yenye thamani ya jumla ya TZS 1,700.0 milioni, ambapo wakopaji ni wafanyakazi wa serikali, taasisi za serikali na mashirika binafsi.

Mipango zaidi inaendelea ili kuweza kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo. Kwa wastani, Benki ya Kiislamu ya PBZ inakuwa kwa wastani wa zaidi ya asilimia 100 kwa kila robo mwaka kwa upande wa wateja na amana zinazo kusanywa. Kwa sasa huduma hii inapatikana kwenye matawi matatu ambayo ni Mwanakwerekwe Unguja, Chakechake Pemba na Dar es Salaam.

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2012/2013 PBZ imekusudia kutekeleza yafuatayo:

i. Kujenga jengo jipya na la kisasa kwa ajili ya Makao Makuu ya Benki;

ii. Kuongeza mtaji wa Benki,

iii. Kutengeneza njia mpya ya kuwafikia wateja kama kupitia kwa simu za mikonononi na mfumo wa mtandao wa intaneti,

iv. Kufungua matawi zaidi ikiwa ni pamoja na Tanzania Bara kwa lengo la kukidhi haja ya soko,

v. Kufanya utafiti na kubadilisha program mama ya benki na mfumo wa mawasiliano baina ya matawi ya benki, mawasiliano yatakuwa kwa kutumia mfumo wa waya za "*fibre optic",*
vi. Kufungua mashine za *ATM* zenye uwezo wa kutoa huduma za *VISA* na *Master cards*,
vii. Kuanza kutoa huduma za mikopo ya nyumba kwa wananchi wa Zanzibar na wateja wake wengine (*mortgage financing*) na mikopo midogo midogo, na
viii. Kutangaza na kutoa huduma kwa wazanzibari wanaoishi ughaibuni (*Diaspora*) pamoja na kuanzisha uhusiano na mabenki mbalimbali yenye mitandao mikubwa duniani.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2012/2013, PBZ imepanga kujikita zaidi katika ushindani pamoja na kuiimarisha Benki ya Kiislamu ili iweze kuwa na nguvu zaidi na inatarajia kufunguwa matawi mengine likiwemo Mpirani katika jengo la Bima.

HITIMISHO

Mhe. Spika, Kama nilivyosema awali kwamba nitaeleza zaidi juu ya mapendekezo ya Serikali juu ya ufanikishaji wa ununuzi wa meli mpya, sasa naomba niliarifu Baraza lako Tukufu juu ya mapendekezo hayo. Nia ya Serikali, ni kununua meli moja kubwa ili kuimarisha huduma za usafiri baharini.

Serikali inapendekeza kuchukuliwa hatua mbili kwa (i) kuongeza kiwango cha mkopo wa ndani kutoka *PBZ* na *ZSSF*, (ii) kufanya marekebisho ya Bajeti kwa kubana matumizi ya kawaida kwa baadhi ya vifungu kwa Wizara zote ili kuongezea kufikia kiwango kitakachohitajika baada ya kufahamika gharama halisi (iii) fedha zilizoondolewa kutoka katika bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Idara ya Ushirikiano wa kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje TZS 40.0 milioni. Fedha zote zitakazopatikana katika marekebisho hayo zitahamishiwa Mfuko Mkuu wa Serikali katika kifungu cha matumizi maalum ya Serikali.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba hatua ya kubana matumizi itaathiri bajeti za Wizara zetu. Wizara zitalazimika kufanya mapitio ya malengo na kufanya usawazishaji ili kwenda sambamba na fedha zitazobakia katika vifungu husika na shughuli zilizolengwa awali kwa kuzingatia vipaumbele. Hata hivyo, kwa kuwa matumizi haya ni muhimu sana kwa maisha ya jamii yetu, naamini Baraza lako hili tukufu litaridhia mapendekezo haya kwa kauli moja.

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kukupongeza kwa dhati kwa umahiri wako wa kuuendesha muhimili huu wa dola. Kwa mara nyengine tena Baraza letu limejijengea heshima kubwa kwa namna linavyoendeshwa, Wajumbe wako wakitimiza vyema wajibu wao wa kuwawakilisha wananchi. Kwa namna ya pekee naomba pia niwapongeze sana kwa upeo wao, wa kupambanunua mambo.

Mhe. Spika, Ofisi yangu ina majukumu nyeti sana katika maendeleo ya wananchi, uendeshaji wa Serikali na uimarishaji wa utawala bora nchini. Binafsi nafarajika sana na wasaidizi wangu kiutendaji na wafanyakazi wote. Naliomba Baraza lako tukufu liendelee kuiamini Ofisi hii na kuipa mashirikiano makubwa zaidi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/13 naomba Baraza liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya TZS **343.45** bilioni na matumizi ya jumla ya TZS **130.760** bilioni kati yake ikiwa TZS **39.584** bilioni ni kwa kazi za kawaida na TZS **38.352** bilioni kwa ajili ya kazi za maendeleo kwa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na TZS **52.824** bilioni kwa matumizi ya Mfuko Mkuu wa serikali kama inavyoonekana hapa chini;

MWELEKEO WA BAJETI 2012/2013

		TZS bilioni
I.	**Matumizi ya Kawaida**	**39.584**
	Mishahara	3.820
	O/C	13.866
	Ruzuku kwa Taasisi	16.888
	Marekebisho ya Mishahara	5.010
II.	**Matumizi ya Kazi za Maendeleo**	**38.352**
	Mchango wa Serikali	8.325
	Ruzuku na Mikopo	30.027

III.	**Mfuko Mkuu wa Serikali**	**52.824**
	JUMLA KUBWA	**30.760**

Mhe. Spika, Uchambuzi wa mapendekezo ya mapato na matumizi hayo pamoja na muhtasari wa maelezo mengine unaonekana katika (viambatanisho i-xi)

Mhe. Spika, Pamoja na hotuba hii naomba kuwasilisha muhtasari wa maelezo ya bajeti inayozingatia programu maalum (PBB) kama inavyoonekana katika (kiambatisho xi)

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Salmin Awadh Salmin: (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukuwa nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezimungu kwa kutujaalia neema ya uhai, uzima na afya na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yetu ya kujenga nchi yetu kwa maslahi ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ya kusimamia vyema majukumu ya Wizara hii ambayo ndiyo moyo na uhai wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya mfumo wa Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Wajumbe wa Kamati hii ya Fedha, Bishara na Kilimo kwa mashirikiano waliyonipa, michango na mawazo yao kwa Serikali kupitia Wizara hii kila Kamati ilipofanya kazi yake.

Kazi, juhudi na moyo wao wa kujituma bila ya kuchoka, imetufikisha katika mafanikio, hata leo hii inawezekana kusimama kwa niaba yao kuwasilisha hotuba hii.

Mheshimwa Spika, naomba uniruhusu, kwa heshima kubwa, niwataje Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti
2.	Mhe. Abdalla Mohamed Ali	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mjumbe
4.	Mhe. Rufai Said Rufai	Mjumbe
5.	Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Mjumbe
6.	Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Mjumbe
7.	Mhe. Hamad Masoud Hamad	Mjumbe
8.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	Mjumbe
9.	Ndg. Shemsa Maabad Mohamed	Katibu
10.	Ndg. Khamis Hamad Haji	Katibu

Mhe. Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii adhimu kumkaribisha Mhe. Hamad Masoud Hamad katika Kamati yetu hii ya Fedha, Biashara na Kilimo. Kamati yetu inaamini kwamba Mhe. Masoud atautumia uzoefu alioupata serikalini, ambao utasaidia kuzisimamia vyema wizara zilizo chini ya kamati yetu.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ina jukumu la Kitaifa na kisekta kufuatilia mipango ya kitaifa, ukuaji uchumi, kuongeza na kukusanya mapato, upatikanaji wa misaada na mikopo, kuandaa program za maendeleo, kuandaa bajeti, kusimamia deni la taifa, takwimu na utunzaji wa mali za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango ya Sekta na Kupunguza umasikini ndiyo inayoratibu dira ya maendeleo ya 2020, ufuatiliaji MKUZA II n.k Idara hii katika dhamira ya kuandaa mafunzo ya uchambuzi wa sera mbali mbali kwa maafisa mipango, ili waweze kusimamia sera hizo Kamati inashauri ni vyema mafunzo hayo yasiishie kwa

maafisa mipango wa mawizara peke yake, mafunzo hayo yashuke mpaka kwa maafisa mipango wa wilaya na mikoa, ambao wanasimamia sehemu kubwa ya wananchi moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ukuzaji Uchumi, huratibu mwenendo wa uchumi na kutoa ushauri kwa Serikali. Katika mwaka 2011 ukuaji uchumi ulifikia asilimia 6.1% kwa mwaka wa 2010. Hali hii ya mfumuko wa bei siyo nzuri, ukiangalia hali za maisha ya wananchi wetu ambao wengi wao ni wenye kipato cha chini na kwa maana hiyo mfumuko wa bei kama huu unaathiri maisha yao kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Naibu Spika, mwenendo wa kodi nchini unapaswa kutazamawa upya kwa kuzingatia wazalishaji wadogo wadogo ambao hawana mitaji mikubwa, kamati yangu inaomba serikali ifikirie kuwapunguzia utitiri wa kodi za bidhaa na mali ghafi wazalishaji hawa kwa vile wanahangaika katika kujinasua na hali ngumu ya maisha kwa kufanya biashara za mitaji midogo, ambayo wanakosa fursa za kuikuza kutokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili kama vile riba kubwa za mabenki na ukosefu wa masoko ya uhakika. Haileti picha nzuri kuona wawekezaji wakubwa wanapewa *'tax holiday'* halafu wazalishaji wetu wadogo wadogo masikini wanabeba mizigo ya kodi.

Hata hivyo, kamati yetu bado inasisitiza juu ya suala zima la kuangalia mpango huu wa kuwapa Wawekezaji nafuu hii ya kutokulipa kodi kwa muda. Tuna wasiwasi kwamba wengine nafuu hii huitumia vibaya kwa kubadilisha badilisha majina ya Wawekezaji na hivyo kuendelea kuitumia fursa hii kwa muda mrefu kwa kisingizio cha kwamba wao ni wapya kumbe ukichunguza sana mmiliki ni yule yule. Suala la kuwapa motisha Wawekezaji si baya lakini nao ni vyema tuwaangalie uaminifu wao.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango ya Watendakazi pamoja na majukumu mengine ina wajibu wa kuratibu maendeleo ya mama na mtoto pamoja na hali ya utumishi nchini. Kamati yangu inapendekeza kuwapo kwa utaratibu wa kuweka taarifa sahihi za maendeleo ya mama na mtoto kuanzia ngazi ya shehia na vijiji, hii itarahisisha upatikanaji wa takwimu zitakazosaidia kutatuwa matatizo yanayokabili mama na mtoto kuanzia ngazi za chini. Kadhalika, kamati yangu inashauri Serikali kuhakikisha kuwa zoezi la utafiti wa hali ya utumishi liende sambamba na kuibua vyanzo vya upatikanaji wa wataalamu kwa kupitia mitaala ya elimu ili iweze kuzalisha wataalamu katika kada tofauti.

Mhe. Naibu Spika, mafanikio ya kiuchumi na mipango hutegemea takwimu sahihi. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ina wajibu mkubwa kukusanya, kuchambuwa na kutoa takwimu. Kamati yangu inapenda kuweka mkazo katika mipango ya bajeti na kushauri kuwa ni vyama bajeti zetu zikazingatia uhalisi wa matumizi ya takwimu katika nyanja tofauti kama vile kilimo, uwekezaji na kilimo. Takwimu sahihi zina umuhimu mkubwa kuwezesha mipango yetu kupanga bajeti ya uhakika.

Mhe. Naibu Spika, Mfano halisi hapa ni katika sekta ya utalii na ajira katika mahoteli ya kitalii, ambako takwimu hazipo wazi. Kamati yangu inapendekeza takwimu zionyeshe ni vijana wangapi wa Zanzibar wameajiriwa katika sekta ya mahoteli, kima gani cha chini cha mshahara wanalipwa, wangapi wana mikataba ya uhakika, wangapi wameajiriwa katika kazi za kitaalamu, wangapi wana uwezo wa kufanya kazi za mahoteli ambazo wameajiriwa wageni n.k Uwepo wa takwimu kama hizi utarahisisha kujuwa ni kwa kiasi gani sekta ya mahoteli inachangia kukuza uchumi na kuinua hali za maisha za wananchi wetu hasa vijana.

Mhe. Naibu Spika, zoezi la sensa nalo linakaribia na umuhimu wake kwa maendeleo ya taifa letu ni mkubwa, hivyo kamati yangu inapenda kuikumbusha serikali kuongeza kasi ya kampeni na matangazo ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa wakati utakapofika, aidha, kamati inatowa wito kwa wananchi wote kushiriki kikamilifu ili kuliwezesha zoezi hili kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, Mpango wa Bajeti ya Programu (*PBB*) ni mpya na umeanza kwa Wizara sita ikiwamo Wizara hii ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kamati yangu imeona kuwa mfumo huu uelezwe vizuri na ushiriki wa wananchi uanze katika ngazi za chini inakolengwa miradi na program zenyewe. Aidha, Kamati yangu inashauri Serikali kabla ya kuendeleza mpango huu kwa Wizara sita zilizoanza, pamoja na mafanikio yatakayopatikana kulingana na mfumo wa bajeti ya zamani (*MTEF*).

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mhasibu Mkuu, mbali na kutoa miongozo ya kiuhasibu kwa Wizara na taasisi za serikali, ina wajibu pia wa kusimamia taratibu za kukabidhi matumizi. Kamati yangu inaiagiza serikali kutazama

kwa umakini mkubwa mfumo wa udhibiti wa matumizi ya Serikali (*IFMS*) kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima ili kuokowa fedha za serikali na kuelekeza katika vipaumbele vyengine. Leo tunapanga kununua meli kupitia vifungu ambavyo tayari tulishavipitisha kwa matumizi mengine jambo ambalo linashangaza laiti kusingekuwa na tatizo hilo maana yake fedha hizo zingetumika katika maeneo ambayo kumbe wala hayakuwa na umuhimu mkubwa. Kwa maana ya kuwa hayakuwa ni kipaumbele chetu.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma ina jukumu la uhakiki wa mali za Serikali pamoja na kusimamia ununuzi na uondoaji wa mali za Taasisi za Serikali na mashirika. Changamoto kubwa hapo ni kuwa bado mali nyingi za Serikali hazijatambuliwa na zile zilizotambuliwa baadhi yao hazijapatiwa hatimiliki. Hivyo, basi, kamati yangu inashauri kufanyike juhudi za makusudi kufanya utambuzi huo na kutoa hati miliki ili kuepuka upoteaji wa mali za Serikali. Ile hadithi ya uwekaji wa Daftari la Mali (*Asset Register Book*) kwa kila Wizara ifike pahala imalizike kwani ni ya muda mrefu na ina umuhimu mkubwa katika kudhibiti mali za Serikali na kutambuliwa taarifa zake. Kwa mfano zimenunuliwa lini, bei gani, na mambo mengine ambayo yanaweza kusaidia hata pale inapoonekana mali hiyo sasa haifai tena kwa matumizi ya Afisi na inataka kuondosha kwa njia yoyote kama kuuza au vyenginevyo kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Naibu Spika, Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali inahitaji marekebisho, kwasababu ilivyo sasa haiendani na hali ya uchumi wa nchi yetu kwa upande wa ununuzi wa vitu vipya, kama sheria inavyolazimisha. Mfano, katika sekta ya usafiri na mawasiliano ambayo zana na vifaa vyake kama vile mashine za uchukuzi bandarini, meli na vifaa vya ujenzi wa barabara vina gharama kubwa. Baadhi ya nchi za jirani zimeshafanya mabadiliko ya sheria zao za manunuzi na sasa wanaweza kununua vifaa na zana kama hizo kwa vifaa vilivyoanza kutumika kwa masharti maalum. Kamati yangu inashauri kuwa ni vyema basi Serikali yetu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikafikiria kufanya marekebisho ya sheria hiyo ili kujivua na kifungo hicho, kwani waswahili wanasema *lisilobudi hutendwa*.

Mhe. Naibu Spika, Kamati pia inatoa pendekezo kwa Serikali kuanzisha jarida au toleo la wazi maalumu la ukaguzi wa kidumu (*Permanent Audit Journal*) ili umma ujuwe ni taasisi ipi ya serikali imefanya manunuzi au imeondowa mali kwa mujibu wa sheria ya manunuzi na ipi haikufanya hivyo. Utaratibu huu utasaidia uwepo wa taarifa za wazi kila wakati na kurahisisha ufatiliaji wa matumizi mabovu ya fedha kwa baadhi ya taasisi hizo kila mara.

Mhe. Naibu Spika, Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) ina mchango kubwa katika kusaidia maendeleo ya nchi yetu, ni urithi tulioachiwa na viongozi wetu, waasisi wetu waliopita, hivyo ni vyema tukaiendeleza na kuimarisha huduma zake, kwani wahenga walisema *"kimfaacho mtu chake".* Kamati yangu inaishauri *PBZ* kutanua mchango wake wa kijamii ambao bado ni mdogo ukilinganisha na benki nyingine binafsi. Hii ni benki ya wananchi wa Zanzibar, ionekane basi, ikiwa mstari wa mbele kutumia sehemu ya faida yake katika mambo madogo madogo ya kusaidia jamii kama zifanyavyo benki nyingine binafsi.

Mhe. Naibu Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) ndiyo pekee wenye wanachama wengi hapa nchini, kamati ingependa kuoana kama wanavyopendekeza wananchi kuwa Mfuko uwekeze katika miradi mikubwa ya uwekezaji kama vile uzalishaji wa chakula, viwanda, majengo ya kisasa na miundombinu n.k ambayo inafaida kubwa katika kuendeleza mfuko.
Kamati pia inataka kujuwa hatua zilizofikiwa na *ZSSF* katika ujenzi wa kiwanja cha Kariakoo ambacho ni siku nyingi sasaumekuwa ni kitendawili. Kadhalika, kama inashauri maekebisho ya sheria ya *ZSSF* yafanywe kwa kushirikisha wadau wote.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Ukuzaji na Uendelezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) inafanya kazi kubwa ya kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje katika kukuza uchumi, kuongeza mapato ya Serikali, kuongeza teknolojia mpya na kuleta ajira. Kamati imeona kuwa ili kazi hiyo iwe ya mafanikio zaidi ni vyema maeneo ya uwekezaji yaimarishwe kwa kuwekewa miundo mbinu ya maji, umeme na barabara za uhakika pamoja na usalama, ili wawekezaji wanapokuja wakute mazingira ya uwekezaji yanavutia. Pamoja na hayo juhudi za makusudi zifanyike ili kuwa na aina nyengine ya uwekezaji badala ya kuegemea zaidi kwenye sekta ya Utalii. Tunadhani idadi ya Hoteli za kitalii kwa sasa inaridhisha na ni muda muafaka wa kuangalia maeneo mengine.

Aidha, Kamati inasisitiza kua bado suala la urasimu linaonekana kurudisha nyuma ari ya wawekezaji hasa katika sekta ya utalii, ambapo baadhi ya miradi inayoendelea ilionekana kusita kutoka na kuchelewa vifaa vyao bandarini kwa kile walichoeleza kuwa ni urasimu. Maneno ya *One Stop* yasibakie kama kauli mbiu tu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaitahadharisha Serikali kupitia Wizara hii kuwa makini na urasimu usiokuwa wa lazima kwa vile mwekezaji ni kama mteja, iwapo bidhaa au huduma zitakuwa mbovu au hasizopo basi ni rahisi mteja huyo kukimbia. Wenzetu waliondelea wana msemo wao wanasema *"unaweza kutumia siku thelathini kutafuta mteja mmoja tu, lakini ikachukua sekunde moja tu kuwapoteza wateja thelathini"*, na ndivyo hivyo hivyo kwa wawekezaji.

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Fedha cha Chwaka (*ZIFA*), ni taasisi muhimu katika maendeleo ya sekta ya fedha, uhasibu, benki, ununuzi na ugavi, kamati inashauri serikali kuwa malengo ya kuanzishwa Chuo hiki siyo kusomesha wanafunzi peke yake, bali pia, kama alivyoeleza Mhe. Waziri kwenye hotuba yake, kazi ya ushauri na utafiti wa mambo ya fedha na uhasibu. Hivyo, ni vyema serikali ikasaidia kuwaendeleza wataalamu waliopo hapo na kuimarisha maslahi yao pamoja na kuziagiza taasisi za serikali kutumia chuo hiki katika tafiti mbali mbali za kiuhasibu na fedha badala ya kutafuta huduma hizo nje, hii itasaidia hata kupunguza gharama za uagiziaji na utegemezi wa huduma kama hizo kutoka nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Bima la Zanzibar (*ZIC*) ni miongoni mwa mashirika machache ya serikali yanayopiga hatua za kuridhisha. Kamati yangu inapongeza hatua ya Shirika kukamilisha jengo jipya la Ofisi zake. Aidha Kamati inataka kujua hatua zilizofikiwa za mipango ya Shirika hili ya kuanzisha huduma ya bima ya kiislamu (*takaful*), kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake ya mwaka jana. Kamati inataka pia kujua, mbali na malengo ya ukusanyaji Tshs.11, 747.98 milioni, yaliyoelezwa na Mhe. Waziri katika hotuba yake, ni kiasi gani cha kodi ambacho Shirika limelipa kama mchango wake kwa serikali kama Sheria ya Mitaji ya Umma No.4 ya mwaka 2002 ilivyoagiza.

Mhe. Naibu Spika, Mfuko wa Barabara unajukumu la kuratibu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Ili jukumu hili lifikiwe Kamati inashauri mfuko huu uwezeshwe na uwe wa kujitegemea badala ya kuwa chini ya wizara kama sheria ya kuanzishwa kwake inavyotaka. Aidha, Kamati inatoa ushauri kwa mfuko kuhusu mradi maalumu wa utafiti wa hali ya barabara (*RMMS*), kamati inapendekeza ni vizuri mradi huu uendane na hali ya fedha zilizopo pamoja na vipao mbele, ili kuepusha malalamiko ya upendeleo kwa barabara zinazohusika na mradi huu.

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha za Muungano (*JFC*) ni taasisi muhimu katika kuainisha mchango wa serikali zetu katika mapato ya Muungano, Tume hii ipo kikatiba, Kamati ingependa Wizara ieleze mfuko huu wa pamoja wa fedha umefikiwa wapi, kwa vile hakuna maelezo ya kina katika hotuba ya Mhe. Waziri kuhusu suala hili ambalo hadi hivi sasa kumekuwa na uzito wa kuanza kwake.

Mhe. Naibu Spika, katika muelekeo wa bajeti ya wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2012/13, malengo yanaonesha kua Wizara inakusudia kukusanya jumla ya Tshs.649.3 bilioni. Kamati yangu inaona kuwa bado kuna uwezekano wa kukusanywa fedha zaidi katika vyanzo vya ndani ya mapato, iwapo mianya ya uvujaji wa mapoto na misamaha ya kodi isiyokuwa ya lazima itadhibitiwa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majukumu hayo ya msingi ya wizara hii katika kuandaa bajeti ya serikali ni vyema ikatoa elimu ya kutosha kwa watendaji wa wizara zote, ili matayarisho ya bajeti yawe wazi na yasiyotia shaka kwa Wajumbe. Kwa vile tunaelewa kwamba katika mkutano huu wa bajeti unaomaliza wa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wajumbe wako wengi walikuwa na wasi wasi juu ya makisio yaliyoletwa mbele ya Baraza hasa hasa katika maeneo ya kasma za Vikao na Kamati, Safari za Kikazi na nyenginezo zinazohusiana na manunuzi zilikuwa na makisio makubwa ambapo unakuta kwa mfano bei ya friji tu bei yake inayowekwa hailingani kabisa na uhalisia.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu sasa inaiomba Serikali kupitia Wizara hii kwamba kuanzia mwaka ujao Wizara zinapowasilisha bajeti zao mbele ya Kamati ni lazima zioneshe mchakato wote wa namna walivyoyafikia makisio yao kwa kila kasma. Ule utaratibu kuwasilisha nambari tu hautatusaidia tena. Kamati ioneshwe kitu kimoja kimoja na bei halisi ama za bidhaa au huduma.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu imepitia na kujadili Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii mara mbili ambapo kumekuwa na marekebisho kwa baadhi ya vifungu, marekebisho hayo yamepelekea kuwa vigumu sasa kufuata vifungu katika kitabu kikubwa, hivyo Kamati imepitia marekebisho hayo ambayo yatawasilishwa katika karatasi nyingine mbali "*loose papers*" wakati wa kupitisha vifungu kwenye Kamati ya Matumizi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba hii, na kuwashukuru Wajumbe wako kwa utulivu wao na kunisikiliza.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu imekubaliana na mapendekezo ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2012/13 na inawaomba Wajumbe wako waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuwasilisha muhtasari wa hotuba hii kwa niaba ya Kamati. Sasa nitumie fursa hii adhimu ili nitoe mchango wangu mfupi sana wa jimbo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni.

Mhe. Naibu Spika, nitazungumzia maeneo matatu muhimu. Eneo la kwanza ni Chuo cha Uongozi wa Chwaka. Chuo hiki Mhe. Naibu Spika, kimepiga hatua kubwa. Kama nilivyoeleza kwamba Kamati yangu inaridhishwa kabisa na maendeleo yanayopatikana katika Chuo kile, chuo ambacho kimepiga hatua kubwa kwa muda mfupi kuliko hata vyuo vyengine.

Sasa mimi ushauri wangu kwa Mhe. Waziri juu ya Tume ambayo Mhe. Rais ambaye ndiye anayesimamia wizara hii, ule utaratibu ambao Tume imeupendekeza kuunganisha vyuo mbali mbali, ambapo mchakato wake sasa hivi unaendelea kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimuombe Mhe. Rais kwamba Chuo hiki kinapiga hatua, sijui mapendekezo yanaelezaje, lakini kitendo cha kuunganisha Chuo hiki na vyuo vyengine ni kukirudisha nyuma na kuna hatari Chuo hiki kikapoteza hata ule mwelekeo wake unaoendelea. Kwa hivyo, nimesema nilizungumze hili makusudi na kwa sababu wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ndio kinachosimamia chuo hiki, lakini pia Mhe. Rais aliyeunda hii Tume ndio mapendekezo haya yanapelekwa kutoka kwake.

Kwa hivyo, mimi niombe kabisa kwa niaba ya Kamati yangu kwamba Chuo hiki bado kinahitaji kubakia kama kilivyo kwa manufaa ya wananchi wetu. Vyenginevyo tunaweza tukapoteza ile sifa iliyokuwanayo chuo hiki na hatimaye kikaweza kurejea nyuma. Hilo moja.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni juu ya Shirika la Bima la Zanzibar. Shirika hili limepiga hatua kubwa, nachukua nafasi hii kulipongeza sana shirika hili. Ni shirika ambalo linafanya kazi zake vizuri, linatengeneza faida, matumizi yake yanakwenda vizuri, na ni shirika ambalo linahitaji kupewa msaada mkubwa sana ili liweze kufanya vizuri zaidi. Kwa kweli Shirika la Bima la Zanzibar tunalipongeza sana na tunampongeza sana Mkurugenzi wa shirika hili, kwa juhudi yake na uwezo wake wa kuliendeleza shirika hili na tunamuomba aendeleze juhudi yake na sisi tuko pamoja na yeye.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, ni juu ya ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Pemba. Mhe. Naibu Spika, sikuona taarifa maalum juu ya ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Pemba katika kitabu cha Mhe. Waziri sikuona. Sasa kama taarifa zipo basi Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, basi na atueleze tu kwa muhtasari juu ya maendeleo ya ujenzi wa jengo lile, baada ya ule wa awali kufeli. Kwa sababu bado Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Pemba wanahitaji ofisi. Kwa hivyo, lile lengo ambalo lilikuwa limekusudiwa la kujengwa ofisi, lakini hatimaye likavurugika, namuomba sana Mhe. Waziri aliendeleze, kwa sababu Pemba bado kunahitajika Ofisi ya Wizara ya Fedha, kwa sababu ofisi waliyonayo haina nafasi, wana vifaa vingi vya kisasa na vya kutosha, lakini bado wanabanana na lile lengo tulilokusudia la kujenga ofisi limepotea.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kama taarifa humu haimo au kama imo basi atakapofanya majumuisho basi hebu tupe kwa muhtasari na tuone wizara imejipangaje juu ya ujenzi wa jengo lile katika kipindi hiki cha fedha.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 na niwaombe Wajumbe wote wa Baraza hili waijadili hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa makini, lakini hatimaye sote kwa pamoja tuipitishe ili tumuwezeshe Mhe. Waziri kwenda kufanya shughuli zake. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Sasa nafasi tunampa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadae Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. Waheshimiwa Wajumbe tungewaomba wale wenye nia ya kuchangia wote wangeleta majina yao ili tukaweza kupanga vizuri orodha yetu, sisi hapa tuna Wajumbe wawili tu. Nategemea keshokutwa tukijaaliwa tuendelee moja kwa moja kuchangia, kwa hivyo atakayekuja hapa kwenye hiki kiti basi akute majina yako tayari, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe. Tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi na mimi mchana wa leo ili nikaweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba hii. Kwanza nianze kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na kipenzi chake Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa hotuba yao nzuri sana iliyojipanga mara hii vizuri sana na hasa yule mwanamama niliyeambiwa ni wa uchumi na yeye, kweli nimeona amepanga vizuri katika uchumi huu.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana na nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shein, kwa kukaa pamoja na Waziri wake na kwa kukubali kabisa na kuona hali halisi ya wananchi wa Zanzibar, kwa hali ambayo inatokezea mara kwa mara na kuweza kuwatafutia chombo cha uhakika ambacho ni meli ambayo itakuwa ni kubwa sana ya mfano wake hapa Zanzibar. Kwa hili natoa pongezi kubwa sana tena sana.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri mara nyingi sana mimi husema ni mtu mkweli na muwazi, kwa sababu alituambia tumuachie mafungu halafu huko mbele tutakuja kuyabana. Ni kweli amethubutu kufanya hivyo na amepata bilioni 17, 167, 000,000, tumshukuru sana Mhe. Waziri na hongera sana kwa utendaji wako. *Wallahi* hapa Dk. Shein hakukosea, ametafuta kiongozi mahiri na ni mtendaji na ni mkweli hasa katika Baraza hili. Tunao sisi hesabu ya viongozi hapa mawaziri wa kweli na mfano wake ndio huyu kimejitokeza leo hii. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Hiyo ni moja kati ya ilani ya Chama cha Mapinduzi sera zake za utendaji.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika ukurasa wa 4. Mhe. Naibu Spika, hapa kwenye kifungu cha 10 kinasema; aidha Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inafanya kazi kwa karibu sana na taasisi za Muungano, zikiwemo za Tume pamoja na fedha za Benki ya Kuu ya Tanzania. Hapa mimi nina baadhi ya mambo nataka niulize kidogo. Mimi nafsi yangu ni Mwakilishi wa Jimbo la Kitope, kwa kweli nasema na natamka wazi kuwa Muungano mimi nautaka wala sina tatizo nao, lakini kuna mambo ambayo yananipasa ni lazima niyaseme ndani ya Muungano wenyewe, jinsi ambavyo utakavyotoa maslahi ya Wazanzibari. Hilo sina budi ni lazima niliseme. Mhe. Naibu Spika, kurudia tena ni vibaya kwa mujibu wa kanuni yetu, lakini inanipasa niseme na nakuomba sana unikubalie kwa hilo usinizuie.

Mhe. Naibu Spika, narudia tena, mimi nautaka Muungano wala siukatai kwa roho yangu safi kabisa pamoja na familia yangu. Lakini Mhe. Naibu Spika, ni lazima niuseme Muungano marekebisho yake kwa Wazanzibari. Hapa leo tunaambiwa Mhe. Waziri ametwambia yupo karibu sana na mambo hayo lakini sasa nataka nimuulize swali. Je, katika mambo haya ya karibu Mheshimiwa nimefungua kitabu chote lakini sijaona jinsi gani ile 4.5 humu siioni. Sasa sijui kwa kuwa sina taaluma zaidi au vipi.

Namuomba sana Mhe. Waziri anieleweshe katika huu ukaribu wake tumepata vipi 4.5 kwa kila mwaka gani na kila mwezi gani. Je, tunaipata inakamilika? Haya ni mambo Mhe. Naibu Spika, ni lazima tuyaseme, wanatutia uchungu, kwa sababu ukikosa 4.5 kwa mujibu wa utaratibu wetu Mheshimiwa mambo yetu mengi yanapotea. *Program* uzetu za kichukumi zinakwenda ovyo tutakuwa tunasema uongo tu kila siku.

Sasa hili nimeona nianze kulisema wazi kabisa watu waelewe jinni Mshimba anavyotetea muungano uwepo na jinsi gani Mshimba anavyotetea muungano kasoro zake ambazo zinamantiki kwa mujibu wa Wazanzibari. Hiyo ni lazima Mheshimiwa tuseme.

Mhe. Naibu Spika, nikenda katika ukurasa wa 215 Bodi ya Mapato *ZRB*, Mheshimiwa nawashukuru sana tena sana. Hii *ZRB* kama ingelikuwa kama tungesema kodi zote wachukue wao basi nafikiri hapa Zanzibar ingekuwa tuna uchumi mzuri. Ni muda mdogo tu tuangalie sasa hivi ina jitahidi kabisa katika ukusanyaji wake. Lakini bado kuna sehemu nyengine nataka niwambie waendeleze kutia mkazo.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana Kamishna Mkuu na Kamishna Mtendaji pamoja na watendaji wake wote, ni watu ambao mahiri, wanafatilia vizuri. Lakini vile vile nataka niwambie kwamba sasa tusimuonee haya mtu katika kutokumpiga mtu *penalty*, katika kumpandisha mtu juu Mahakamani ili mapato yazidi kuendelea. Naamini ile kitu wanafanya vizuri, naamini kabisa hawana mzaha. Maana ukizubaa tu kama ukifika muda wao hujalipa, karatasi ya onyo inakuwepo.

Mimi nawaomba sana Mhe. Naibu Spika, hii *TRA* ambayo inatubugudhi kila leo wapewe wao kodi hizo wakusanye. Tusiwape tena *TRA* Mheshimiwa tumesema zamani kwamba hatuitaki. Ninaomba sana wapewe wao kama ni sehemu ya pili ya ukusanyaji wa upande huo lakini jina litumike hili hili *ZRB*.

Mimi ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri jitihadi sana kwa suala hili. Hawa wanaweza, wanakusanya mapato yanayopitikia katika muda ambao tumeuweka, wanapindukia na kupindukia sana, kutokana na hitihada zao walivyojipanga vizuri. Ukitizama *TRA* patolao linakuwa ni dogo zaidi kuliko wao, asilimia kubwa ni wao *ZRB*. Mimi ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, kuwa hizi kasoro ambazo tunaziona sasa hivi tuzirekebishe haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 18 Mfuko wa Barabara, mfuko huu unatusaidia kwa hivyo naomba sana uendelezwe na asilimia ipandishwe kidogo ili iweze kufanyiwa kazi vizuri katika kusaidia majimbo yetu. Naomba sana kuna barabara yangu moja Kitope na pale Kinduni, ile barabara ni ya siku nyingi sana, naomba sana waimalizie ili wananchi waendelee kunufaika na mfuko huu. Walijitahidi lakini kwa bahati mbaya kulitokezea mambo ya hapa na pale. Nawaomba sana mfuko huu uongezwe ili tumalizie haya mabakaa yaliyobakia katika majimbo yetu.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika sehemu ya 35. Hapa *ZIPA* kwanza niwashukuru watu wa *ZIPA* tena sana. Mhe. Naibu Spika, watu wa *ZIPA* wamejipanga vizuri katika shughuli zao za kila siku, mimi nakubaliana nazo. Changamoto ambazo zinawafika za hapa na pale nazo nakubaliana nazo. Lakini ninachoomba *ZIPA* sasa hivi ni sehemu ya uti wetu wa mgongo na wao. Katika sehemu ya uti wa mgongo ya kutafuta uchumi ni pamoja na *ZIPA*. Kule kuna Hoteli ya *Venta*, hii sasa hivi watu wameona hawana cha kuiba sasa wanaiba matofali wanavunja zile nyumba.

Nawaomba sana hetu jamani, tukalihami lile boma. Mara moja mimi nilitoa wazu zuri tu kwamba kuna watu wanadai sasa basi hebu utuwagaie zile nyumba kuliko kuharibiwa sasa hivi. Imekuwa pesa zao hawazipati, wengine wameshapelekwa Mahakamani. Mimi naomba sana Mhe. Waziri kama hamuyataki yale magofu wananchi wapewe kule, wananchi wa Kiwengwa wanadai pesa chungumzima, habu wapeni zile nyumba, wapewe mmoja mmoja zitakidhi haja na wao wataweza kukodisha watarudisha pesa zao. Lakini kwa kweli ni aibu.

Tulikwenda siku moja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Haki ya Mungu, tuliona jinsi gani nyaya za umeme zilivyotolewa, milango, vitanda. Leo tunakwenda kuiwacha hivi jamani, ituume ile ni haki yetu, lakini tunaacha. Hali halisi sasa hivi katizameni, hasara tupu. Tunao wazalendo hapa wa Kizanzibari wana uwezo wa kuendesha hoteli kama zile, hebu tuwapeni basi. Tumekuwa kama joka la mdimu, maana yake joka la mdimu yeye hali ndimu na hataki mwengine achume, ndio maana yake hiyo. Sasa ndiyo ile hoteli hatima yake, hebu twendeni tukatizameni hali halisi ilivyo. Jamani lituume hili suala kwa sababu tumekosa ajira kwa wananchi wetu, wanahangaika mitaani wanakwiba tu kila siku, zogo limekuwa kubwa mitaani. Mhe. Waziri mimi naomba sana na hichi kitengo chako hebu nendeni kabisa mkaone.

Jengine, hivi sasa linataka litokezee zogo kubwa sana na mimi nasema lisitokezee. Kuna muwekezaji ambaye sasa hivi anataka kuwabugudhi wananchi wetu wa Kiwengwa. Naomba sana hili tulichukulie hatua, mwekezaji huyo walikubaliana na vijana suala la Uwanja wa Mpira. Sasa hivi amewakanusha vibaya vibaya ana amesema hatoukenga ule uwanja kwa vile alivyokubaliana nao. Ataujenga kama ni *simple* tu wakati sivyo alivyokubaliana nao. Vijana wamehamaki, jana wameniletea barua miye wao wako tayari kufanya la kufanya.

Mimi nitawaunga mkono kwa sababu mtu ardhi zao ni haki yao wanafikwa pahali wanadhalilishwa na wazee wao, wamenifuata nyumbani saa 12 za jioni wanakuja wazee kulalamika. Hetu mimi naomba sana kitengo hiki kihusike, kishuke chini kikae pamoja na muwekezaji, sasa hawamtaki hata huyo muwekezaji. Nimeangalia mimi sehemu ya mkataba wake alipoji *commit* mwenyewe, hana ruhusa ya kufanya jambo la aina yoyote kama hajafanya uwanja mbadala wa juu. Lakini sasa hivi keshatia uzio wa makuti.

Sasa naomba sana na hili Muheshimiwa tusiongeze tu matatizo, nawaomba sana watu wa *ZIPA* washuke kule chini. Tena mimi nawaamini sana Mhe. Naibu Spika, kwa mambo kama haya ni mujarabu sana. Mimi sina historio nao mbaya, mara nyingi sana katika asilimia nawapa 100% au 99%, kesi nyingi wanazitatua masuala kama haya. Sasa na hili nawatwisha mzigo nao waendelee kuwatatulia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, sio huko upande wa pili naingia na upande mwengine. Naomba sasa hivi kuna wimbi la wawekezako wetu kufutiwa hati zao. Hili nalo nawaomba sana watu wa zipa, twendeni katika Sheria mnazozijua nyiye. Mimi niliwauliza swali watu wa *ZIPA*, wakasema sisi taratibu yetu kama ni sisi tukitaka kuwafutia watu mradi lazima tunatoa *notes*, tunamwambia yule mtu mwenye kuweka mradi kwa nini mradi wako tusikufutie. Kwa hivyo, yeye anajibu na *ZIPA* wanakaa kitako wanakubaliana nao au wanapanga njia ya kuweza kuwasaidia.

Hili wimbi sasa limekuwa kubwa, tunawafutia tu kiholela, nalo hili tunaomba sana Mheshimiwa, wasizubae tu kwa kunyamaza kimya. Sheria wanazo *ZIPA*, hebu awafanyie kuwasaidia hawa na wao. Kuna watu wameshajenga magofu yao lakini mpaka leo yamekwama. Kule kwao nje wanadaiwa pesa chungumzima, wakishindwa suala hili basi ina maana hichi kitengo kisiwepo hakina maana kuwepo. Kwa sababu wao ndio wasuluhishi na wao ndio wenyewe wale.

Namuomba sana Mhe. Waziri hili suala nije kupewa jibu. Vyenginevyo kifungu nitakizuia mimi hichi. Shemeji niwie radhi kwa hili, nataka uchumi wa maendeleo wa nchi yetu. Tukisema tungoje pesa za kupewa hatupewi, ziko wapi? Hatuzipati kabisa. Sasa naomba sana Mhe. Naibu Spika, hili suala ulifatilie kweli kweli, shuti uwe na *good plan*, kabisa. Uwe na *plan* ya kuwa *please* wale wawekezaji, kabisa waridhike, vyenginevyo hatuwapati tena hawa. Tunakwenda kuwatafuta nje, tukishakuwaleta hapa tunakuja kuwabirua, nini maana yake.

Mimi hili suala sikubaliani nalo, niko *very serious* kwa suala kama hilo kwa sababu tunakosa uchumi. Hichi si kitu cha mchezo, hili nalisema wazi. Ndio maana hufika pahala watu wengine wanakuwa hawanifahamu, nikisema miye kwamba hebu tujaribuni kutupa na sisi tuone kama hatukuiletea nchi hapa maendeleo. Naamini tutaifanya Zanzibar itakuwa njema atakae aje, na watakuja kwaraha kabisa na kuwekeza. Kwa sababu nikiwepo miye pale nitakuwa naweza kusema vizuri. Mheshimiwa kifungu hichi cha Mipango na Sera nakisema tu lakini baadaye hichi kama sikupata jitu nitakuja kukuzuia hapa.

Mhe. Naibu Spika, katika mfuko wa *ZSSF* hapa nataka niingie, kwanza nawashukuru sana na wamo katika mikato mizuri. Lakini nataka kuwaomba Mkurugenzi Muhusika asione tabu kuzitumie zile fedha kwa kuwasaidia hawa wadau wake. Kivipi basi? Mheshimiwa wangu Mwenyekiti, alisema kuwa hebu tuwajengeeni nyumba za mkopo nafuu nimeona katika *business* hiyo. Tuiingia katika mambo haya ya Serikali kutafuta *contract* haya tuiingie nao. Vyuo hivi tusimamie sisi fedha wanazo sasa naomba sana watanue wigo wa kuweza kuuchangia zaidi ya kupata hizi fedha.

Sasa namuomba sana Mheshimiwa Mkurugenzi akae na wataalamu, wasichelewe maeneo yapo kibao huko ya kujenga nyumba za mkopo nafuu. Mtu leo anastaafu mshahara wenyewe mdogo lakini wakiwajengea nyumba mtu akistaafu anajua kwamba ile nyumba imeshakuwa yake fedha nyengine za kiinua mgongo atafanya biashara zake.

Hili tusilifumbie mamcho, kama hawana wataalamu wapo wataalamu kibao wa biashara akina Mhe. Mazrui awaite akae nao, mtaalamu wa majenzi atawambia *instrument* zao nyumba atawambia nyumba moja itasimamia kiasi gani na mtu unaweza kumkopesha kwa kiasi gani. Naomba sana wasaidie.

Lakini katika sheria hizi watuletee tuzibadilishe muda umeshakuwa mrefu na hasa kwenye Mahoteli, mtu akifanya kosa kidogo tu kwa muda wa mwezi mmoja keshafukuzwa kazi na kule anakuwa keshachangia. Ile ni moja ambayo mimi sifurahiki nayo.

Naomba sana sheria tujaribu kuiboresha ili tuwe na muda mchache mtu aweze kupata haki yake au tutafute mbinu nyengine. Kuna wengine bado hawajafikia kuleta *ZSSF*, hawataki wale matajiri wao. Hebu naomba Mkurugenzi afanye *team work* ya makusudi wapitie katika zile sehemu ambazo kuwa wabahili kutaka kupeleka zile fedha. Na wao kule wawapige *penalty* wawashtaki, wasiwaachie hawa. Kwa sababu wale wengine wanakuwa hawapati mafao yao vizuri.

Suala hili nililisema sana hasa katika sehemu ya Miperani kule. Nawashukuru sana wale watendaji, walikuja vizuri sana lakini *feed back* yake sijui ikoje. Mhe. Waziri utatusaidia kama walifanikisha vizuri, fedha zao zinakwenda kwa utaratibu watu wa Miperani kule Kitope. Naomba sana na hilo nisaidiwe.

Halafu la pili nawaomba sana wanapokuwa katika kutaka kujenga kitu wawatumie wale wataalamu wa Michenzani. Tena namuomba sana Mkurugenzi wangu, atakapokuwa anataka kujenga jengo la aina yoyote lazima wale wawemo mmoja. Kwa sababu wale ni watu wataalamu, naomba ajaribu kuwaita wale ku-*contract,* ili mambo yake yaende kwa uzuri kabisa. Namuamini sana Mkurugenzi wangu huyu anafanya kazi vizuri sana na msikivu, *Alhamdulilah* Mwenyezi Mungu amzidishie.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa mwisho kwa kuchangia ni ukurasa wa 51 unaozungumzia *PBZ* ya Watu wa Zanzibar. Hapa mimi ninakilio kidogo. Kilio change mimi wajibu wangu niseme. Pale panatoka ajira nyingi sana lakini huwa nashangaa na hasa sisi Wawakilishi sijui tuna bahati gani na sisi.

Mhe. Naibu Spika, tunaposikia ajira na sisi tunapeleka watu wetu ambao tayari wana level zile kama vile za wengine. Lakini ukenda kule unaambiwa kuna wakubwa zaidi wameshaleta watu wao pale. Sasa sisi tuna maana gani? Mimi nilikuwa niseme hapa tuunde tume, nina wasi wasi sana pengine wamepelekwa watu waliokuwa sio, hawana sifa zinazotakiwa. Lakini kwa kuwa Wizara hii ya Swahiba wangu anaweza akanipa jibu zuri bila ya kumuundia Kamati Teule.

Mhe. Naibu Spika, zaidi ya mara tatu shahidi mimi mwenyewe kila nikipeleka mtu wangu anapigwa *disco*. Kwa hivyo, kijana yule ana *experience* nzuri lakini kwa nini sisi tusipewe kama ni wawakilishi wa wananchi. Mhe. Naibu Spika, kwa hilo namba na sisi watufikirie. Lakini katika utendaji wa benki ile sasa hivi imefika katika kiwango kizuri sana, nawashukuru sana na tunajivunia kwamba sasa tuna benki.

Sasa inaingia katika mtandao wa kimataifa, inajinafasi inafungua sasa hivi matawi mengi mengi. Ni moja katika sifa nzuri, ukiwa na mbawa refu unaonekana kwamba wewe ni mahiri unaruka vizuri sana. Sasa benki hii *Alhamdulilah*, namshukuru Meneja Mkuu kwa jitihada zake pamoja na watendaji wake, maafisa wake wote na Meneja wamo katika hali nzuri na ni wasomi wazuri ni wachumi wazuri.

Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe ushauri wangu katika Benki hii. Ushauri wa kwanza hebu tufungue benki ya akina mama, hebu waunde na wao tuone jinsi gani inawasaidia sasa hivi akina mama katika kuwaondolea umasikini. Lakini hata hizi *society* ndogo ndogo na wao wanajitahidi ili ikae vizuri kuwaona na wao kuwasaidia kama benki za wenzetu kule Bara. Wenzetu Bara kule sasa hivi Benki zile wanasaidia akina mama ntilie, wanawasaidia watu wenye miradi midogo midogo. Kwa nini na sisi tusiingie katika sehemu hizo.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie sasa hivi katika jimbo la kitope, sasa hivi taaluma za kihisia wanazo lakini sio taaluma zenyewe za *qualification* zinazotakiwa. Wana-*SACCOS*, wana visanduku hivi, wana mambo chungumzima.

Sasa nawaomba sana watufanyie semina kwenye majimbo yetu ili kwa kuweza kuwasaidia wale watu kuwakopesha zile fedha na kuweza kurudi. Wanaweza kufanya vitu kama hivyo. Kwa sababu wana visanduku na inafika baada ya muda wanagawana laki mbili mbili. Na hiyo hawana taaluma basi tu. Sasa na wao wajipange vizuri, tulipokosea tujirekebishe. Maana ule mfuko wa AK na JK sijui umeishia vipi. Kwa hiyo nawaomba sana mfuko ule usitufanye kama tumefeli isipokuwa sasa tujipange vizuri tuwasaidie wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache niseme kuwa nikushukuru sana Mhe. Naibu Spika, naomba mkono asilimia mia kwa mia hotuba hii ya Mhe. Waziri, shemeji yangu, Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante na sasa nafasi tunampa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na muda ukibakia tutampa Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili, matatu katika Wizara hii ya Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mengi sana ya kuzungumza katika Wizara hii hususan ilivyokuwa wizara hii iko chini ya Kamati ambayo mimi ni mjumbe na kazi kubwa tayari tumeshaifanya kazi kamati. Kwa hivyo, hivi sasa tunajazia jazia tu mule ambamo mulimobakia.

Kwanza nianze kwa kutoa shukurani. Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na Kamati yake yote ya watendaji ambayo iko ndani ya Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kazi kubwa na nzito ambayo wameifanya kwa umoja wao hadi leo hii kuweza kufikia pahala tukaweza kuwasilishiwa bajeti ya Wizara hii, ikiwa na mambo lukuki ndani yake.

Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na timu yake kwa kazi nzito waliyoifanya ya kuhaulisha vifungu kutoka katika Wizara tofauti na hatimaye kuzikusanya pamoja na katika Wizara ya Fedha na Uchumi na kuweza kupata shilingi bilioni 17,166,560,250/= fedha ambazo Wawakilishi wa Baraza hili Tukufu la Wananchi wa Zanzibar, waliona kwamba hazina matumizi. *(Makofi)*

Kwa kweli matumizi ambayo yangeliweza kuwasaidiwa wananchi wa Zanzibar na wakafanya utaratibu wa kuweza kuonesha njia kwa Mhe. Waziri na yeye kuweza kufanya kazi hiyo ya kutoonesha idadi ya fedha nyingi kama hizi ambazo zilikuwa zinaweza kutumika na baadaye majawabu yake hapa yangekuwa yakutatanisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumuomba Mhe. Waziri pamoja na taarifa hii ambayo ametuletea, kwa kweli taarifa hii imetengenezwa kitaalamu mno na umekuja katika utaratibu wa mafungu. Kwa hivyo, tumuombe Mhe. Waziri wakati atakapokuja hapa atusaidie ufafanuzi wa kila Wizara zimeweza kupunguziwa kima gani cha fedha, ili tuweze kufahamu kila wizara imechangia nini katika utaratibu huu wa kukusanya mapato ya serikali kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nianze na mchango ambao niliutoa mwaka jana. Mhe. Naibu Spika, wakati nilipokuwa nikichangia bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mwaka 2011/2012 Mhe. Waziri nilikuwa na maombi juu yako, katika suala zima la hawa ndugu zetu ambao wanaendesha magari ya kupakia watalii.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na juhudi zile na maelezo yote ambayo tumeyatoa katika kipindi kile bado tatizo la watu wenye magari ya kuchukulia watalii bado linaendelea. Kwa kweli hawa watu pamoja na kukata leseni, lakini bado wanataka kupakia watalii wanaendelea kubughudhiwa na kutakiwa kukata vibali maalum, ili waweze kufikia safari ambazo zinalengwa.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba suala hili katika bajeti hii ya mara hii atupe mwelekeo rasmi ambao utakuwa unaeleweka na kufahamika juu ya suala hili na hawa tayari tumeshawapa leseni za kubebea watalii, sasa imehusu nini sasa kuja kutafuta maeneo mengine ya kuja kulipa wakati tayari leseni zao kwa ajili ya kupakia watalii.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi naomba anipe maelekezo ambayo nitayafahamu katika suala kama hili.

Pili wakati nilipokuwa nikichangia mwaka jana niliulizia suala zima la *Hotel* ya Mpapindi pamoja *Venta Club*, jawabu lake Mhe. Waziri kwa kipindi kile alielezea kwamba kuna ripoti ambayo unausubiri itatoka kwa Makamu wa Pili wa Rais, ili iweze kutoa mwelekeo wa kuweza kujua hatua gani zichukuliwe, kwa ajili ya kuweza kufikia mustakbali wa hoteli hizi mbili. Mhe. Naibu Spika, mwaka umepita.

Matatizo ya Mawasiliano Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea nakuja katika tatizo sugu la Zanzibar na Dar-es-Salaam juu ya suala zima la mizigo ambayo inahaulishwa kutoka eneo moja la Muungano kwenda eneo jengine la Muungano.

Pamoja na melekezo mazuri ya ufafanuzi ambayo amefanya Mhe. Waziri wakati tulipokuwa tunapitisha bajeti ya Biashara, Viwanda na Masoko. Lakini bado wazanzibari wanakaa katika njia panda na kutojijua, sababu zipi za

msingi zinazosababisha bado tunashindwa kulitumia soko la Dar-es-Salaam katika kuhaulisha mzigo kutoka eneo moja la Muungano kwenda eneo jengine, hususan ukitilia maanani sheria zote za *TRA* hazimfungi mfanyabiashara wa Zanzibar kuondosha mzigo eneo moja la Muungano kuelekea eneo la pili la Muungano. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja hapa atupe jawabu ambalo litaweza kuwasaidia na kuwapa faraja wazanzibari wanaoendelea kuathirika na tatizo ambalo linasababishwa na watu wachache tu.

Kwa mfano, tukiangalia vikao ambavyo vinakwenda kukaa juu tunafika pahala na tunakubaliana, tatizo hili limeisha wazanzibari wapitishe mizigo yao, waende bila ya usumbufu wa aina yoyote, kwa sasa kuna *limit* maalum ambayo imepangwa mpaka shilingi milioni 3 mzanzibari anayeondosha mzigo eneo moja kwenda eneo jengine asibughudhiwe. Lakini ndugu zetu wanaondoka na vyombo hata usiku bado wanapata kadhia na matatizo yasiyokuwa na maana.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa sababu nimetokea katika taasisi hii pia nashindwa kuelewa mpaka dakika hii, ni sababu zipi zinazosababisha yule mtu ambaye amewekwa katika Kitengo cha *Wharfage* kuwekewa makisio ya ukusanyaji wakati uwezekano wa kuondosha mizigo baina ya Bara na Zanzibar ni kuweka takwimu sahihi na wala hakuna makusanyo kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wakati atakapokuja hapa naomba atusaidie, ili tuweze kupata ufafanuzi juu ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupatie maelezo juu ya suala zima la *exemption* ambazo tumezitoa kwa mwaka 2011/2012. Vile vile pamoja na *exemption* hizo tunaomba utuelezee faida iliyopatikana au itakayopatikana baada ya kutoa *exemption* hizo ndani ya nchi yetu ya Zanzibar.

Suala jengine lilikuwa ni kuhusu Visa lakini nitashindwa kulitolea ufafanuzi kwa sababu taarifa zake sikuweza kuzipata kwa ukamilifu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka kuchangia katika siku ya leo hii ni kuhusu magendo ya mafuta. Kwa kweli bado Serikali yetu ya Zanzibar inapoteza mapato mengi katika magendo ya mafuta. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atusaidie kutuelekeza ni mikakati gani wizara yake imetengeneza kwa ajili ya kupambana na magendo ya mafuta ndani ya Visiwa vyetu vya Zanzibar kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Vile vile ningelipenda niwapongeze ndugu zetu hawa wa *PBZ* kutokana na kazi nzuri ambayo yanaifanya chini ya usimamizi wa Menaja wao ndugu yetu Amour Juma, ambaye ameweza kufanyakazi kwa malengo ambayo Mhe. Waziri yale ambayo ulikuwa umeyakusudia na umeyataka, kwa sababu benki hii kwa taarifa tulizonazo ilikuwa imefikia pahala na kuonekana bora ifungwe. *(Makofi)*

Lakini chini ya usimamizi wako Mhe. Waziri ukaweza kutoa maelekezo pamoja na Kamati ambayo iliundwa na sasa katika usimamizi wa Meneja ambaye aliyenaye wamefanyakazi vizuri na makusanyo yao ni mazuri mno yanaridhisha na wanastahiki kupewa pongezi. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu pia napenda kuchukua fursa hii kutaka kuelewa pia Mfuko wa Barabara katika mwaka uliomalizika wa fedha 2011/2012, ilikuwa imekuja kuomba katika Wizara ya Fedha kiasi gani cha fedha na imepewa kiasi gani na kama ikiwa fedha hizo ambazo walizoomba hawakupewa kwa kiasi ambacho wametaka ni kwa sababu zipi? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kumuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze ni sababu zipi zinazosababisha, kwamba hadi leo hii bado tunaendelea na utaratibu wa kukusanya Mapato ya Serikali katika Vyanzo vya Mapato kwa kutumia utaratibu wa kuandika risiti kwa mkono kama tunavyoendelea.

Hivi kwa nini mpaka leo hatujaweza kutumia vyombo vya *electronic* na tukaweza kukusanya mapato, ili taarifa zikawa zinapatikana kila upande na kila pahala tena taarifa hizo zikawa za uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja hapa atueleze kuhusu tatizo linaloikabili suala zima la hizi *ATM* kutokufanyakazi katika mabenki ambayo yako hapa nchini petu. Kwa mfano, Benki ya *PBZ, NBC na NMB*, mara nyingi sana ukienda katika *ATM* hizi na hususan siku za *weekend* ambapo ndio wakati hasa tunaokusudia kuzitumia *ATM* hizi na tukifika huwa hazifanyikazi, yaani zina matatizo ya hapa na pale. *(Makofi)*

Baada ya maelezo haya mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kikwajuni, naomba kuunga mkono bajeti ya wizara hii. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi jioni hii kupata nafasi ya kutoa mchango mdogo juu ya Wizara hii ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia kumshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha kwake vizuri hotuba yake hii ambayo Wizara ya Fedha pamoja na mambo mengine yote ndiyo mama wa wizara zote, bila ya fedha yote tuliyoyajadili mwanzo itakuwa hayana maana kwa sababu itakuwa hayatendeki.

Waziri wa Fedha sijui teseme mama au baba lakini ndiye mkubwa wa mambo yote, bila ya yeye matumizi yetu itakuwa hayapo. Kwa hiyo nimpongeze sana kwa maandalizi yake mazuri haya na nafikiria kuwa ataweza kuziwezesha Wilaya zote ili ziende kama zinavyotakiwa ziende bila ya kuzikwamisha kwa kuzikosesha fedha.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu utakuwa mdogo na nitaanzia kwenye mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kama unavyojieleza wenyewe kuwa ni mfuko wa Hifadhi ya Jamii lengo lake ni kutoa hifadhi kwa jamii zaidi ya kufanya kazi na hatimaye wanapostaafu.

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi huwa wanachangia asilimia 6 ya mishahara wao katika mfuko huu. Muajiri na yeye kadhalika huwa anatoa sehemu fulani kupeleka katika mfuko huo. Lakini hutokezea baadhi ya waajiri ama wakachelewa au mara nyengine kutopeleka kabisa mchango wao kwa yule mfanyakazi muhusika. Hatimaye anapostaafu mara nyengine anakutia alichoweka ni kile tu alichochangia yeye mwenyewe.

Ningemuomba Mhe. Waziri na wafanyakazi kwa jumla mara kwa mara wawe wanapita katika chombo hichi ili kuhakikisha waajiri wao ule mshahara wao unafika ili huko mbele wasije wakaathirika.

Mhe. Naibu Spika, mfanyakazi anapostaafu ndio haki hii anaipata, lakini je, tujaalie pale mfanyakazi kwa njia moja au nyengine ama kafukuzwa kazi au kaacha kazi kabla ya umri wa kustaafu kwa nini ikawa kile alichoekeza hapewi ni haki yake. Lakini mara nyingi kama kafukuzwa kazi au kaacha kazi yeye mwenyewe mapema kabla ya umri huwa mfuko huu unamtaabisha sana. Kwa nini wakati kile alichoweka ni haki yake yeye mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, jengine niupongeze mfuko huu unaanzishwa mpango wa kujenga nyumba kwa bei nafuu ambazo nadhani wafanyakazi na jamii wataweza kuzitumia hii ni kuwasaidia wafanyakazi na jamii kupata maisha bora katika nchi yao. Kadhalika wazo la kuweza kuufufua uwanja wa uhuru wa Kariakoo ni wazo zuri. Pale hivi sasa fedha ya serakali inapotea bure, uwanja uliwanja kwa madhumuni ya kufurahishia watoto, karibuni huenda pakawa msitu pale. Kama katokezea mfadhili huyu wa kuushughulikia huo uwanja mimi nitampongeza na nitafurahi kama nitauona uwanja ule unafanya kazi mapema iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuhusu Benki ya Watu wa Zanzibar. Benki ya hii ni ya kibiashara na pia ya kihuduma. Lakini kwa kuwa hii ni Benki ya Serikali ningeomba Benki hii huduma zake ziwe bora zaidi ili kwenda na ushindani wa Benki ambazo zimeingia Zanzibar kuwavutia wateja wengi waekeze rasilimali zao katika Benki hii ya Zanzibar ili iweze kutoa huduma na kutudaidia Wazanzibari kupata mikopo ya kuweza kutuendesha katika shughuli zetu za kimaisha.

Pia niipongeze kwa kukufungua matawi ya Benki ya Kiislamu ndani yake ambayo itaweza kuwasaidia Waislamu kuwekeza bila ya riba yoyote na kupata mikopo kutokana na Benki hii.

Mhe. Naibu Spika, jengine niipongeze Serikali na nimpongeze Waziri kwa kuandaa mpango mahasusi wa kutafuta fedha za kuweza kupata meli mpya ya usafiri wa abiria. Hiki ni kilio chetu cha siku nyingi, ni vyema tupate meli ya serikali ya usafiri baina ya visiwa vyetu na hata ndugu zetu wa Tanganyika ikenda si vibaya, lakini zaidi baina ya Unguja na Pemba. Meli za watu binafsi iwe ni kama visaidizi tu lakini isiwe moja kwa moja tunawategemea wao.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na wazo zuri la serikali lakini bado inahofu kwa sababu serikali si dhani kwa hizi pesa Mhe. Waziri alizozitengua kwa hapa na pale kuwa zinatosha kwa ajili ya kununua hizo meli. Je, kama fedha hizi hazitoshi hizi nyengine ili meli ipatikane zitatoka wapi. Na serikali huko nyuma ilikuwa imeshatangaza rasmi kuwa haina pesa ya kununua meli, lakini baada ya ajali hii na kwa bahari mbaya ikatokezea kuna mmoja ni raia wa kigeni mzungu, ndio maana serikali ikafanya vyovyote vile tupate meli. Kwa hili Serikali naipongeza na naomba ifanye juhudi ili meli hii ipatikane.

Mhe. Naibu Spika, huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani na wafanyakazi wanaingia katika Sikukuu ikiwa mwisho wa mwezi uko mbali sana. Kile walichopata chote wameshakitumia ndani ya mwezi wa Ramadhani. Ningemuomba Mhe. Waziri afanye mpango kwa yote, wafanyakazi awalipe kabla ili wapate Sikukuu. Ingawaje ni mapema mno lakini Waziri husika wa Utumishi wa Umma ajipige pige mifuko yake ili wafanyakazi awawezeshe mapema. Haidhuru mwezi ujao utakuwa ni mkubwa lakini hapa atakuwa amewaokoa pazuri.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha maana naona muda uliobaki ni mdogo naomba nitoe tangazo kwamba kesho tarehe 8/08/2012 tutaendelea na semina yetu ya kuhusu elimu ya Katiba saa 2:30 watu kujiorodhesha, saa 3:00 tunaanza Semina Ukumbi wa Juu wa Baraza la Wawakilishi. Baada ya tangazo hilo sasa naomba niakhirishe Kikao chetu hichi hadi siku ya Alkhamis tarehe 9/8/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 9:00 Jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 9/08/2012 saa 3:00 asubuhi)